

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Pili – Tarehe 6 Novemba, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevyia ya mwaka 2018.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi robo ya kwanza 2019/2020.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Katibu.

NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mashimba Ndaki sasa aulize swali kwa niaba ya Mheshimiwa Makame Mashaka Foum.

Na. 14

Sheria Na.9 ya 2010 ya Watu Wenyewe Ulemavu

MHE. MASHIMBA M. NDAKI (K.n.y. MHE. MAKAME MASHAKA FOUM) aliuliza:-

Sheria Na.9 ya mwaka 2010 ya Watu wenyewe Ulemavu imemeanisha haki za msingi za Watu wenyewe Ulemavu ikiwa ni pamoja na haki ya ukalimani katika maeneo ya utoaji huduma kama vile hospitali, taarifa ya habari, shuleni nk:-

Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuharakisha utekelezaji wa sheria hii?

NAIBU SPIKA: Majibu, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE WALEMAVU (MHE. STELLA IKUPA ALEX) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Makame Mashaka Foum, Mbunge wa Kijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Watu wenyewe Ulemavu Na.9 ya mwaka 2010, imeweka misingi ya upatikanaji wa haki kwa watu wenyewe ulemavu ikiwepo haki ya upatikanaji wa habari kwa kundi la viziwi kuititia wakalimani katika sehemu mbalimbali ikiwemo hospitali, shuleni pamoja na vyombo vyaya habari yaani luninga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kuweka mikakati ya kuwa na wakalimani wa kutosha wa lugha ya alama kwa kuanzisha programu ya mafunzo ya lugha ya alama katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuititia Mradi wa LAT (Lugha ya Alama Tanzania). Chuo kimeandaa mwongozo wa mwaka 2019 wa majaribio ya kufundishia na kujifunza Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa kutumia Lugha ya Alama ya Tanzania kwa darasa la awali, la kwanza na la pili. Aidha, imeandalowi kamusi ya lugha ya alama na machapisho mbalimbali yanayotoa mwongozo wa namna ya kujifunza lugha hiyo kwa lengo la kuongeza wakalimani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza kundi kubwa la wakalimani na watumiaji wa lugha ya alama, Serikali imechukua hatua ya kutumia lugha ya alama kama lugha ya kufundishia na kujifunzia shulenii. Aidha, kufundisha lugha ya alama kama somo mojawapo katika shule na vyuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuititia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kilele cha Wiki ya Viziwi iliyofanyika katika Manispaa ya Iringa alitoa maagizo kwa vyuo vya elimu ya juu na kati kuweka mtaala ambao utawezesha wahitimu kusoma lugha ya alama kama somo la lazima katika masomo yao (*compulsory subject*). Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliagiza vyombo vyote vya habari kuwa na wakalimani wa lugha ya alama katika vipindi vya luninga zao.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa sasa lugha ya alama inatumika kwenye chombo kimoja tu cha *TBC* lakini *TV stations* zingine hazina ikiwa ni pamoja na *TV station* ya hapa Bungeni. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba *TV stations* karibu zote zina wakalimani na watafsiri wa lugha ya alama? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA

MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipongeze pia maswali ambayo yamejibowi na Naibu Waziri lakini kama ambavyo swalii limeulizwa kwamba sisi kama Serikali tuna mpango gani katika kuhakikisha kwamba vyombo vyote vinatoa huduma ya ukalimani kwa watu ambao wana tatizo la ulemavu, sisi kama Serikali ambao tumekuwa tukisimamia masuala mazima ya habari, kwa upande wa *TBC* ni wazi kwamba tumeboresha na sasa hivi tuna wakalimani zaidi ya wanne na vipengele vyote muhimu ikiwepo taarifa ya habari na vipindi maalum, wakalimani wa lugha za alama wamekuwa wakitoa hizo tafsiri. Ni takwa la kisheria kuwa na wakalimani na sisi kama Wizara ambayo tunasimamia masuala ya habari tumekuwa tukisisitiza kwamba vyombo vyote vya habari vikiwepo vyombo vya umma pamoja na binafsi vihakikishe kwamba vinakuwa na wakalimani wa lugha za alama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wamiliki wote wa vyombo vya habari kuhakikisha kwamba wanatekeleza takwa hilo la kisheria kwa kuwa na wakalimani wa lugha za alama. Nashukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watu wenye ulemavu wamekuwa wakipata shida sana wanapokwenda kutibiwa katika hospitali zetu kwani kumekuwa hakuna mawasiliano kati ya daktari na mtu mwenye ulemavu kwa sababu ya daktari kutojua lugha za watu wenye ulemavu. Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaweuka mkalimani kati ya daktari na mtu mwenye ulemavu ili aweze kutibiwa kile ambacho anatakiwa kutibiwa?

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu wenye Ulemavu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA IKUPA ALEX): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa suala ambalo ameliuliza Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi kwamba tuna upungufu wa wakalimani wa lugha ya alama. Wizara ya Afya ilishatoa maelekezo kwamba kwa kuwa sasa hivi tunajiandaa na tunawaandaa wakalimani wa lugha za alama basi watu wenye ulemavu wanapoenda hospitali waruhusiwe kwenda na watu ambaa wanawaamini ili mawasiliano yaweze kufanyika vizuri kati ya mtu mwenye ulemavu na daktari ama na mtu anayemhudumia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh, swalii la nyongeza.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa kitu chema kinaanza nyumbani basi napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwa nini lugha ya alama haianzii hapa Bungeni pale juu tukawa na mkalimani maana hii haioneshi kwamba kweli tunataka mabadiliko kwa sababu Bunge lilitakiwa liwe mfano? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu wenye Ulemavu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA IKUPA ALEX): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Ally Saleh, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wapo wakalimani wa lugha ya alama wawili. Hata sasa hivi tunavyozungumza haya yanayoendelea hapa yanatafsirwa kwa lugha ya alama. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khadija Nassir.

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Tanzania ni nchi wanachama wa *UN* na tuliridhia na kusaini Mkataba wa Haki za Walemavu. Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kupeleka Ripoti ya Utekelezaji wa Haki za Binadamu *UN* ili sasa tuweze kuona *way forward* ya wenzetu ambao wana ulemavu? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu wenye Ulemavu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, WATU WENYE ULEMAVU (MHE. STELLA IKUPA ALEX): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Khadija Nassir, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kweli iliridhia Mkataba huu wa Kimataifa na inatambua kwamba iko haja sasa ya kupeleka *UN* Ripoti ya Utekelezaji wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu. Ripoti hii inaandaliwa, ipo kwenye hatua za mwisho na karibia itawasilishwa. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Kuteuliwa.

Na. 15

Mwaka 2019 Kuwa Mwaka wa Uwekezaji Tanzania

MHE. ANNE K. MALECEL A aliuliza:-

Tarehe 8 Machi, 2019, Mheshimiwa Rais Dkt. John Magufuli, alipokuwa ikulu kwenye dhifa ya Mabalozi wanaowakilisha nchi mbalimbali Duniani aliutamka mwaka 2019 kuwa ni mwaka wa uwekezaji: -

Je, Serikali imejipangaje katika kutekeleza tamko hilo muhimu sana?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI)
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Kuteuliwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mipango na mikakati mbalimbali inayolenga kuhakikisha tamko la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alilolitoa katika dhifa ya Waheshimiwa Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa Tanzania, la mwaka 2019 kuwa Mwaka wa Uwekezaji Tanzania, linatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza tamko hilo, Ofisi ya Waziri Mkuu imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996 pamoja na Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 ili kuweka misingi imara ya kuboresha mazingira ya uwekezaji yatakayoendana na hali ya sasa ya kiuchumi duniani.

Aidha, Serikali imeongeza mkazo katika kuimarisha miundombinu wezeshi ya kiuchumi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa nishati ya uhakika na ya bei nafuu, maji, mawasiliano, ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji ya reli, barabara, madaraja, anga, vivuko na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kuboresha Mifumo ya Udhibiti wa Biashara (*Blueprint Action Plan*) ambapo hadi sasa Serikali imeweza kufuta na kuboresha tozo na ada 54 zilizonekana ni kero kwa wawekezaji na wafanyabiashara kuitipia bajeti ya mwaka 2019/2020. Hatua nyine ni pamoja na kuondoa migongano na muingiliano wa majukumu mionganoni mwa Mamlaka za Udhibiti kama vile Shirika la Viwango Tanzania na Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa na Vifaa Tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo mikoani vilevile Ofisi ya Waziri Mkuu kuitia Kituo chetu cha Uwekezaji (*T/C*) imeendelea kushirkiana na Ofisi za Mikoa kuandaa makongamano ya uwekezaji yanayonadi vizuri fursa za uwekezaji mikoani. Kwa mwaka huu 2019 kwa mikoa ambayo tayari imeshafanya makongamano hayo ni takribani mikoa 9 na kwa sasa tunaendelea na maandalizi katika Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Serikali imejidhatiti kuhakikisha changamoto zinazokabili wawekezaji nchini zinapatiwa ufumbuzi kuitia mikutano ya mashauriano kati ya Serikali na sekta binafsi katika ngazi za Mikoa na katika sekta mbalimbali. Kwa sasa tumeshafanya mikutano hiyo katika Mikoa ya Arusha, Ruvuma, Lindi na Mtwara.

Aidha, Serikali inaendelea kuvutia uwekezaji kutoka nje kwa kutekeleza ipasavyo diplomasia ya uchumi kuitia Balozi zetu za nje pamoja na kufanya mikutano ya kimkakati na wawekezaji wa nje waliowekeza nchini ili kuvutia uwekezaji zaidi na kufanya mashauriano nao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

MHE. ANNE K. MALECELÀ: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupata jibu kwamba Serikali inashughulikia suala hili lakini naomba kuuliza swali moja tu la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania ni nchi mojawapo katika nchi 4 za Afrika ambazo zinalima pamba ambayo ni *organic*. Naomba Serikali iniambie ina mikakati gani ya kuwaalika wawekezaji katika zao hili la pamba nchini ili wafungue viwanda hapa nchini kuliko ambavyo tunauza pamba ghafi ambapo tunapata hasara sana? (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):
Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze kwa namna ambavyo amekuwa akisimama imara katika kuhakikisha kwamba zao letu la pamba linaongezewa thamani ili badala ya kuuza zaidi ya asilimia 70 ya pamba yetu ghafi basi kwa kiasi kikubwa tunaweza kuiongezea thamani hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kama Serikali tunayo mikakati ya muda mfupi, wa kati pamoja na muda mrefu. Mfano ukiangalia katika nchi zingine kama Bangladesh na Ethiopia kwa upande wa Afrika ambazo zimefanikiwa unaangalia kuna mnyororo wa thamani, wapo ambao wameanzia katika utengenezaji wa nyazi, mfano kama Bangladesh na Ethiopia wao wameanzia katika mnyororo wa mwisho kabisa wa kutengeneza mavazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika masuala ya mtaji, mfano mwekezaji mmoja tu ambaye anatengeneza mavazi anaweza akaajiri mpaka watu 20,000 lakini wakati huohuo mtaji wake anaoutumia inaweza ikawa ni dola milioni 3 mpaka milioni 4. Wakati ukianzia katika ngazi labda ya nyazi pamoja na vitambaa inaweza ikakugharimu zaidi ya dola milioni 10 au zaidi na wakati huohuo ajira pia inakuwa sio nyangi sana. Kwa hiyo, kama Serikali tunatambua umuhimu wa mnyororo mzima wa thamani, tunachokifanya kwa sasa ni kuangalia sasa twende vipi, twende na hatua zote kwa upande huo wa mnyororo au tujikite zaidi kama ambavyo wenzenetu wa Ethiopia wamefanya na ukizingatia kwamba hata hawazalishi pamba nyangi zaidi hai kama ambavyo tunafanya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisema tu kwamba kwanza naendelea kuwapongeza wakulima wote wa pamba na naendelea kutoa rai kubwa waone ni kwa namna gani wanaboresha ubora wa pamba yenyewe wanayoizalisha kupitia kilimo. Ukiangalia katika uzalishaji wenyewe wa mavazi

pamoja na nguo zetu kwa kiasi kikubwa zinahitaji kuwa na *consistency* katika mnyororo mzima. Haiwezekani leo ukawa na ubora wa aina hii halafu kesho una ubora mwininge. Kwa hiyo, niendelee kutoa rai kwa Maafisa wetu wa Ugani waendelee kutoa elimu kwa wakulima wetu wa pamba kuhakikisha kwamba katika uzalishaji wa pamba wanayoizalisha basi kuona kwamba inaendelea kuwa na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukiangalia hata katika viwanda vyetu, pamba inayozalishwa ni takribani tani 300,000 mpaka 400,000 kwa mwaka. Katika msimu wa mwaka huu kwa makadirio ya Wizara ya Kilimo ni kuweza kupata takribani tani 450,000 lakini ukiangalia uwezo wa viwanda vyetu takribani 54 ni kuweza kuzalisha zaidi ya tani 786,000. Kwa hiyo, bado tuna upungufu ni lazima yote haya uzalishaji pamoja na kuboresha uwekezaji viweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni suala zima la mitaji. Ukiangalia katika sekta nzima ya uzalishaji wa nguo na mavazi, viwanda vinahitaji mitaji mikubwa sana. Si hilo tu, wapo ambao wamefanikiwa kama kina Jambo Spinning lakini wamejikuta wameshindwa kuendelea na uzalishaji. Hii ni kutokana na sababu kwanza mtaji ni mkubwa lakini akifanikiwa kuweka mtaji bado mazingira siyo wezeshi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunachokifanya kama Serikali sasa hivi ni kuangalia sekta ndogo hii ya nguo na mavazi kupitia Mkakati wetu ule wa Nguo na Mavazi wa mwaka 2016 – 2020 kuweza kuona ni kwa namna gani sasa tutaweza kuweka vivutio maalum. Kwenye hili siwezi kusema tutaweza vivutio vya aina gani kwa kuwa tutatunga sheria pamoja, Mungu akijaalia nadhani muda si mrefu tutakuja na Muswada wa Sheria ya Uwekezaji ili tuweze kuangalia katika zile sekta ndogo mbalimbali, ni sekta zipi ndogo ambazo kama nchi tunaziwekea kipaumbele tukitambua kwamba ndizo zinaajiri watu wengi lakini tukitambua kwamba inakuwa na mnyororo mkubwa wa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Kilango na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamekuwa wakifuatilia sana uzalishaji wa pamba lakini zaidi uongezaji wa pamba na matumizi yake. Nakushukuru. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuuliza swali langu kwanza kwa ruhusa yako napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake kwa kutuletea ndege mpya aina ya *Dreamliner* Na.787 ambayo imefanya ndege zetu sasa kuwa saba (7). Sambamba na hilo, pia uboreshaji wa miundombinu ya barabara na madaraja katika Jiji la Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, sasa naomba niulize swali langu la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha inaleta wawekezaji wengi na kuendeleza miradi mingi ya uwekezaji kwenye Jiji la Dar es Salaam katika maeneo ya Kigamboni ambayo yana ardhi ya kutosha, llala maeneo ya Chanika lakini pia Kinondoni katika maeneo ya Mabwepande? Ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Angella Kairuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri ya Mkuu, Uwekezaji, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niseme kwamba tunashukuru kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Mheshimiwa Rais kwa pongezi alizozitoa kwa jitihada ambazo Mheshimiwa Rais amezifanya mpaka sasa katika kuhakikisha kwamba tunaongeza miundombinu ya usafirishaji lakini vilevile miundombinu mingine kama vile ya mawasiliano pamoja na ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maeneo ya uwekezaji nipende tu kumhakikisha Mheshimiwa Mariam Kisangi kwamba kuptitia Wizara Ardhi tayari maeneo ya uwekezaji yameshatengwa kwa Dar es Salaam Kigamboni na tutaendelea kufanya hivyo katika maeneo mengine ya Mkoa wa Dar es Salaam na tutaona ni kwa namna gani tunaendelea kuhakikisha kwamba tunapeleka Wawekezaji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwa Kigamboni tulishapata Wawekezaji hao wanaojenga Mradi huu wa Nyerere *Hydro*, wamekuwa wana nia ya kujenga *Industrial packs* pamoja na vyuo vya kiufundi na tayari tumeshawapeleka Kigamboni waweze kuangalia na endapo wataridhika na maeneo hayo, basi kwa hakika wataweza kuwekeza kwa upande wa Kigamboni.

Pia niendelee kumuhakikisha pia Mheshimiwa Mbunge wapo Wawekezaji wengine katika viwanda vya nguo kuptitia Wizara ya Viwanda na Biashara watakuja tarehe 8 Novemba, kutoka Italy na kwenyewe pia tutafanya hivyo kuona ni kwa namna gani tunawapeleka wakaangalie na kuendelea kuwashawishi ili waweze kuwekeza katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niendee kutoa rai kwa Wizara ya Ardhi pamoja na Mamlaka zetu za Halmashauri kuendelea kutenga maeneo ya uwekezaji ambayo yana miundombinu wezeshi ili na sisi iwe kazi rahisi kuvutia uwekezaji, lakini wanapokuja basi wapate maeneo ambayo ni tayari ambayo watatumia muda mfupi katika kuanzisha uwekezaji wao, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji naomba nijikite kwenye suala la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kuhusiana na suala la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli mnyororo wa thamani katika suala la pamba *cotton to cloth* unapaswa kufanyiwa mkakati mahsusini kwa kumwezesha mkulima aweze kupata thamani ya kile anachokifanya, lakini swali langu ni kwamba wakulima wa pamba ambao mwaka hadi mwaka wamekuwa wakifanya kazi ya kulima pamba wanakuwa wanapata hasara; kwa mfano leo hii wakulima wa Mkoa wa Simiyu na hasa Wilaya ya Busega wameuza pamba toka mwezi wa Tano mpaka leo hawajalipwa fedha yao? Sasa Mheshimiwa Waziri haoni kwamba hii ni ku-*discourage* wakulima wasiweze kufanya kilimo kizuri zaidi na nini tamko la Serikali juu ya hili? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Chegeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiri kwamba baadhi ya wakulima wa pamba hawajalipwa fedha zao, pamba mwaka huu mpaka sasa hivi jumla ya bilioni mia nne kumi na saba zimeshalipwa kwa wakulima wa nchi nzima. Wakulima ambao hawajalipwa wanadai bilioni hamsini kufikia sasa hivi na sababu ya msingi ni nini? Ni kwa sababu lazima tufahamu kwamba pamba asilimia zaidi ya 80 inakwenda nje ya nchi, wanunuzi wetu wanakabiliwa na mtikisiko wa bei ambao umewakabili katika soko la dunia na sisi kama nchi tulitoa maelekezo ya bei ya kununulia kama Serikali. Haya yalikuwa maamuzi ya Serikali kwa ajili ya kumlinda mkulima asipate

hasara, lakini Serikali imefanya *intervention* kuongea na *financial institutions* zote na kuweza kuwasaidia namna gani ya kupunguza *interests* kwa wanunuzi ili waweze kwenda sokoni kununua bei ya pamba kwa Sh.1,200.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, siku ya tarehe 14 tutakutana na Kamati ya wanunuzi wote makampuni yote yanayonuna ili kuangalia *flow* ya fedha inavyokwenda, lakini pamba yote iliyokuwa kwa wakulima imeshakusanywa, sasa hivi kilichobaki mkononi mwao ni tani 5,000 tu, ambayo tunaamini mpaka mwisho wa mwezi huu itakuwa imekwishaondoka mikononi mwa wakulima na msimu unapoanza tarehe 15 tunaamini wakulima wote pamba yao itakuwa imeondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili la *intervention* ya bei Serikali tunajitahidi kupunguza gharama kuanzia msimu huu unaokuja na hatutoingilia kupanga bei, bei itakuwa *determined* na soko na sisi jukumu letu kama Serikali itakuwa kuhakikisha mkulima hatopata hasara. Tutatafuta njia zingine za kumlinda mkulima kuliko kumwathiri mnunuzi. Hii ndiyo hatua ambayo tunachukua kama Serikali. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swalı lake. (*Makofii*)

Na. 16

Ujenzi wa Soko Jipyä - Mpwapwa

MHE. GEORGE M. LUBELEJE aliuliza:-

Soko la Mji wa Mpwapwa, ni dogo, limechakaa na halifanani kabisa na hadhi ya Mji wa Mpwapwa ambao idadi ya watu ni zaidi ya laki moja?

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ujenzi wa soko jipyä na la kisasa katika mji huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa inafahamu changamoto ya udogo wa soko la Mji Mpwapwa na imekwishaandaa mikakati ya kujenga soko hilo la kisasa linaloendana na hadhi ya idadi ya watu katika eneo hilo. Halmashauri imetenga eneo katika Kiwanja Na. 61 Kitalu B Mazae chenye ukubwa wa mita za mraba 15,000 kilichopo katika Kata ya Mazae.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri inaendelea kuandaa Andiko la Mradi pamoja na kufanya usanifu ili iweze kuwasilisha andiko hilo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na hatimaye Wizara ya Fedha na Mipango kupitia utaratibu wa Miradi Mikakati, vilevile Halmashauri inaendelea na mazungumzo na uongozi wa Mradi wa *Local Investmest Climate* ili kupata fedha za ujenzi wa soko. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa George Malima Lubeleje, swalii la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza, kwa kuwa Serikali ilichukua vyanzo vingi vya mapato katika Halmashauri zetu, kwa hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa haina mapato ya kutosha ya kuweza kujenga soko; je, kwa nini Serikali isitoe fedha kwa ajili ya kujenga soko la Mpwapwa kama vile inavyotoa fedha kujenga majengo mengine kama vile Vituo vya Afya na majengo mengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, swal la pili, kwa kuwa mimi niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na kwa kuwa jukumu la Mikopo ya Serikali za Mitaa ni kukopesha Halmashauri ili ziweze kujenga masoko, kujenga Vituo vya Mabasi; je, huo mpango umeishia wapi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli kwamba kuna vyanzo vingine vilichukuliwa na Serikali Kuu kutoka Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri, lakini hizi fedha ambazo zilichukuliwa kuletwa Serikali Kuu, kwa maana Mfuko Mkuu wa Serikali ni fedha ambazo zinatumika kujenga miradi mikubwa ya Kitaifa ambayo inanufaisha maeneo yote ya nchi. Zingeachwa kama ilivyokuwa maana yake kuna Halmashauri zingine zingepata miradi zingine zingekosa miradi, kitendo cha kupelekwa Hazina maana yake fedha hizi zinasimamiwa na Serikali na inapeleka miradi mikubwa ambayo kila Mtanzania mahali popote alipo wanifuafaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niliweke sawa jambo hilo, lakini jibu langu la swal la pili ni kwamba, ni kweli kwa sasa kuna miradi ambayo Halmashauri Kuu inapewa fedha kutoka pengine kwa Wafadhili wa nje, kadri muda ulivyokuwa unaenda miradi hii ilikuwa unapanga mipango ambayo huna uhakika nayo. Sasa Serikali imeleta Mpango Mkakati ambayo ina uhakika hata mikopo kutoka Mfuko wa Serikali za Mitaa ilikuwa ni fedha ambayo ina riba na wakati mwingine haina uhakika sana na kuna Halmashauri zingine zimekopa fedha zinadaiwa mpaka leo hawajawahi kurejesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo Serikalia imetengeneza Mkakati pamoja na Wizara ya Fedha, fedha zipo Halmashauri inaandika andiko na Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe katika Halmashauri yake vikao vyta Kamati ya Fedha wanaainisha mradi ambao wanadhani wao utakuwa ni mkakati wao kupata fedha nyingi, wanaleta Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa unaenda Hazina unapitiwa na Wataalam, wakipata fedha hizo wataanzisha mradi mkubwa kama hilo soko Mbunge alivyosema hiyo, hiyo fedha ikipatikana watafanya miradi ambayo wana uhakika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo juzi nilikuwa Manispaa ya Moshi, wana Mradi wa zaidi ya shilingi bilioni ishirini na nane, Jiji la Dar es Salaam wana bilioni hamsini na nane, maeneo mengine bilioni kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kwa hiyo fedha zipo Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri husika waandae Andiko la Kimkakati, tufanye tathmini wapate fedha wajenge mradi ambao utapata fedha za uhakika ili waweze kufanya miradi ya maendeleo katika eneo lao. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Qulwi Qambalo, swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mji wa Karatu ni Mji wa Kitalii na ni mji ambao unakua kwa kasi sana, lakini bahati mbaya mji huo hadi wa sasa hauna soko la uhakika, Halmashauri kwa kutumia mapato yake ya ndani imeanza ujenzi wa soko la kisasa, je, Serikali lini itaunga mkono jitihada hizo za Halmashauri ya Karatu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Qambalo Mbunge wa Karatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba Halmashauri zote hizi Wakurugenzi wameelekezwa, wameitwa Dodoma Wakurugenzi wote nchi nzima, Waweka Hazina, Maafisa Mipango wakapewa utaratibu, Serikali inachofanya kama soko lenu mnadhani kwamba linakidhi viwango walete kama nilivyosema andiko ili fedha zitolewe waweze kufanya kazi, wanakopeshwa fedha, wanawekeza, wanasimamia wenyewe, wanaanza kurejesha kidogo kidogo. Hiyo ni fedha ambayo ina uhakika tofauti na kuahidiwa bilioni kumi halafu hajji au unapata bilioni moja. Fedha za Miradi ya Kimkakati zipo, walete andiko tupitie, wapate fedha wasimamie na Mheshimiwa Mbunge awepo ili wapate fedha ya uhakika na soko lisimame wapeleke huduma na kupata mapato mema ya kujenga Halmashauri yao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali la nyongeza.

MHE. DKT. MARY M. NAGU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kama ulivyo Mji wa Mpwapwa kuna Mji wa biashara unaitwa Endasak Wilaya ya Hanang ni mahali ambapo wanahitaji soko kama hilo wanadolihitaji Mpwapwa, naomba kujua kwa Mheshimiwa Waziri ni nini kitakachofanyika kushirikiana na Halmashauri yetu pale tujenge soko kwa sababu imezungukwa na vitunguu saumu, vitunguu maji, makabichi na nini na hakuna soko, Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mbunge wa Hanang kama ifuatavyo:-

Naomba majibu haya pia yaende kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao wana maswali yanafanana na hayo; maelekezo ni kwamba Wakurugenzi na Wataalam wetu katika Halmashauri wameelekezwa, hii ni fursa tunaomba waitumie. kila Halmashauri inaangalia fursa ya kibashara iliyopo, kuna wengine wameandika Miradi ya Kimkakati kujenga masoko, wengine wamependekeza kujenga stendi na miradi mbalimbali kama hiyo na wale ambao wamefanikiwa tunavyozungumza fedha wamepewa wanaendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa wengine wote Halmashauri zote walete maandiko katika Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Hazina tutapitia, fursa iliyopo waitumie, fedha hizi zipo pale, isipokuwa wale ambao walileta mkakati wakapewa fedha na fedha zile hawakuzitumia, maelekezo yametoka vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, waandike haraka andiko lao, washirikishe Wataalam wao, Waheshimiwa Wabunge washiriki, fedha zipo waanzishe miradi ya kimkakati tupate fedha za uhakika ili kukamilisha miradi ya maendeleo ya wananchi na kuondoa kero katika maeneo yetu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na. 17

Walimu wa Shule za Sekondari Kuhamishiwa Shule za Msingi

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y MHE. SALOME W. MAKAMBA) aliuliza:-

Je, kuna sababu gani za kitaalam zinazosababisha Walimu wa Shule za Sekondari kuhamishwa Shule za Msingi

wakati ufaulu kwa Shule za Sekondari kwa masomo ya sanaa upo duni?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilihamisha baadhi ya walimu waliokuwa wanafundisha shule za sekondari kwenda kufundisha shule za msingi katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo walimu 8,693 walihamishwa. Walimu hao walihamishwa kutokakana na ziada ya Walimu wa masomo ya sanaa waliokuwepo katika shule za sekondari za Serikali nchini ambapo wakati huo shule za msingi za Serikali zilionekana kuwa na upungufu mkubwa wa Walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitaalam Walimu wote wa shule za msingi na sekondari wameandaliwa na wana mfanano katika maeneo ya mbinu za kufundisha, ya kisaikolojia na malezi na makuzi ya watoto wetu. Maeneo hayo ambayo kimsingi ni muhimu kwa kila Mwalimu na hufundishwa katika ngazi zote za vyuo vinyavotoa taaluma ya Ualimu nchini.

Naomba pia nilifahamishe Bunge lako Tukufu kuwa, suala la ufaulu duni husababishwa na sababu mbalimbali zikiwemo za kimazingira, ushiriki wa wazazi na jamii katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji kwa watoto. Hivyo, wingi wa Walimu pekee hautoshi kumfanya mwanafunzi afanye vizuri katika mtihani wake. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Serikali haioni kwamba imewavuruga Walimu wa sekondari ambao wamesomea kufundisha watu wa rika ya sekondari na kuwapeleka katika elimu ya msingi, haioni kwamba imewachanganya na imeshusha morari ya utendaji kazi zao? Hilo ni swali la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali haioni umuhimu wa kuajiri Walimu ambao wako mtaani hawajaajiriwa kwa kukosa ajira kwa muda mrefu, kwa nini wasiwaajiri Walimu hawa wakaenda kufundisha shule za msingi katika ngazi ambayo wao wameisomea? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakagenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza anazungumza kwamba tunashusha morari, siyo ya kweli, hayo yalikuwa ni mapokeo tu, sisi wengine Walimu tunafahamu kwanza mzigo wa kufundisha sekondari na shule ya msingi unatofautiana, ni *heavy duty* sekondari kuliko shule ya msingi, ile inawaelekeza kwamba watu walipopelekwa pale hatukuwa na maandalizi mazuri, watu wakapokea tofauti, lakini waliopokea vizuri wameendelea kufundisha na hakukuwa na shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kupanga Mwalimu afundishe shule ya msingi au shule ya sekondari siyo kushusha morari yake, hili tu nimesema kulikuwa na upungufu mkubwa, kama Serikali, kama una watu zaidi ya 11,000 wako wanafundisha vipindi vichache sana kwa siku na kuna Walimu katika shule ya msingi wanafundisha vipindi vingi, ilikuwa ni busara kutumika kuwapeleka kule kufundisha, lakini tumeshachukua hatua, tuliwaelekeza Maafisa Elimu wa

Mikoa na Halmashauri zetu, wakakaa wakazungumza nao wanaendelea kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ajira, ni kweli kwamba tuna upungufu mkubwa wa Walimu katika shule za msingi na sekondari, lakini juzi hapa tumeajiri Walimu 4,500, tumeomba kibali cha Walimu 22,000 hasa masomo ya shule za msingi, masomo ya fizikia na hisabati katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kadri Serikali itakapopata uwezo ndivyo inaweza kuajiri, huwezi kuajiri tu kwamba kuna Walimu mtaani, hapana, lazima uajiri Walimu lakini wapate stahiki zao na uwezo wa kuwalipa kila mwisho wa mwezi pamoja na mahitaji mengine. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini.

Na. 18

Fedha za Elimu Zinazotumwa Moja kwa Moja Mashulenii

MHE. KABWE Z. R. ZITTO aliuliza:-

Katika kutekeleza mpango wa kutuma fedha za elimu moja kwa moja mashulenii Serikali hutuma shilingi bilioni 18 kila mwezi kwenye akaunti za shule nchini kwa mujibu wa maelezo ya viongozi kwa umma?

(a) Je, Serikali imeshatuma kiasi gani cha fedha kati ya Januari – Desemba, 2016, 2017 na 2018 kwenda kwenye shule nchini?

(b) Je, Serikali imefanya ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo na kama zilizotoka Hazina zilifika kwenye shule husika; Je, Serikali ipo tayari kuleta Bungeni Ripoti za Ukaguzi huo?

(c) Kama Serikali hajifanya ukaguzi huo; Je, ipo tayari kuagiza ukaguzi maalum utakaofanywa na CAG na kuweka Taarifa ya Ukaguzi huo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Mpango wa Elimu msingi Bila Malipo kuanzia Januari, 2016 hadi Disemba, 2018 jumla ya Sh.798,170,400,005.04 zimetolewa na Serikali na kutumwa moja kwa moja shulenii. Fedha hizo zimejumuisha chakula kwa wanafunzi, fidia ya ada, uendeshaji wa shule, posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu na Maafisa Elimu wa Kata. Fedha hizi zinajumuisha pia fedha zinazokwenda Baraza la Mitihani kwa ajili ya maandalizi ya mitihani ya Kitaifa kwa ngazi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utaratibu wa kawaida wa ukaguzi wa fedha za Serikali, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali hufanya ukaguzi katika Wizara, Taasisi, Mashirika ya Umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa kila mwaka. Kwa kuwa, fedha za Elimu Msingi Bila Malipo ni sehemu ya fedha zinazotumwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwa kuwa fedha hizo hutengwa kwenye bajeti kila mwaka wa fedha, ni dhahiri kuwa fedha hizo hukaguliwa na CAG pale anapofanya ukaguzi kwenye mamlaka husika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, swali la nyongeza.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu kila mwaka linatenga jumla ya shilingi elfu 10 kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi. Katika fedha hizo shilingi elfu sita zinapaswa kwenda moja kwa moja kwenye

mashule na shilingi elfu nne zinakwenda TAMISEMI kwa ajili ya ununuzi wa vitabu, lakini Serikali inafahamu kwamba katika mpango wa *GEP*, Serikali ilipata zaidi ya shilingi bilioni 45 kwa ajili ya kununua vitabu, na kwa jumla ya idadi ya wanafunzi waliopo nchini wa shule za msingi, kuna zaidi ya shilingi bilioni 144 zilipaswa zinunue vitabu na shule hazina vitabu na kuna vitabu ambavyo viliondolewa, Serikali....

NAIBU SPIKA: Uliza swali.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haioni kwamba, ni muafaka sasa kufanya ukaguzi maalum ili kuweza kutambua jumla ya fedha hizi shilingi bilioni 190 zimetumika namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika uchunguzi uliofanywa kwenye jumla ya halmashauri za wilaya 12 hapa nchini, katika shilingi elfu sita inayopaswa kwenda kwenye mashule kwa kila mtoto, fedha inayofika, kwenye hii *sample* ya wilaya 12 ni shilingi elfu 4200 tu. Serikali haioni haja ya kufanya ukaguzi maalum ili kuweza kufahamu hii shilingi 1200 ambayo haifiki kwenye shule inakwenda wapi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza ni la kitakwimu, una uhuru wa kulijibu kama unalo, lakini swali la pili, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza si kweli kwamba TAMISEMI tunanunua vitabu, tumegawana kazi, suala la vitabu na kiwango chake na ubora wake linafanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa ameuliza swali la kitakwimu na Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu yupo hapa, basi unaweza ona namna ya kutenda hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la kujibu hapa ni kwamba, Mheshimiwa Zitto, anasema halmashauri zimekaguliwa, sisi kama Serikali hatuna taarifa ambayo anaizungumzia hapa Mheshimiwa Zitto, kwamba fedha

hazifiki katika shule zetu, na Mheshimiwa Zitto Kabwe, bahati nzuri kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ya LAAC, Halmashauri ya Kigoma Ujiji ambayo ni Halmashauri ya chama chake cha ACT, ndiyo halmashauri ambayo imekuwa na hati chafu miaka minne mfululizo, lakini vilevile miradi ya elimu iliyopo pale, ina hali mbaya kweli kweli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna halmashauri imekaguliwa tuna takwimu za kutosha ni halmashauri ya Mheshimiwa Mbunge. Jibu ni kwamba, hakuna taarifa ambazo anazitoa, siyo za kweli, hakuna ukaguzi uliofanyika mahususi na hakuna malalamiko ambayo yameletwa kwamba Serikali tufanye ukaguzi maalum, tukipata taarifa hizo na maombi hayo, Serikali itachukua hatua kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa fedha ya elimu na miradi ya Serikali inafanyika kila wakati, kuna Kamati za Bunge, imeenda TAMISEMI, imeenda watu wa Ustawi wa Jamii wamekagua na taarifa zipo. Kila wakati tunachukua hatua kabla ya bajeti na baada ya bajeti hii ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la mwanzo ambalo linahitaji takwimu, utampatia takwimu Mheshimiwa Zitto Kabwe. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Zitto kasema kwamba fedha za *Global Partners for Education* dola milioni 46 zinatumika kwa ajili ya vitabu. Naomba nimfahamishe kwamba, fedha hizo zinatumika kwa ajili ya kuendeleza sekta ya elimu kwa ujumla na siyo *specific* kwa ajili ya vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba nimhakikishie kwamba, fedha zote ambazo zinakwenda kwenye vitabu, zimeenda kwenye Taasisi yetu ya Elimu na

kwa sasa tumejikia sehemu ambayo karibia vitabu vyote vinapati kana. Kuna vitabu ambavyo tuna endelea kuvicha pisha lakini kwa sehemu kubwa vitabu vinapati kana sasa isipokuwa kama kuna changamoto kwenye halmashauri moja moja, inakuwa ni kesi ambayo ni *specific* lakini kwa ujumla kwa sasa tumesha ondokana na shida ya vitabu, tulichapisha vitabu vipyta na tena vitabu ambavyo havina makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi, ninaweza nikakutana na Mheshimiwa Zitto nimueleweshe zaidi kwa sababu takwimu yeye ndiyo kaja nazo ambazo ziyo takwimu za Serikali, kwa hiyo, akitaka ufahamu zaidi anaweza akakutana na mimi nikamfahamisha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, swali la kwanza linalohusu takwimu limeshajibowi na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu. Mheshimiwa James Mbatia, swali la nyongeza!

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, katika kuibadilisha dunia, *ku-transform* dunia, kigezo cha elimu kimepewa kipa umbele namba nne na kigezo cha elimu bora. Je, fedha hizi zaidi ya bilioni 900 ambazo zimekwenda kwenye shule zetu, kigezo cha kupima zimefanikisha kwa kiasi gani ubora wa elimu na viashiria vyake vyote ukoje!

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tumepeleka fedha zaidi ya shilingi bilioni 900 kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi la swali la Mheshimiwa Zitto, na Mheshimiwa Mbunge anataka kujua vigezo vya kuonyesha kwamba elimu imeboreka ni kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, fedha hii inafanya mambo mengi sana ikiwepo ni pamoja na uendeshaji wa shule, usimamizi wa elimu Tanzania umeimarika sana. Tumenunua pikipiki katika Waratibu Elimu wa kata zote nchini, sasa wanawenza ku-move kutoka shule moja kwenda nyiningine, maana yake ni kwamba hata utoro rejareja umepungua shulenii, kiwango cha watoto kupata mimba na kuchukua hatua, tuna kesi mbalimbali mahakamani na baadhi ya watu ambao wametuhumiwa kuwapa wasichana wetu mimba wameshafikishwa mahakamani na wengine wamefungwa, kesi ziko katika hatua mbalimbali. Hiyo ni kwa sababu fedha hiyo imekwenda, imepeleka vifaa vya utendaji, pikipiki na imewezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, tumejenga hosteli maeneo mbalimbali, kitendo ambacho kimepunguza watoto wa kike wengi sasa wanakaa katika shule zetu na utaangalia matokeo mbalimbali, darasa la saba, *form four* na *form six*, kiwango cha ufaulu cha watoto wa kike kimeongezeka sana. Tumejenga mabweni na hosteli maeneo mbalimbali, watoto wa kike wengi wanakaa katika maeneo ya shule na usimamizi wao umekuwa ni mzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini elimu msingi bila malipo, sasa hivi tunapozungumza, vijana wetu wa kidato cha nne wanafanya mitihani. Mwaka 2018 wanafunzi ambao walisajiliwa, watahiniwa wa kufanya mitihani, walikuwa 427,000, mwaka huu ni 485,866, maana yake ni ongezeko la wanafunzi ambao wameingia kidato cha nne zaidi ya asilimia 1.37, huu ni ufaulu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vijana wengi wa Tanzania maskini ambao walikuwa hawana uwezo wa kusoma wa kike na wakiume, wengine walifanya kazi za *house girl*, wengine walikuwa makuli kwenye masoko, walikuwa wapiga debe, ninapozungumza hapa, vijana wengi kitendo cha Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kuondoa ada katika masomo yao, watoto wengi wapo mashulenii, hata wananchi ambao wanataka ma-

house girls wanapata shida sana kuwapata, vijana, wasichana wengi wanasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ni kwa uchache, lakini Mheshimiwa Mbaitia ni kweli kwamba, ye ye anafahamu, hata matokeo ya *form six* yameongezeka, elimu ya *high school* imekuwa ni kubwa sana, kwa sababu ya fedha hizi ambazo zimekwenda kuimarisha huduma. Ndiyo maana, hata wananchi ambao walitoa nguvu zao kuchangia kujenga maboma, tumepeleka fedha zaidi ya bilioni 29, angalia halmshauri zote nchini ili tumalize maboma, watoto wetu waendelee kukaa katika madarasa ambayo yapo sawa na wapate matundu ya yooo. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, swali la nyongeza!

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kumekuwa na matumizi ya hovyo kabisa katika halmashauri zetu na kupelekea halmashauri hizo kupata hati chafu. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga imepata hati chafu kwa mwaka mmoja, mimi najiona kama natembea bila nguo, lakini halmashauri kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, Halmashauri ya Ujiji ambayo inaongozwa na ACT anapotoka Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe, miaka minne mfululizo imepata hati chafu wakati ye ye akishinda *twitter* na *Instagram*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifuta halmashauri hizi? (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Ulanga, alikuwa anasema maneno mengi sana hapa Bungeni wakati mwingine akaonekana kwamba ni kituko, lakini naomba ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kauli ya Mheshimiwa Mbunge wa Ulanga imetusaidia sana TAMISEMI na watu wengi

wamewajibishwa katika halamshauri ile na uchunguzi mahususi umefanyika tukagundua kuwa ni kweli kwamba watumishi wetu wamwekuwa wabadhilifu, fedha nyingi ziliwi, kama alivyokuwa analalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, ni kweli, Kamati ya Bunge ya *LAAC* wapo, Mwenyekiti yupo hapa na Wajumbe wenzake wanafamu. *CAG* alipopitia baadhi ya halmashauri, hata mimi nilishangaa, halmashauri mbili, wamepoteza fedha zaidi ya shilingi bilioni kumi na kitu, lakini Halmashauri ya Kigoma Ujiji, halmashauri hii imekuwa na hati chafu mfululizo miaka minne, lakini tulipowahoji viongozi wa pale, wakatuambia viongozi wetu wa kisiasa, wanaingilia mpaka manunuzi ya kisheria, mpaka tenda ambazo zinagawanywa pale Kigoma Ujiji, wanapewa kwa itikadi za kivyama, hizi ni taarifa rasmi za Bunge, ninazozitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumetoa maelekezo, ni kweli kwamba, ile halmashauri ikiendelea kupata hati chafu ya tano na itapewa ukaguzi mahususi, kuna uwezekano mkubwa Mheshimiwa Zitto halmashauri yako kufutwa kwa sababu husimamii vizuri, na wewe ni mtaalam wa mahesabu. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Ofisi ya Rais, (Utumishi na Utawala Bora), Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, Mbunge wa Bahi, sasa aulize swali lake.

Na. 19

Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

MHE. OMARY A. BADWEL aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa baadhi ya wananchi wamekuwa wakinufaika na mradi wa *TASA* Fambao kwa kiasi umekuwa ukifanya vizuri, aidha mradi huu umefika vijiji

vichache tu na vijiji vingine bado havijafikiwa na Serikali iliahidi kuwa vijiji vyote vitanufaika na mradi huu.

(a) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya mradi wa *TASAF* kufikia vijiji vyote nchi nzima?

(b) Kumekuwa na utaratibu wa baadhi ya viongozi kukata fedha za walengwa wa *TASAF* moja kwa moja kwa kuwakatia bima, michango mbali mbali ya vijiji na kadhalika bila ridhaa yao. Je, Serikali inatoa kauli gani katika jambo hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel Mbunge wa Bahi lenye maswali mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ulipoanza mwaka 2013 uwezo wa fedha uliokuwepo ultosheleza kufikia Viji/Itaa/Shehia 9,986 ikiwa ni asilimia 70 ya Viji/Itaa/Shehia zote nchini. Viji/Itaa/Shehia ambavyo havijafikiwa ni 6,858.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshakamilisha hatua zote za maandalizi ya Kipindi cha Pili cha Mpango huu wa Kunusuru Kaya Maskini ambacho kinatarajia kuanza utekelezaji mwishoni mwa mwaka huu 2019 baada ya Serikali kupata fedha. Kipindi cha Pili ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kitatekelezwa kwenye Halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar katika Viji/Itaa na Shehia zote ikiwa ni pamoa na kufika kwenye Viji/Itaa/Shehia 6,858 ambavyo bado havijafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ufanuzi kuhusu matumizi ya fedha za walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Fedha hizi ambazo ni ruzuku zinatolewa ili kaya iweze kugharamia mahitaji ya msingi kama chakula, gharama za elimu na afya na kuwekeza kwa ajili ya kuanzisha miradi ya kuongeza kipato. Hivyo, ni maamuzi ya kaya husika kupanga matumizi ya fedha hizi ili mradi haziendi kwenye matumizi ambayo hayaisaidii kaya kujikwamua na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika baadhi ya maeneo, viongozi wa vijiji wanalazimisha kukatwa kwa ruzuku za walengwa ili kukatiwa bima ya afya au kulipia michango mbalimbali. Hii si sawa na haikubaliki. Napenda kusisitiza, lakini vilevile niagize, kwamba walengwa wasikatwe fedha zao moja kwa moja bali walipwe stahiki zao na iwapo kuna michango inayotakiwa kama ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya kijiji basi michango hii itozwe kwa wananchi wote wa kijiji husika na siyo kukata moja kwa moja kutoka fedha za walengwa wa *TASAF* peke yao. Nimalizie kwa kusisitiza kwamba viongozi wote waliokuwa wanatoa amri ya kukata fedha za walengwa wa *TASAF* moja kwa moja bila ridhaa ya walengwa hao, waache kufanya hivyo mara moja, kwa kuwa huu siyo utaratibu na wala siyo sahihi na vinginevyo watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba, baadhi ya halamshauri zilishawahi kufanya hivyo na Wakurugenzi waliagizwa warudishe fedha hizo na tayari wamesharudisha. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omary Ahmad Badwel, swali la nyongeza!

MHE. OMARY A. BADWEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja namajibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ninampongeza kwa kazi nzuri, nilikuwa na maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa katika miradi ya *TASAF* Awamu ya I na *TASAF* Awamu ya II, ulikowepo pia utekelezaji wa miradi ya miundombinu kama ujenzi wa barabara, ujenzi wa madarasa, miundombinu ya maji, utoaji wa fedha kwa ajili ya VIKOBA na miradi mingine mbalimbali, zikiwemo zahanati. Lakini baadaye katika *TASAF three*, *TASAF* Awamu ya II miradi hiyo kwa kiwango kikubwa iliondolewa, ama ilikuwepo kwa kiasi kidogo au haikuwepo kabisa.

Sasa je, katika huu mpango wa awamu ya pili wa *TASAF* inayofuata sasa miradi hii itahusika katika utekelezaji katika vijiji vyetua mbapo ilikuwa imetoa faida kubwa sana katika sekta mbalimbali? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swalii la pili, kwa kuwa Awamu hii ya III ya ugawaji wa fedha kwa walengwa walikuwa wanakwenda kugawa fedha moja kwa moja kwa walengwa kwa maana hizi kaya maskini, lakini ilijitokeza pia uwepo wa kaya hewa, jambo ambalo liliساببشا fedha hizi za Serikali kwenda mahali ambapo kwa watu hawakuwa waaminifu na hivyo kutokufikia malengo yaliyokusudiwa.

Je, katika awamu hii ya pili ya ugawaji wa mradi huu wa fedha za *TASAF* Serikali imejipangaje kuhakikisha kwamba hakutokei tena walengwa hewa ili fedha hizi ambazo zimepangwa na Serikali kupelekwa huko ziweze kupelekwa huko ziweze kufanya kazi iliyokusudiwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Utumishi na Utawala Bora, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na yeye ninampongeza akiwa mmoja wapo wa watu ma-champion mahiri katika kufuatilia walengwa wetu wa kaya maskini kuititia mpango wetu wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge kabisa kwamba, mpango wa kunusuru

kaya maskini, ni kweli awamu ya kwanza ulihusisha sana miundombinu, na ninaomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba, katika awamu yetu hii ya tatu kipindi cha kwanza, ambacho kinaisha mwezi huu na kipindi cha pili ambacho kinaanza mwezi ujao wa 12 mwaka 2019, tutaendelea na mpango wa miundombinu lakini tutajikita zaidi katika *public works*, kwa maana ya kwamba, zile ajira kwa muda, kwa wale walengwa ambao wanatokana na kaya maskini sana ili waweze kufanya kazi, waweze kupata ujira na ajira katika kuwawezesha maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, anasema Serikali tumejipangaje katika awamu ya tatu, Awamu ya II niliambie Bunge lako Tukufu kwamba tumejipanga, Serikali ya awamu ya tano, kuhakikisha kwamba walengwa wote kuanzia sasa hivi tutakuwa tunawaendea kwa kutumia njia za kidijitali kwa maana ya *GPS*, tutakuwa tunapiga picha kwenye kaya husika, lakini tayari tumeshafanya *pilot project areas* katika Mtwara *DC*, katika Halmashauri ya Nanyamba, lakini hata kule Siha na changamoto tulizopipata kule, ndizo ambazo zitatusfanya tuboreshe katika maeneo mengine ambayo tutafika katika sehemu yetu hii ya pili inayoanza mwezi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba pia tutakuwa tunawalipa walengwa kwa njia za kielektroniki, vilevile VIKOBA na tayari tumeshaweka mpango mkakati mwingine, kuhakikisha kwamba tutakuwa na wale wanaofuzu, kwa maana ya *graduation*, tutakuwa tunawapatia mafunzo na tunawaunganisha na taasisi za kifedha na hii yote ili kuweza kuwa na *multiply effects*. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Toufiq, swali la nyongeza!

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wanufaika wengi wa *TASAF*ni wazee wasiliojiveza na wanatoka katika maeneo ya pembezoni na inapofikia siku ya kupokea mafao, huwa wanafika pale katika maeneo

ya vijji kwa kutumia usafiri na usafiri huo wanalipia zile fedha za mafao. Je, Serikali haioni umefikia wakati wa kubaini wazee hawa wasiojiweza na kuweza kuwapelekea zile fedha katika maeneo yao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Utumishi na Utawala Bora, majibu kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, hapa wakati najibu maswali yangu ya msingi na ya nyongeza ya Mheshimiwa Badwel nimesema, mkakati mmoja wapo wa Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha tunaboresha, kwamba tutakuwa tunawalipa walengwa wote kwa njia za kielektroniki kwa maana ya kwamba tumegundua kwamba walengwa wengine walikuwa wanakatwa fedha zao bila ridhaa yao na wengine walikuwa wanadhirumiwa, ndiyo maana katika kuboresha, tumeamua kwamba tutakuwa tunawalipa kwa njia ya kielektroniki. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza!

MHE. HAWA S. MWAI FUNGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, kumekuwa na utaratibu mbovu kwa baadhi ya viongozi wanaogawa fedha hizi, wakitumia itikadi za kisiasa, ikiwepo ukiwa mwanachama wa chama fulani, unaweza ukapewa fedha hizo, lakini ukiwa mwanachama wa chama kingine hupewi fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Serikali itoe tamko fedha hizi wanaotakiwa kupewa ni watu wa aina gani? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Utumishi na Utawala Bora, majibu.

NAIBU WAZIRI WA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli haina

ubaguzi. Ni Serikali ya Watanzania wote. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba pesa hizi zinazotokana na Mpango wetu wa TASAF ni kwa walengwa wote wanaotokana na zile kaya masikini sana na hakuna ubaguzi wowote. Nitoe rai na agizo kwamba ye yote atakayeleta ubaguzi katika kuhakikisha kwamba walengwa wanaotokana na mpango huu wa kunusuru kaya masikini wanasaidiwa, watoe taarifa na watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 20

Elimu Juu ya Majanga ya Moto

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA aliuliza:-

Majanga ya moto yamekuwa yakinoteka mara kwa mara hasa Viwandani, Majumbani na katika majengo ya Serikali:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa mafunzo kwa Wafanyakazi na wananchi juu ya mbinu za kujihami na kuijokoa katika majanga ya moto?

(b) Je, Serikali imejipangaje katika kutoa mafunzo katika maeneo ya kazi na wananchi juu ya matumizi ya mitungi ya kuzima moto (*Fire Extinguishers*)?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kukagua mitungi hiyo kama bado inafaa kwa matumizi au imeshapita muda wake wa kutumika?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Kaskazini Unguja, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa mafunzo ya mbinu za kujihami na jinsi ya kujiokoa katika majanga ya moto kwenye maeneo ya kazi na wananchi kwa ujumla. Elimu dhidi ya kinga na tahadhari ya moto imeendelea kutolewa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo maeneo yenye mikusanyiko ya watu kama vile masoko, Shule za Sekondari na Msingi, Vyuo, Makanisani na Misikitini kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo magazeti, radio na televisheni.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limejipanga vyema kutoa mafunzo kwenye maeneo ya kazi na wananchi juu ya matumizi ya mitungi ya kuzimia moto kwa kuanzisha kampeni mbalimbali kama vile "Ninacho, Ninajua Kukitumia," "Mlango kwa Mlango" na "Nyumba Salama" zenyelengo la kuhamasisha watu kuwa na vizimia moto na kujua kuvitumia katika maeneo ya makazi, viwanda, maeneo ya vyombo vya usafiri na usafirishaji, majumbani, maeneo ya biashara na katika mikusanyiko mikubwa ya watu. Aidha, wananchi wanaendelea kupatiwa elimu na mafunzo juu ya mifumo yote ya kuzima kuzima katika majengo na maeneo mbalimbali ili kuepusha majanga ya moto.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto kwa mujibu wa Kanuni za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji umeendelea kufanyika sambasamba na ukaguzi wa mitungi ya kuzima moto na kumshauri mtumiaji juu ya ubora wa mtungi na kumshauri mmiliki ipasavyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Angelina Malembeka, swali la nyongeza.

MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanaonesha kabisa Serikali ina nia nzuri ya kusaidia wananchi wake. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja nilikuwa nina maswali mawili ya kuongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nilitaka kujua: Je, huduma ya uokoaji na kuzima moto kuna gharama zozote ambazo mhudumiwa anatakiwa alipe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu la pili: Je, kama gharama hizo zipo, ni utaratibu gani unatakiwa ufanywe ili aliyepatiwa huduma aweze kulipa bila kuwa na taharuki? Maana kipindi kile anakuwa amechanganyikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa dhati kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Malembeka kwa kazi nzuri ambayo anayoifanya katika Mkoa wake wa Kaskazini. Kwa kweli anawatendea haki wapiga kura wake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nikijibu maswali yake pamoja, kwanza huduma za kuzima moto ni za bure, hakuna gharama. Hata hivyo, kwa mujibu wa sheria ya Jeshi la Uokoaji na Zimamoto ya mwaka 2007 Sura ya 427, inaeleza kwamba Jeshi la Zima Moto na Uokoaji lina Mamlaka ya kuweza kutoa leseni kwa makampuni binafsi kutoa huduma hizo ikiwemo huduma ya kuzima moto pamoja na vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, makampuni haya ndio ambayo yanaingia mikataba na Taasisi binafsi na ndio yanakubaliana malipo, lakini kwa maana ya huduma hizi za zimamoto ni bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na utaratibu ambao unatumika, unapiga namba 114 na kikosi chetu kinafika pale haraka iwezekanavyo kutoa huduma hizo bila malipo yoyote. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 21

REA III Kupitia *Perry Urban* – Tanga

MHE. MUSSA BAKARI MBAROUK aliuliza:-

Tanzania ina jumla ya Majiji sita likiwemo Jiji la Tanga; katika Majiji hayo kuna maeneo ambayo yako nje ya Jiji ambayo ni Mitaai, Vitongoji na Vijiiji (*Perry Urban*); Kitengo cha *Perry Urban* kimekabidhiwa jukumu la kusambaza umeme wa REA III katika Majiji:-

Je, ni lini *Perry Urban* itaanza kusambaza umeme katika Jiji la Tanga?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijiiji (*REA*) inaendelea na utekelezaji wa miradi ya umeme iliyopo katika vijiiji, vitongoji na maeneo mbalimbali kandokando ya miji na vijiiji yaani *Perry Urban*. Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huu umeanza katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa Pwani na kwa upande wa Dar es Salaam katika Wilaya ya Kigamboni. Utekelezaji wa mradi huu utakamilika mwezi Aprili, 2020. Baada ya kukamilika kwa mradi huu, Serikali itaanza kutekeleza mradi huu katika Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jiji la Tanga Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na kubainisha kuwa miradi wa kupeleka umeme maeneo ambayo yako kandokando ya Jiji la Tanga unahusisha ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 15, ufungaji wa transfoma 15 kati ya hizo transfoma 4 ni za KVA 200, transfoma sita za KVA 100 na 5 za KVA 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi ya *Perry Urban* katika Jiji la Tanga pia utahusisha ujenzi wa njia ya Msongo wa kilovoti 11 yenye urefu wa kilomita 48.8, ufungaji transfoma 35; na kati ya hizo transfoma nane ni za 200KVA, 20 za 100KVA na saba za KVA 50. Kazi nyiningine ni kuvuta laini ndogo ya KV 0.4 yenye urefu wa Kilomita 200. Wateja wa awali watakaonufaika na mradi huu katika Jiji la Tanga ni 5,125 ambaao wanatarajiwu kupata umeme katika maeneo hayo. Utekelezaji wa mradi huu utaanza mwezi Julai, 2020 na kukamilika mwezi Machi, 2021. Gharama za mradi huo ni shilingi bilioni 7.5

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Mbarouk swali la nyongeza.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini pamkuwa na malalamiko katika yale maeneo ambayo yameshapelekewa transfoma za Kilovolt 50. Je, tatizo hili kwa nini linajirudia tena? Kuna baadhi ya maeneo yametajwa kwamba katika transifoma 35, transifoma saba za KV 50 halafu kuna transifoma nyiningine nne. Kwa nini tusipeleke zile ambazo ni za kuanzia KV 100?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili katika taarifa hii haikuainisha baadhi ya maeneo ambayo ndiyo hasa yaliyokusudiwa. Kwa mfano, kwenye Kata ya Kirare kina maeneo ya Mapojoni, Mtambuuni, Msakangoto, Kirombere lakini kwenye Kata ya Mzizima kuna maeneo ya Kihongwe, Rubawa, Mleni, kwenye kata ya Kiomoni kuna maeneo ya Pande Muheza, Pande Masaini, Pande Mpirani, Kata ya Marungu kuna Mkembe, Geza Ndani na Geza Barabarani;

Pongwe kuna maeneo ya Pikinangwe; na Kata ya Maweni kuna Machembe, Mtakuja na Mwisho wa Shamba: Je, maeneo haya sasa hususan noyo yamo katika huu mradi na lini hasa yataanza kufanyiwa huu uwekezaji wa *REA III?* (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli yako maeneo ambayo tulikuwa tukipeleka transfoma za KV 50 na nyininge 100 na 200 na kuendelea, lakini maeneo tunayopeleka KV 50 inategemea pia na uwekezaji na aina ya wateja. Ziko faida nyngi sana za kupeleka transfoma ndogo ndogo katika baadhi ya maeneo na hasa katika kukabiliana na uharibifu wa mitambo inapotokea dharura. Kunapokuwa na transfoma za 50 nyngi, kwa hiyo, kunapokuwa na dharura ya kuharibika transifoma moja, wateja wengine wanaendelea kupata umeme bila matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hasara za kuwa na transifoma moja kubwa, ni kwamba ikishaharibika wateja wengi wanakosa umeme, lakini tumelichukua ombi la Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kusambaza transifoma za kila aina kukabiliana na hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili katika Jiji la Tanga tunayo maeneo 12 yatakayopelekewa umeme wa *Perry Urban* ikiwemo kama alivyotaja maeneo yake, lakini yako maeneo ya Chongoleani, Mabwakweni, Majani Mapana na maeneo mengine mpaka 12 na utekelezaji unaanza Julai mwakani na kukamilika mwezi Desemba, 2021. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Halima Bulembo.

Na. 22

Hitaji la Umeme wa REA – Kagera

MHE. HALIMA A. BULEMBO (K.n.y. MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU) aliuliza:-

Mkoa wa Kagera una vijiji 134 ambavyo havijafikiwa na umeme wa *REA*; Biharamulo Vijiji 29, Bukoba Vijiji 9, Karagwe Vijiji 8, Kyerwa Vijiji 31, Misenyi Vijiji 5, Muleba Vijiji 25 na Ngara Vijiji 27:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa *REA* katika Vijiji hivyo?

(b) Umeme wa *REA* ulifika kwenye vijiji vingi lakini haukusambazwa: Je, mradi wa ujazilizi utaanza lini Mkoani Kagera ili wananchi waliorukwa wapatiwe umeme?

WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu liloulizwa na Mheshimiwa Halima Bulembo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inatekeleza mradi kabambe wa kupeleka umeme katika vijiji vyote nchini kufikia mwezi Desemba, 2021. Kwa sasa Mkandarasi *Nakuroi* anaendelea na kazi ambapo kufikia mwezi Oktoba, 2019 vijiji 82 vimewashwa umeme katika Mkoa wa Kagera na kazi ya uunganishaji wa wateja inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote vitakavyosalia katika Mkoa wa Kagera vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* awamu ya pili, unaozunguka kuanza sasa ambao utakamilika mwezi Januari, 2020. Pia kukamilika kwa mradi huu mwezi Desemba, 2021 kutapeleka umeme katika

maeneo yote katika Mkoa wa Kagera pamoja na Vitongoji vyake.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ujazilizi awamu ya pili (*Densification IIA*) utatekelezwa katika Mikoa tisa na utaanza kutekelezwa kuanzia mwezi Novemba, 2019 hadi mwezi Juni, 2020. Mradi wa ujazilizi katika Mkoa wa Kagera utaanza kutekelezwa kupitia mradi wa ujazilizi awamu ya *IIB* (*Densification IIB*) utakaoanza kutekelezwa kuanzia mwezi Julai, 2020 na kukamilika mwezi Machi, 2021. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, swali la nyongeza.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa naomba nimpungeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri kabisa, lakini nina maswali mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mkoa wa Kagera siyo vijiji peke yake ambavyo havijapata umeme wa *REA*. Kumekuwa na Taasisi kubwa kama shule na Vituo vya Afya ambavyo bado havijapata umeme wa *REA* na kupelekea kushindwa kutoa huduma zinazotakiwa kwa wakati. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha taasisi hizi zinapata umeme? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, wananchi wa Mkoa wa Kagera wamekuwa wakikumbwa na kadhia ya kulipishwa nguzo za umeme. Serikali au Wizara inazungumziaje kadhia hii inayowakuta wananchi wa Mkoa wa Kagera? Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nimpungeze sana Mheshimiwa Halima Bulembo anapofutilia masuala ya umeme katika Mkoa wa Kagera. Nampongeza sana na kweli kazi kubwa imeonekana

kutokana na jitihada zake hasa kwa kupitia vijana. Hongera sana Mheshimiwa Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze katika masuala yake mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza anataka kujua kuhusiana na upelekaji wa umeme katika taasisi za Umma. Naomba nitoe maelekezo kwa Halmashauri zetu na Waheshimiwa Madiwani wanaonisikiliza. Ni kweli Serikali imekuwa ikipeleka umeme katika maeneo yote hasa vijijini lakini baadhi ya taasisi zimekuwa hazilipiwi na wamiliki wa taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba sana wamiliki wanaohusika walipie gharama ya 27,000 ili taasisi zote zipelekewe umeme. Maelekezo na mwelekeo wa Serikali ni kuhakikisha taasisi zote zinapelekewe umeme. Nakupongeza Mheshimiwa Hallima Bulembo kwa sababu katika Mkoa wa Kagera hadi sasa taasisi 897 zimepelekewe umeme na hii ni jitihada kubwa. Naomba maeneo mengine ambayo hayajapelekewe umeme, wanaohusika waendelee kulipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia taasisi tukiwa na maana ya shule, Vituo vya Afya, Zahanati, Misikiti, masoko na hata kama kungekuwa na maeneo madogo ya viwanda. Kwa hiyo, nitoe sana ombi kwa Waheshimiwa Wabunge kupidia kwa Madiwani na Wenyeviti wa Halmashauri tupeleke kwa kulipa shilingi 27,000/= katika Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swalii la pili kuhusu kulipishwa nguzo; ni kweli zipo changamoto katika baadhi ya maeneo, yapo maeneo bado Wakandarasi na Mameneja wa TANESCO wanaendeleza kutoza nguzo wateja. Naomba nitoe tamko kali sana kupitia Bunge lako Tukufu kwamba ni marufuku kutoza nguzo kwa wateja wote; iwe Mkandarasi awe Meneja wa TANESCO, awe Injinia, awe Kibarua wake ni marufuku kulipiza mteja nguzo. Hii ni kwa sababu Serikali imegharamia kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekimbia, kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 23

Barabara ya Njia Nane Kutoka Ubungo Hadi Kibaha

MHE. SILVESTRY F. KOKA aliuliza:-

Serikali inajenga njia ya barabara nane kutoka Ubungo hadi Kibaha:-

Je, barabara hiyo inaishia eneo gani la Mji wa Kibaha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ipo katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara na madaraja nchini ikiwemo mradi wa upanuzi wa barabara kuu ya Morogoro sehemu ya Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani. Mradi huu unahusisha upanuzi wa barabara kutoka njia mbili za zamani mpaka njia nane hadi njia 12 katika baadhi ya maeneo pamoja na ujenzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya, Mpiji na Mlonganzila *Overpass*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali ipo katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu kuanzia Kimara na kuishia Kibaha Maili Moja mbele ya mizani ya

zamani takribani mita 150 kutoka mizani ilipo. Barabara hii inayopanuliwa ina jumla ya kilometra 19.2. Lengo la mradi huu ni kupunguza msongamano mkubwa wa magari yanayopita katika barabara hiyo ambayo yanazidi magari 50,000 kwa siku ikizingatiwa kuwa Jiji la Dar es Salaam ni kitovu cha biashara hapa nchini na kuna bandari inayotumiwa na nchi jirani za Malawi, Zambia, Burundi, Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi *Estim Construction Co. Ltd* wa hapa nchini kwa gharama ya Shilingi bilioni 140.45 na kusimamiwa na Kitengo cha Usimamizi wa Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS Engineering Consulting Unit – TECU*). Utekelezaji wa mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Hadi sasa utekelezaji umefikia asilimia 48 na mradi umepangwa kukamilika mwezi Januari, 2021.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Silvestry Francis Koka swali la nyongeza.

MHE. SILVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kweli nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Kibaha kumpongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa kazi nzuri ya ujenzi wa daraja lile la Ubungo, lakini vilevile barabara hii kubwa ambayo kwa sasa itaishia Kibaha na itaokoa għarama kubwa za msongamano wa magari kutoka Mjini Dar es Salaam kuja Pwani. Pamoja na pongezi hisz kubwa, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ambayo ni kilometra 19.2 inaishia kidogo tu baada ya mizani ya zamani pale Kibaha. Maana yake ni kwamba ile *traffic* ya magari yote ambayo yatakuwa yanakwenda mikoani yatakuja kwa kasi na yataishia pale ambapo ni *almost* katikati ya mji wetu mdogo wa Kibaha. Kwa maana hiyo ni kwamba Mji wetu wa Kibaha magari yatakuwa mengi na hakika utakuwa umesimama wananchi wa Kibaha hawataweza kufanya

shughuli zao za kiuchumi katika mji ule kwa sababu ni mdogo na magari yatakuwa mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao chetu cha *Regional Road Board* tuliomba barabara hii angalau iongezewe mpaka pale Kwa Mathias ili sasa iweze kuhudumia Mji ule wa Kibaha na kuleta maana njema zaidi ya maendeleo katika mji wetu. Vilevile kama tutamwongeza mkandarasi huyu aliyepo kazini gharama zitapungua kwa maana hakutakuwa na *mobilization* hata *process* za tenda. Je, Serikali ina mpango gani sasa kukubaliana na ombi letu ili barabara hii iweze kuleta manufaa zaidi katika mji wetu wa Kibaha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili barabara Kwa Mathias hadi Msangani ambayo inakwenda mpaka Makao Makuu ya *Land Force* tumejenga mita 400 za lami na barabara ya TAMCO kwenda Mapinga inaendelea kujengwa kilometra 4 na wananchi hawajapata fidia. Je, Serikali ina mpango gani kukamilisha barabara hizi na kuhakikisha wananchi wanapata fidia? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nizipokee pongezi nyingi alizotoa Mheshimiwa Koka lakini pia nimpongeze sana kwa juhudhi anazofanya kwa kushirikiana na Mkoa wa Pwani kuhusu maendeleo mbalimbali ya Jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anazungumzia juu ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kutoka eneo ambalo tunaishia kwa maana ya Maili Moja kwenda mpaka Kwa Mathias. Kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi ni kwamba ujenzi wa kilomita 19.2 ni awamu

ya kwanza. Kwa hiyo, tutaendelea na awamu zingine kadri tunapopata pesa kwa maana ya kuendelea na ujenzi kwenye eneo hili kupita Picha ya Ndege - Kwa Mathias - Mlandizi – Chalinze. Kwa hiyo, nimtoe hofu tu tumejipanga vizuri na Serikali tunafahamu kwamba baada ya upanuzi huo wa barabara kwa kweli tutaleta magari mengi sana kwa upande wa Kibaha na maeneo haya Mlandizi kwa maana hiyo tutakuwa tumehamishia foleni kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, tumejipanga vizuri kwamba tutakuja na awamu zingine ili tuweze kutatua na kuendelea kufanya maboresho makubwa ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amezungumzia barabara ile ya Kwa Mathias kwenda Msangani na barabara ya kutoka TAMCO kwenda Mapinga ambayo ni kilometra 24 na tumeshapata wakandarasi kuanza ujenzi katika maeneo haya. Nlmhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba suala la fidia tunalishughulikia kwa sababu ni utaratibu na kanuni kwamba kabla mkandarasi hajaanza kazi fidia zitakuwa zimelipwa. Tunafanya jitihada za kuwasiliana na wenzetu Wizara ya Fedha ili tuweze kulipa fidia. Pia niwahakikishie tu wananchi wa maeneo haya waondoe hofu tumejipanga kuwafanya maboresho ya barabara zao lakini pia tutawalipa stahili zao za fidia kama ilivyo kulingana na taratibu zetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swal lake.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza kabisa, kabla ya kuuliza swal langu, naomba uniruhusu niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunifariji wakati wa kipindi kigumu nilipoondokewa na baba yangu. Nawashukuru sana kwa mapenzi yao na ninawashukuru wananchi wa Mkoa wa Kigoma. (*Makof!*)

Na. 24

Tatizo la Mawasiliano ya Simu – Kigoma

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Maeneo ya mipakani katika Wilaya za Kakonko, Kibondo, Kigoma Vijijini, Buhigwe na Kasulu yanakabiliwa na tatizo la mawasiliano ya simu kutokana na kukosekana kwa minara ya simu:-

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika maeneo ambayo hayana minara Mkoani Kigoma ili kuondoa tatizo la mawasiliano kwa Wananchi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Gezabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote mwezi Julai 2019, ilitangaza zabuni kwa ajili ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 521 zenye vijiji 1,222 nchini. Zabuni hii ilifunguliwa Oktoba, 2019 na baada ya tathmini yake maeneo yaliyopata wazabuni nchi nzima na maeneo mbalimbali ni kama yafuatavyo:-

(i) Kwa upande Wilaya ya Kakonko, nikizungumzia Mkoa wa Kigoma kata zilizopata miradi ni Kata za Nyamtukuza na Rugenge, Kijiji cha Kasongati;

(ii) Katika Wilaya ya Kigoma Vijijini, ilikuwa ni Kata ya Ziwanu ikijumuisha Vijiji vya Kalalangabo na Kigalye;

(iii) Katika Wilaya ya Buhigwe, tulikuwa na Kata ya Mugera, Kijiji cha Katundu; na

(iv) Katika Wilaya ya Kasulu, ilikuwa Kata ya Kitanga na Kijiji cha Kitanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maeneo yaliyopata wazabuni, utekelezaji utaanza mapema mwezi wa Desemba, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Upande wa Wilaya ya Kibondo, Kampuni ya Simu ya Viettel (Halotel) itajenga mnara ili kufikisha huduma za mawasiliano katika Kijiji cha Kibuye ambapo wanatarajiwu kuanza mwisho wa mwezi Desemba, 2019.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya hizo nilizozitaja, vipo vijiji ambavyo ukipiga simu mawasiliano unayoyapata ni ya nchi jirani ya Burundi siyo Tanzania. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kakonko ipo Kata ya Mgundu, kipo Kijiji cha Kigra na Chulazo ambavyo mawasiliano yake ni ya shida. Hata katika wilaya nilizozitaja viko vijiji ambavyo havikuweza kutajwa kwenye jibu la Waziri ambavyo mawasiliano yake bado ya wasiwasi. Je, Serikali iko tayari kuendelea kuhamasisha makampuni kujenga minara katika maeneo hayo ili wananchi waweze kupata mawasiliano ya uhakikika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza Mheshimiwa Josephine Gezabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Josephine Gezabuke kwa jinsi

anavyopambana kuhakikisha kwamba wananchi katika maeneo mbalimbali hasa ya Mkoa wa Kigoma na maeneo mengine ambayo yapo mpakani ya nchi yetu yanapata mawasiliano ya uhakika bila muingiliano kutoka nchi nyingine za jirani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kujibu swali lake, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*) tumeendelea kuwasiliana na nchi jirani ili sheria iliyowekwa kutokana na Mkataba wa *East Africa Communication* uwe unawenza kutekelezwa vizuri. Utaratibu unataka mnara wa mawasiliano uwekiwe kilometra 5 toka eneo la mpaka kwa kila nchi ili wananchi wanaohusika waweze kupata mawasiliano kutoka nchi husika lakini kuna maeneo ambayo kwa nchi za wenzetu wamekiuka utaratibu huo. Katika kikao kinachotegemewa kukaa mwezi Februari, 2020 tunategemea *East African Communication* wata-resolve suala hilo kwa sababu kuanzia Julai limekuwa likijadiliwa ili kuhakikisha wananchi amba wanapaswa kupata mawasiliano ya nchi husika wanaendelea kupata bila kuingiliana na watu wengine. Hilo linahusu vilevile na muingiliano wa masuala ya redio. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, sasa aulize swali lake.

Na. 25

**Fidia kwa Wananchi waliopisha Miradi ya
Mchuchuma na Liganga**

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA aliuliza:-

Kumekuwa na uhakiki wa mara kwa mara wa maeneo ya watu waliopisha miradi ya Mchuchuma na Liganga:-

Je, ni lini wananchi hao waliopisha na kutoa maeneo yao watalipwa fidia?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi alivyo makini katika kuwakilisha wananchi wake katika mradi huu muhimu hapa nchini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumekuwa tukijibu mara kwa mara, Serikali imeendelea kuipanga kutekeleza miradi ya kimkakati awamu kwa awamu sambamba na kuandaa wataalam wenye ujuzi wa kutosha katika kuendeleza miradi hiyo kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mradi huu muhimu wa Chuma cha Liganga chenye ujazo wa takribani tani milioni 126 na makaa ya mawe tani milioni 428 ikiwa ni pamoja na kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la mradi, Serikali imeendelea kutafuta fedha ili kukamilisha ulipaji huo wa fidia. Nikuahidi Mheshimiwa Mbunge, Serikali itatekeleza ahadi hiyo mara pale hali ya kifedha itakaporuhusu ikizingatiwa kuwa kwa sasa iko katika majukumu mengine muhimu yanayofanana na hayo yakiwemo ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwl. Nyerere, ujenzi wa Vituo vya Afya pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa uwekezaji wenye tija unaohusisha kufanya tafiti stahiki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, swali la nyongeza.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanzaa, suala la kuanza Miradi ya Liganga na Mchuchuma nimekuwa nikililiza mara nyingi katika Bunge lako na nimekuwa nikiuliza mfulizo miaka yote. Kwa hiyo, kuhusu fidia imikuwa ni sintofahamu kubwa kwa wananchi wa maeneo ambayo miradi hii inatakiwa kufanyika. Je, kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa wananchi hao kuendelea kuyatumia maeneo hayo mpaka hapo itakapokuwa tayari kulipa fidia hizo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, imikuwa ikiwekwa bajeti miaka miwili mfululizo sasa juu ya ulipaji wa fidia. Kwa nini Serikali isilipe fidia wakati inaweka kwenye bajeti zake? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, kama ifuatavyo:-

Katika suala la wananchi kuendelea kutumia maeneo hayo mimi kwa mtazamo wangu naweza nikasema kwamba wanaweza kuendelea kutumia katika misingi ya kilimo na shughuli zile ambazo hazitakuwa na uwekezaji mkubwa ili kuhakikisha kwamba wanaweza kupata tija inayotokana na matumizi hayo lakini masuala ya ujenzi au kuwekeza kwa gharama kubwa zaidi na kwa sababu tayari tathmini imeshafanyika ni vema wasifanye hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu bajeti imikuwa ikitengwa lakini haipatikani, kama nilivyosema hapo awali kwamba kutenga bajeti ni namba moja lakini upatikanaji wa fedha unategemeana na makusanyo yetu lakini pia matumizi kutegemeana na mahitaji na vipaumbele tunavyojoivekea. Sasa tumeona badala ya kulipa fidia wakati mradi huu hauendelezwi kwa sasa ni vema hela zikaelekezwa kwenye yale maeneo ambayo tayari miradi inatekelezwa ili sasa

miradi hiyo iendelee kuwezesha kuzalisha fedha nyingi zaidi zitakazowezesha kukamilisha hata hiyo miradi mingine ya kimkakati.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ili tusipate wakati mgumu, wananchi wanaruhusiwa kufanya shughuli zao kwenye maeneo hayo? Kwenye jibu lako la swali la nyongeza la swali la kwanza, je, wanaruhusiwa sasa kwenda kulima na kufanya shughuli nyingine ukiacha hizo za ujenzi?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni kawaida kwa masuala ya kilimo hata maeneo ambayo yana uwekezaji ulimaji wa kawaida huwa upo tu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Nadhani Mheshimiwa Mbunge amesikia atawapelekea majibu watu wake.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Jaku.

Na. 26

Bidhaa za Zanzibar kuwekewa Vikwazo Tanzania Bara

MHE. JAKU HASHIM AYUOB (K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA) aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko ya bidhaa zinazozalishwa Zanzibar kupata vikwazo kuingia katika Soko la Tanzania Bara:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuondoa tatizo hilo katika kulinda misingi ya Muungano hasa baada ya maziwa na sukari kuwekewa vikwazo zaidi?

(b) Je, Zanzibar inaweza vipi kutumia Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati soko la ndani bado bidhaa zinazozalishwa zinawekewa vikwazo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ussi Pondeza Mbunge wa Chumbuni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka utaratibu mahsusii wa kushughulikia changamoto zisizo za Muungano zikiwemo za kibashara ili kuimarisha Muungano wetu. Utaratibu huo huendeshwa kwa kutumia vikao vya ushirikiano wa kisekta ambapo Ofisi ya Makamu wa Rais imetoa mwongozo kwa sekta za pande mbili za Muungano kujadili changamoto kuititia vikao kuanzia ngazi ya Wataalam, Makatibu Wakuu na Mawaziri na kushauri mamlaka za maamuzi. Utaratibu huo unazingatia pia kutekeleza matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 katika kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya utaratibu huo, Sekta ya Viwanda na Biashara kwa nyakati tofauti imekuwa ikipokea, kujadili na kutafutia ufumbuzi changamoto za biashara zilizoibuliwa kutoka pande zote mbili za Muungano. Baadhi ya bidhaa zilizowahi kushughulikiwa chini ya utaratibu huo ni pamoja na kuku, sukari, maziwa na bidhaa nyinginezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuititia utaratibu huo, mwaka 2019 Wizara ya Viwanda na Biashara (SMT) na Wizara ya Biashara na Viwanda (SMZ) kwa pamoja zilipewa maagizo ya kushughulikia malalamiko kuhusu suala la sukari kutoka Zanzibar kuingia Tanzania Bara. Wizara hizo ziliunda Timu ya Pamoja ya Wataalam ambao walichambua suala hilo na kuwasilisha taarifa yake kwa Viongozi wa Wizara hizo mwezi Septemba, 2019 kwa hatua zinazofuata. Hivi sasa suala hilo linafanyiwa kazi kuititia ngazi zilizobainishwa ili hatimaye

maamuzi yaweze kufanyika. Hivyo, namuomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira katika suala hilo na yale yanayofanana nalo yanayoendelea kushughulikiwa ili kupata suluhu ya kudumu, yenye tija na maslahi mapana kwa pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada anazofanya kufuatilia kwa karibu na kushauri namna ya kuboresha na kuimarisha masuala yanayohusu biashara katika pande hizi mbili za Muungano.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jaku, swali la nyongeza.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, subira ina mipaka yake, nisubiri hadi lini maana hata kuna wimbo umeimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, je, ni lini mtairuhusu Zanzibar kujunga moja kwa moja katika soko la Jumuiya la Afrika Mashariki kwa nchi zile za Uganda, Burundi na Rwanda kwa vile soko la Tanzania Bara limefungwa kabisa, Zanzibar hairuhusiwi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa vile Jamhuri ya Muungano ndiyo yenye nguvu katika sekta ya fedha, sera za kodi na ndiyo mhimili mkubwa wa uendesha wa biashara na nchi. Je, hamuoni mnaendelea kuikandamiza Zanzibar kiuchumi kwa vile bidhaa za Tanzania Bara zinaingia Zanzibar bila vikwazo kwa maana kwamba saa 24 milango iko wazi na zinapokelewa na kupigiwa *salute*? Je, lini mtaondosha pingamizi hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali masuala yanayohusu Muungano wa nchi yetu hii ni muhimu na *sensitivity* na ndiyo maana yamewekewa utaratibu maalumu wa namna ya kujadiliana. Kwa hiyo, niseme tu kwamba hayo yote ambayo yanaonekana yanahitaji kufanyiwa maboresho mbalimbali ni vema yakajadiliwa kuititia vikao hivyo ambavyo tumeona ni muhimu sana na vimeduwa vikifanya kazi nzuri sana katika kutatua changamoto za Muungano.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Timotheo Mnzava

Na. 27

Mbegu Bora ya Viungo vya Vyakula

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA (K.n.y. MHE. DUNSTAN L. KITANDULA) aliuliza:-

Kata za Kigongoi, Mhinduro na Bosha Wilayani Mkinga zinalima kwa wingi viungo vya chakula kama vile hiliki, mdalasini, pilipili manga na karafuu:-

Je, Serikali ipo tayari kuwawezesha Wakulima hao kupata mbegu bora ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao yao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwekeza katika mazao mbalimbali ya kilimo yakiwemo

mazao ya viungo ambayo mahitaji yake yanaendelea kuongezeka ndani na nje ya nchi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (*TARI*) imeanza kufanya utafiti wa kupata mbegu bora za mazao ya viungo na mazao mengine ya bustani aina ya *horticulture* ili kuongeza uzalishaji na tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inapitia Sera ya Kilimo ya Mwaka 2013 ambapo sekta ndogo ya mazao ya bustani ni miongoni mwa maeneo muhimu yanayozingatiwa. Vilevile, kutokana na umuhimu wa mazao hayo, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo itafanya kikao cha wadau wa mazao hayo tarehe 8 Novemba, 2019 ili kuandaa Mkakati wa Miaka Mitano wa Kuendeleza Mazao ya Bustani. Mkakati huo unalenga kuongeza uzalishaji, ubora wa mazao na kuimarisha mifumo ya masoko ya mazao hayo. Aldha, mkakati huo utakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa unaolenga Taifa letu kufikia uchumi wa kati mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hizo, Serikali inaendelea kutoa elimu ya kilimo bora cha mazao ya viungo na mazao mengine; uhifadhi, usindikaji na masoko kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kikiwemo Chama cha Wadau wa Mazao ya Viungo Tanzania (*Tanzania Spices Association - TASPA*), *Sustainable Agriculture Tanzania (SAT)* na vyama vingine vya wakulima.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kabla sijaauliza maswali ya nyongeza, niruhusu niendelee kuwapa pole wananchi wa Jimbo langu la Korogwe Vijijini na Mkoa mzima wa Tanga kwa mafuriko makubwa yaliyotupata siku chache zilizopita. Tunaendelea kutumaini juhudhi ya Serikali kurejesha miundombinu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili

ya nyongeza. Swali la kwanza; moja ya sababu ya nchi tunazoshindana nazo kwenye soko la mazao ya viungo na mazao ya bustani kufanya vizuri ni wao kuwa na mamlaka za kusimamia mazao haya. Je, ni lini Serikali yetu itaona umuhimu wa kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Mazao ya Viungo na Mazao ya Biashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wananchi wa Tarafa ya Bungu, Wilaya ya Korogwe, ni wakulima wakubwa na wazuri sana wa mazao ya viungo na zao la chai, lakini tumekuwa na changamoto kubwa sana ya bei kwenye zao la chai. Je, ni upi mkakati mahususi wa Serikali wa kuhakikisha kwamba wanaboresha bei ya zao la chai ili kuweza kuwaletea tija wananchi na wakulima wa zao la chai nichini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mnzava kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwamba Wizara ya Kilimo inafahamu umuhimu wa kuanzishwa kwa taasisi itakayosimamia mazao ya *horticulture* na mazao ya viungo. Hivi sasa tunapitia mfumo na muundo wa Wizara kupunguza idadi ya bodi na kuanzisha mamlaka chache ambazo hazitazidi tatu, mojawapo ikiwa ni Mamlaka ya Maendeleo ya Mazao ya *Horticulture*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu akijaalia hivi karibuni Bunge hili litapokea sheria ambayo itaonesha mabadiliko ya muundo wa taasisi mbalimbali ndani ya Wizara ya Kilimo ili kuipa sekta hii nafasi inayostahili kwa sababu ni *subsector* ndogo katika Sekta ya Kilimo inayokua kwa kiwango kikubwa sana na inahitaji *attention* inayostahili. Kwa hiyo nimtoe hofu kwamba tuko katika hatua za awali na kabla

ya kufika Bunge Ijalo la Bajeti tutakuwa tumeshaanzisha Mamlaka ya Mazao ya *Horticulture*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la chai; ni kweli kama Serikali hatua tunazochukua mojawapo sasa hivi tuko katika hatua za mwisho za kuanzisha *a primary market* katika eneo la Dar es Salaam ili tuwe na mnada wa kwetu hapa Tanzania. Tumesha-earmark eneo na sasa hivi tuko katika hatua za awali kutengeneza utaratibu ili chai yetu badala ya kwenda kuuziwa katika soko la Mombasa sasa ianze kuuziwa katika soko la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tutatumia mfumo wa *TMX* ili kuwaruhusu wanunuzi duniani waweze ku-*bid*. Mchakato huu unawahusisha Sekta Binafsi ambao wamewekeza katika chai ili kuhakikisha kwamba zao la chai linapata soko na bei ya uhakika. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tunaamini kwamba ndani ya muda mfupi tutaanzisha soko la kwetu ndani ya Tanzania na chai yetu itauziwa hapa na itapunguza gharama na kumpatia mkulima bei nzuri.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Katika Mkoa wa Simiyu tayari mbegu za pamba zimeshaanza kusambazwa na kupata mbegu za pamba kwa wakulima mpaka uzinunue. Wapo baadhi ya wakulima bado hawajalipwa pamba na wanunuzi; je, Serikali inawasaidiaje ili wakulima hao waweze kupata mbegu za pamba?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua tatizo hilo alilolisema Mheshimiwa Leah Komanya, ni kweli kampuni binafsi na ningeomba kuititia Bunge Watanzania wote wakaelewa;

walionunua pamba sio Serikali ya Jamhuri ya Muungano, walionunua pamba ni kampuni binafsi za Watanzania, lakini tunafahamu kwamba Watanzania wote hawajalipwa wanaodai kampuni hizi. Mpaka sasa wameshalipa bilioni 417, wakulima wanadai bilioni 50. Tarehe 14 tutakutana na wanunuzi ili kulitatua tatizo la wao kumalizia kulipa kwa wakulima ili wakulima waweze kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo vilevile makampuni yaliyopewa haki ya kusambaza mbegu bora katika maeneo ya wakulima wa pamba nao tutakutana nao ili kutengeneza utaratibu ambao hautowalazimisha wakulima wanaodai kulazimishwa kulipia mbegu ya pamba. Tutatengeneza utaratibu ambao utamfanya mkulima kama anaidai kampuni kampuni hiyo impe mbegu wakati anamlipa atakata gharama yake ya mbegu alizompatia. Kwa hiyo tarehe 14 tutamaliza tatizo hilli na hilli halitakuwa tatizo tena muda mfupi ujao.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu.

Na. 28

Kushuka kwa Bei ya Nazi Nchini

MHE. ZAYNAB M. VULU (K.n.y. MHE. MBARAKA K. DAU)
aliuliza: -

Bei ya zao la nazi imekuwa ikishuka kwa kasi kubwa katika miezi ya hivi karibuni: -

- (a) Je, ni zipi sababu za kushuka kwa bei ya zao hilo?
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuokoa zao hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)

alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swal i Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kushuka kwa bei ya zao la nazi ni pamoja na:-

Uwepo wa wanunuzi wachache wa nazi na hivyo kutokuwepo kwa bei ya ushindani ikilinganishwa na misimu iliyopita; kupanda kwa gharama za usafirishaji wa nazi kutoka Sh.2,800 miaka mitatu iliyopita na kufikia Sh.5,500 kwa gunia lenye nazi 200 mwaka 2019; kupungua kwa wanunuzi wakubwa wa viwanda vya mafuta ya nazi na bidhaa zake; kuongezeka kwa matumizi ya bidhaa mbadala za nazi kama vile mafuta ya kula ya mawese toka nje ya nchi na matumizi ya mafuta ya kupaka yasiyotokana na nazi; kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola na kushuka kwa mfumuko wa bei toka asilimia 11 kwa mwaka 2006 mpaka asilimia nne mwaka 2018/2019; kushuka kwa uzalishaji wa nazi nchini kutokana na magonjwa na mabadiliko ya tabia ya nchi ambayo yamesababisha kupungua kwa uzalishaji wa nazi na kutowavutia wawekezaji wa ndani na nje kwa sekta ya viwanda vya kuchakata nazi kutokana na hofu ya kukosa malighafi ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inafanya jitihada za kuongeza wawekezaji katika zao la nazi kwa lengo la kumpatia mkulima soko la uhakika na bei nzuri. Jitihada hizo ni pamoja na kutoa elimu katika mnyororo wa thamani wa zao la nazi ikiwa ni pamoja na kuwapatia wakulima mashine za kukamua mafuta ya nazi. Hadi kufikia tarehe 30 Septemba, 2019, Vikundi vya Wajasiriamali vya Tujitegemee na Kaza Moyo vimepatiwa mashine zenye uwezo wa kukamua mafuta ya nazi lita 400 kwa siku ambapo lita moja huuzwa kati ya Sh.8,000 hadi Sh.10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali inaendelea kutafuta masoko ya mazao yote ya kilimo likiwemo zao la nazi kwa kuwaunganisha wakulima na wanunuzi kuititia vikundi na vyama vya ushirika. Vilevile, Serikali inaendelea kuweka miundombinu ya usafiri kwa kuunda kivuko kitakachowezesha kuwaunganisha wananchi wa Mafia na sehemu zingine kwa usafiri kutoka Mafia hadi Nyamisati, Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti na hivyo kuwawezesha wakulima wa Mafia kusafiri na mizigo yao pamoja na nazi kwenda Dar es Salaam ambapo watauza kwa bei nzuri katika masoko makubwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, swali la nyongeza.

MHE. ZAYNAB M. VULU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imebaini kwamba kuna tatizo la soko; na kwa kuwa Serikali imebaini kuna uhaba wa zao lenyewe na watumiaji. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuweka mkakati madhubuti wa kuwatufutia wakulima hawa soko la nje waweze kusafirisha nazi zao kwenda nje ya nchi kwani hapa Tanzania kwa mujibu wa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri inaonekana kwamba soko limepungua? Pia wangeweza kutoa elimu ya kutosha watu wakajua matumizi na thamani ya zao la nazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; bila shaka Naibu Waziri anajua thamani ya zao la nazi, zao la nazi lina thamani kubwa sana. Kwanza mti wenyewe unatumika kama mbao, unatumika kwa kutengenezea *furniture*, mti wenyewe unatoa nazi, nazi inatoa tui ambalo linapikiwa, nazi ina maji ambayo yanatumika kwa afya zetu; nazi machicha yake yanatumika kwa ajili ya kutengenezea kashata na vitu vingine, lakini pia mnazi huohuo unatoa makuti ambayo yana thamani katika utalii wetu wa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo mnazi huo huo unatoa kitu kinaitwa kitale, kitale kina thamani kubwa

sana watu wa afya wanaweza wakajua na watu wa Pwani wanaweza wakaelewa thamani ya kitu kinachoitwa kitale. Sasa ni lini Serikali itaweka mkakati wa kuhakikisha zao hili la nazi halipotei nchini kwetu kwa kurudisha vituo vytafifi viliviyokuwa Dar es Salaam, Mafia, Bagamoyo na Lindi ili wakulima wale wasiweze kupoteza thamani ya zao la nazi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anataka kujua mikakati ya Serikali kutafuta soko la nazi nje ya nchi; ni kweli kwamba kama Serikali tuna mikakati mbalimbali lakini tufahamu kwamba matatizo makubwa ya soko la nazi sio bei, tatizo kubwa ni kipato kidogo wanachopata wakulima wa nazi na kipato hicho kinaweza kuongezeka kutokana na bei kubwa au tija kuongezeka au kuongeza uzalishaji, lakini pia kupunguza gharama za uzalishaji wakulima hao wa nazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Serikali moja ambalo ndiyo tumeanzisha vituo vytafifi hivi 16, kimojawapo ni Kituo chetu Cha Utafiti cha pale Mikocheni ambacho kimepewa mahususi kwa ajili ya utafiti wa zao la nazi. Lengo ni kuja kupunguza gharama za uzalishaji, lakini kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili ukame na magonjwa kwa ajili ya kuongeza tija na uzalishaji kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anataka kujua ni lini Serikali tutaanza kurudisha vile vituo vyetu vytafifi kama zamani. Kama nilivyosema katika majibu yetu ya msingi, kwanza zamani hatukuwa na vituo vile vytafifi

zaidi ya hiki cha Mikocheni, tulikuwa na vituo vya kuzalisha miche ya minazi na baadaye kuisambaza kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo utaratibu mpaka sasa hivi tunao, tunacho kule Zambezi Bagamoyo, tunacho pale Mkuranga na tutaendelea kufungua vituo hivyo Mafia na sehemu zingine kwa wakulima wakubwa wa nazi, lakini hasa baada ya kupata taarifa za utafiti kutoka kwenye kituo chetu hiki cha *TAR*/pale Mikocheni ambacho tumewapa mahususi kwa ajili ya kufanya utafiti wa zao la nazi ili kuja sasa na mbegu ambayo inahimili ukame na magonjwa tuachane na mbegu yetu ile fupi tulioletewa kutoka nje ambapo kule ni nchi ambazo ni za baridi, haiwezi kuhimili kutokana na hali ya joto na hali ya mazingira ya nchini kwetu. Kwa hiyo, nitoe wito kwa wakulima wote; sasa hivi tunasisitiza tutumie mbegu yetu ile ya asili ya *East African Tall* ambayo inahimili ukame, joto na mazingira yetu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumalizie swalii letu la mwisho, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalii lake.

Na. 29

Kuliwezesha Shirika la Mzinga

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA aliuliza:-

Shirika la Mzinga limekuwa likifanya kazi zake kwa weledi na uaminifu mkubwa lakini lina changamoto za vifaa kama vile mashine za ramani:-

Je, kwa mwaka 2019/2020 Serikali ilitenga kiasi gani cha fedha kwa ajili ya Shirika hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Shirika la Mzinga limetengewa jumla ya shilingi 2,000,000,000.00 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha shirika linatekeleza majukumu yake kwa ufanisi, shirika limeanza kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2017/2018 – 2021/2022) ambao unakusudia kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kijeshi. Aidha, shirika limepanga kuanzisha kiwanda cha kutengeneza baruti kwa ajili ya matumizi yasiyo ya kivita (*civil explosives*) na kupanua mradi wa kutengeneza mashine ndogo ndogo zitakazowezesha wajasiriamali kuongeza thamani ya mazao ya killimo na misitu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maryam Msabaha, swalii la nyongeza.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri maswali mawili madogo ya nyongeza. Swalii la kwanza, shirika limekuwa likipata tenda kutoka ndani ya Serikali na limekuwa likifanya kazi hizi kwa weledi mkubwa sana. Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha shirika linalipwa kwa wakati ili hata zile changamoto ndogondogo wanapopata zile hela kwa wakati wapate kuzitatua wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; miundombinu ya haya mashirika, hiki Kikosi cha Mizinga kwenye makambi mengi ni chakavu na si rafiki sana na ni siku nyngi. Sasa Serikali ina mikakati gani ya kutenga fedha na kuangalia hiki kitengo kwa sababu hiki kitengo ni kwa kazi maalum na kinafanya kazi kwa ujasiri na kwa weledi mkubwa. Je, Serikali na Wizara ya Fedha ina mkakati gani kuhakikisha kwamba kile kinachotengwa kwa ajili ya kitengo hiki kinapelekwa ili kutoa hizi changamoto ambazo zipo katika Kikosi hiki cha Mizinga katika hili Shirika la Mzinga? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maryam Msabaha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malipo kwa kazi ambazo shirika linafanya za Serikali naweza nikamueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba malipo hayo yanafanyika. Hivi karibuni Shirika la Ujenzi la Mzinga limepata kazi kadhaa ikiwemo ujenzi wa ofisi za Serikali hapa Dodoma, lakini katika baadhi ya halmashauri pia wamekuwa wakipata kazi. Kwa taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba malipo yanafanyika na fedha hizo zinawasaidia kuboresha mambo madogomadogo katika shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu miundombinu ya shirika lenyewe; ni kweli kwamba kwa kiwango kikubwa miundombinu pale katika Shirika la Mzinga imechakaa, ni ya muda mrefu na ndiyo maana kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba sasa wametengeneza mpango mkakati ambao kwa kiwango kikubwa ukipata fedha utaweza kushughulikia yote haya ikiwemo kuboresha miundombinu, lakini kuleta wataalam wallobobeat katika fani hizo na kuwa na mtaji wa kuweza kuendeleza shirika hili. Ni matumaini yetu kwamba mpango mkakati huo utapitishwa na Serikali ili shirika liweze kupata fedha na kuweza kuboresha miundombinu yake.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo Kwanza ni tangazo la wageni waliopo Bungeni siku ya leo. Tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika, na hawa ni wageni wa Mheshimiwa Spika.

Wa kwanza ni ndugu Faustine Martine Kasike ambaye ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, karibu sana. Karibu sana, karibu sana Kamishna wa Magereza. (*Makof*)

Pia, tunaye ndugu Mgongoro Jonathan ambaye ni mwandishi wa vitabu, karibu sana. Tunao pia wageni kutoka Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania na Shirika la *Karagwe Community Based Rehabilitation Program* wakiongozwa na Katibu wao ndugu Mussa Kabimba. Karibuni sana, karibuni sana. Tunao pia wageni kutoka Shirika lisilo la Kiserikali la *Tangible Initiatives for Local Development Tanzania*, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo ndugu Christina Kamili, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na wageni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, wageni 26 ambaao ni Wachungaji wa Makanisa ya Kipentekoste kutoka Tukuyu, Mkao wa Mbeya wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mchungaji John Mwakapugi. Karibuni sana, karibuni sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni wanne (4) wa Mheshimiwa Juma Hamad Omar ambaao ni familia yake kutoka Zanzibar wakiongozwa na mke wake ndugu Zamda Mnete. Karibu sana, karibu sana, karibuni sana. (*Makof*)

Zamda Mnete ndio yupi kati yenu! Ndiyo wifi yetu huyo jamani, karibu sana. Wengine shemeji yao, naona wanaume walikuwa wanaona wametengwa kidogo hivi!

Tunao pia wageni wawili (2) wa Mheshimiwa Maftaha Nachuma ambaao ni viongozi wa wafanya biashara kutoka Mkao wa Mtwara, na hawa ni ndugu Abilahi Shilingi na ndugu Twaha Ngozoma, karibu sana. (*Makof*)

Tunao pia wageni 12 wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab ambaao ni Viongozi wa Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUWA), wakiongozwa na Mwenyekiti Taifa

ndugu Hassan Mchanjama. Karibuni sana, karibuni sana.
(*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge tuonao pia wageni ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo, nao ni wanachuo 40 kutoka Chuo cha Uhasibu Arusha ambao wameongozwa na Rais wa Chuo hicho ndugu Laurent Wilson, karibuni sana (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge hao ndiyo wageni tulionao Bungeni siku ya leo, lakini pia lipo tangazo kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali watu. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba Wabunge ambao ni Mabalozi wa Usalama Barabarani kwamba, *TAWLA* wameandaa semina ya kuwajengea uwezo juu ya athari za kiafya na kiuchumi zinazosababishwa na ajali za barabarani. Semina hiyo itafanyika *Nashera Hotel*, Dodoma kuanzia Saa 07:30 mchana mpaka Saa 10:30 jioni leo tarehe 06 Novemba, 2019. Orodha ya Wabunge ambao ndiyo wanaoalikwa huko itakuwa Lango A la kuingilia hapa Bungeni.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge majina ya Wabunge wanaoalikwa huko yapo Lango A yakaangaliwe huko. Kama hukualikwa basi nadhani sasa wapo wahusika wenyewe wanaotakiwa kwenda huko, usije ukajikuta unarudishiwa mlangoni.

Pia, lipo tangazo la Mwenyekiti wa Jumuia ya Mt. Thomas More hapa Bungeni, Mheshimiwa Shally Raymond, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa siku ya leo kutakuwa na Ibada ya Misa ya Wakristo Wakatoliki saa saba mchana mara baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote na wageni wote mlioko Bungeni mnaalikwa katika misa hiyo ambayo itafanyika Jengo la Pius Msekwa, ghorofa ya pili.

Waheshimiwa Wabunge hayo ndiyo matangazo tuliyokuwa nayo siku ya leo tutaendelea na ratiba yetu. Katibu!

MHE. ANATROPIA K. THEONEST: Mwongozo.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Hoja ya kuahirisha mjadala wa Bunge unaoendelea.

MHE: ANATROPIA K. THEONEST: Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwakajoka.

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ili niweze kutoa mwongozo wangu kwenye suala la dharura ili Shughuli za Bunge ziweze kuahirishwa tuweze kujadili jambo la dharura katika Bunge letu. Kutokana na jambo ambalo jana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ametoa ufanuzi kwamba kutokana na malalamiko ya mchakato wa uchaguzi ambao unaendelea sasa hivi wa Serikali za Mitaa kwamba jana na leo iwe ni siku ya kupeleka pingamizi ya wale wote ambao walikuwa wameondolewa kwenye mchakato huo. Lakini cha kushangaza ni kwamba mpaka sasa hivi Watendaji toka asubuhi hakuna ofisi yoyote iliyofunguliwa, ofisi zote za wasimamizi wa uchaguzi zimefungwa na hakuna kinachoendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wananchi wanataka kupata kauli ya Serikali, hivi taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Waziri jana ni kwamba Wasimamizi wa Uchaguzi katika maeneo yote na Wasimamizi Wasaidizi wamegoma kauli ile kwamba hawawezi kutekeleza na jambo hili halitafanyika kama ambavyo amezungumza na nini kifanyike? Kwa sababu tunaona ni jinsi gani ambavyo kuna dhamira ovu ya kuvuruga uchaguzi na kuvuruga amani na mshikamano wa Taifa hili kwa sababu ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunataka tupate ufanuzi pia kutokana na jambo hili ili ikiwezekana Bunge lako lijadili, kwa idhini yako Bunge lijadili jambo hili la dharura na lina maslahi mapana ya Taifa, lakini pia linaweza kusababisha mvutano mkubwa, lakini pia na uvunjifu wa amani katika Taifa hili. Tunashangaa sana kwanini jambo hili

Serikali inalifumbia macho na lisii chukulie kama ni jambo la msingi. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anatropia.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ANATROPIA R. THEONEST: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasimama kwa Kanuni ya 47 sitaisoma, lakini suala ninaloongelea hata gazeti la Mwananchi wameandika, "Wapinzani walia kila kona Chaguzi za Serikali ya Mitaa". Tunataka ufanuzi, kuna mambo yamefanyika huko kwenye mchakato wa kurudisha fomu wa Serikali ya Mitaa ambao wakati mwingine ukiyafikiria unashindwa kuelewa dhamira. Eti mgombea anaenguliwa kwa madai kwamba Chama cha CHADEMA, Chama ACT Wazalendo, Chama cha CUF, NCCR na vyama vingine kwamba havijasajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka ufanuzi, tunataka tusikie kauli ya Serikali; Je, nini dhamira yake? Ni dhamira ya Serikali kuona nchi inajaa machafuko kwa kuminya haki za wananchi kufanya uchaguzi? Au, na kama dhamira yake ni kulinda amani, itangaze mchakato uangaliwe upya kwa maana ya watendaji ambao wamewaondoa wagombea kwa hila, kwa kasoro ndogondogo, lakini kwa kuonesha kwamba walikuwa na lengo la kuitisha wagombea wa CCM bila kupingwa. Watoe kauli, watoe maagizo kwamba huo mchakato batili urejewe upya na tupate haki zetu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Maftaha.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Jana nilisimama kwa Kanuni ya 69(1), na leo naomba nisimame tena kusimamia hoja yangu ambayo *nili-raise* jana kwamba mjadala wa Bunge unaoendelea kujadili Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2020/2021 uahirishwe kwa sababu ya suala hili ambalo naenda kulizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilisema kwamba uchaguzi huu ambao Wapinzani wameenguliwa nchi nzima, maeneo yote ya ngome za Chama cha Wananchi - CUF, CHADEMA, NCCR, ACT, Wapinzani wote wameenguliwa. Hivi sasa ninavyozungumza kuna taharuki kubwa sana huko mitaani, wananchi wanatupigia simu sana kama viongozi wa vyama vyaa siisa wanatuuliza tufanye nini. Tunawaambia tulieni, tulieni, tulieni, kwa hiyo, kuna taharuki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sisi Bunge tunajadili Mpango wa Maendeleo na hakuna maendeleo bila amani, duniani kutakuwa na maendeleo bila amani. Nilikuwa naomba kutoa hoja katika Bunge lako tukufu kwamba liweze kujadili hili suala tuweze kujadili amani ya Watanzania kwa kufuata demokrasia ya vyama vingi. Hivi sasa kama unavyoona wapinzani walivyoenguliwa wote jana tulielezwa kwamba tulete vielelezo hapa, leo nimekuja na vielelezo ninavyo kibao hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba tuwasilishe mezani Wabunge nitoe hoja ya kujadili suala hili kwa sababu ni suala muhimu sana kwa mustakabali wa taifa letu hili, vinginevyo nchi haitakuwa sawa sawa. Hatuwezi kama Wabunge kujadili maendeleo hapa wakati huko hali haiku sawa sawa. Naomba kutoa hoja Waheshimiwa Wabunge, naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kujadili hili suala. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Naomba mkae, Mheshimiwa Musukuma.

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nilikuwa naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) kwenye swali Na. 18 lilitolizwa na Mheshimiwa Zitto wakati Serikali ikitoa majibu na swali la nyongeza lilitolizwa na Mheshimiwa Mlinga imeeleza vizuri tu kwamba Halmashauri ya Ujiji imepata hati chafu kwa miaka minne. Nimekuwa Mwenyekiti wa Halmashari, upo mwongozo unaotuelekeza kwamba Halmashauri inapopata hati chafu mara tatu inatakiwa kufutwa na kuwa kwenye usimamizi mkali. Pia imeelezwa na Mheshimiwa Waziri kwamba, moja

ya sababu inayosababisha kupata hati chafu kwenye halmashauri hiyo ni pamoja na mvutano wa Waheshimiwa Madiwani na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kufahamu, kama tumeshaingia hasara miaka minne, tunaenda mwaka wa tano tunajua kabisa tunaenda kudumbukia kulekule. Ni nini hatua ya Serikali kutekeleza Waraka wa kuifuta Halmashauri ya Ujiji ili iweze kuwa kwenye uangalizi wa Kamati?

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijajibu mambo ambayo yameelezwa na Wabunge hapa. Kuna wageni wa Mheshimiwa Spika ambao wameingia sasa hivi hapa Bungeni, na mmoja ni Mheshimiwa Balozi wa Canada nchini Tanzania, Bi. Pamela O'Donnell. (*Makofi*)

Honorable Pamela, can you stand up! Karibu sana, karibu sana. (*Makofi*)

Pia, tunaye Bi. Sandra Rossiter ambaye ni *Councilor Political Economic and Public Affairs*, naye anatoka Ubalozi wa Canada, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgani wa Mheshimiwa Joyce Sokombi ambaye ni Hilda Newton, karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Frank Mwakajoka akiomba mwongozo halafu akatoa maelezo kwamba ni jambo la dhararu ambayo wote mmeyasikia. Ameeleza mambo kwa kirefu yanayohusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na jambo ambalo alilitolea ufanuzi Mheshimiwa Jafo. Pia, amesimama Mheshimiwa Anatropia Theonest Rwehikila kuhusu jambo linalofanana na hilo, ye ye akisema anasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47 kwamba ni jambo la dharura na tulijadili. Wakati huohuo amesimama Mheshimiwa Maftaha Nachuma, ye ye amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 69 akiomba Bunge liahirishe jambo linalofanywa sasa ili tuweze kujadili hilohilo jambo linalohusu uchaguzi.

Waheshimiwa Wabunge jambo hili lilianza kujitokeza Bungeni jana na Mheshimiwa Spika alitoa maelezo kwamba alewe vielelezo kuhusu mambo aliyokuwa akiyazungumza Mheshimiwa Maftaha. Mheshimiwa Maftaha wakati huohuo anasema ameleta vielelezo vya kuonesha yale yaliyotokea huko. Kwa hiyo, haya mambo matatu yote yaliyozungumzwa kwa kuwa yanazungumzia jambo moja, na wote wamekiri kwamba Mheshimiwa Jofo alitoa maelekezo jana ambayo yanafanyiwa kazi jana, leo na kesho, maana yake Serikali imeshaanza kuchukua hatua juu ya mambo ambayo yanalamikiwa humu ndani. (*Makofii*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge hatuwezi sisi humu ndani ambao hata hivyo vielelezo hatuna sote kushiriki huu mjadala. Na kwa kuwa Serikali imeshatoa maelekezo na ndicho kilichokuwa kinaombwa hapa, maelekezo na kauli ya Serikali imekwisha kusikika, na kwa kuwa leo ni sehemu ya hizo siku ambazo Serikali inalifanya kazi jambo hilo Serikali inaendelea na utaratibu wake. Kwa mujibu wa Kanuni zetu, sote tunafahamu jambo ambalo linakuwa kwenye utaratibu huo Bunge haliwezi kuingia hapo kufanya kazi. Kanuni ya 47 ambayo inazungumzia udharura wa jambo ni pamoja na hilo jambo kushindwa kufanyiwa kazi katika utaratibu wa kawaida.

Nimeombwa pia mwongozo na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma kuhusu Halmashauri ya Ujiji kupata hati chafu mara nne mfululizo au kwa miaka minne mfululizo, na ameelekea kwenye majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ameeleza jambo hilo kwamba limefanyiwa utafiti ama ukaguzi na inaonesha kwamba hati chafu wote tunafahamu zinatolewa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hiyo maana yake ni jambo liliodhahiri.

Lakini kwenye kuuliza swali kama Serikali ina mpango gani kuhusu kufuta hiyo halmashauri, nadhani Naibu Waziri ameeleza vizuri hapo akijibu swali kwamba wao wanaendelea na utaratibu wao na si Bunge linalofuta halmashauri ni Serikali. Kwa hiyo, Serikali inaendelea na utaratibu wake ikiwa ni hiyo halmashauri haitabadilika ikipata

chafu mara tano mfululizo. Kwa hiyo, tunataka kuamini kwamba, kwa kuwa hilo jambo limezungumzwa hapa ndani wanaohusika katika kuingilia michakato ya manunzi huko Kigoma kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaamini kwamba watajirekebisha na watafanya mambo yatakuwa mazuri kuliko kusubiri mpaka wafutwe na Serikali kama ambavyo wametoa majibu hapa.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kwa yote yaliyokuwa wamesimama Waheshimiwa Wabunge majibu yake ni hayo, lingine tunasubiri Serikali imalize mchakato wake lakini pia hilo la Ujiji limeshatolewa majibu hapa kwa hiyo tutaendelea na ratiba yetu.

Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

NAIBU SPIKA: Kamati ya Mipango!

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati tutaendelea na uchangiaji kama tulivyoanza jana na kwa mujibu wa utaratibu wetu wa kikanuni nimeletewa majina hapa ya wachangiaji kutoka vyama wawakilishi Bungeni. Tutaanza na Mheshimiwa Salim Turky atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa ajiandae.

MHE. SALIM HASSAN TURKY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana wa Taallah kwa kutujalia sisi tulioko humu wazima wa afya. Nachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri wetu wa Mipango kwa kweli mpango alionleta ni mzuri sana na madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea na safari hii pia nataka nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa Chama cha Mapinduzi ambaye ndiyo Rais wa nchi hii, Mheshimiwa

Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayotufanya ya kutaka kuhakikisha kwamba Tanzania tunaingia katika uchumi wa kati. Sitaki kutafuna maneno, wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani na alipotoa matamko yake yale kwa kweli nilipigwa na butwaa nikasema hivi kweli mambo haya yanawezekana kwa kipindi hiki kifupi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ameweza kuthibitisha na mimi nachukua fursa hii kumpigia *salute* kabisa kwamba, kwa kweli anatupeleka kwenye maendeleo makubwa sana japo njia ni ngumu lakini dalili njema zimeshaanza kuonekana. Katika hilo wakati akiwa kama Waziri alikuwa akipiga kelele sana hapa kutaka madaraja yale ya ubungo pamoja na *airport* lakini nashukuru alipoingia madarakani tu alihakikisha daraja lile la pale njia ya *airport TAZARA* linasimama la Mfugale mara moja na limesimama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa sisi ambao tunatoka Zanzibar kuja Dar es Salaam na Dar es Salaam Zanzibar, kwa kweli njia sasa hivi imekuwa ni ya muda mfupi sana. Kwa hiyo, hizi nia ambazo amezipanga, Mwenyezi Mungu azibariki na amjalie afya njema. Kwa wale wanaomtakia mabaya Mwenyezi Mungu amwepushe nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na-declare interest kwamba ni mfanyabiashara pamoja na viwanda, kwa hiyo, mada ambazo nitaongelea ni hizo na nitaanza na viwanda. Juzi moja tulirushiwa *clip* nzuri sana ya viwanda kutoka Ethiopia. Kwa kweli ukitaka kujifundisha jambo lolote, tushindane kwa mazuri. Katika Afrika yetu hii, Ethiopia ndiyo inaonekana kwamba ni nchi moja iliyojizatiti kweli kweli kutokana na umasikini na kuendelea mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walichokifanya wao kama Serikali, wametafuta wawekezaji wakaingia nao ubia, wakajenga eneo kubwa sana la viwanda. Wamejenga eneo hilo na kuwakaribisha wawekezaji. Kwa hiyo, mwekezaji anapokuja nchini, hahangaiki tena kwenda kutafuta maeneo ya kuwekeza, kuanza kutafuta umeme na maji. Hayo

yote yamepitwa na wakati katika dunia hii tunayokwenda nayo. Kwa hiyo, inatakiwa katika eneo hilo sasa hivi Serikali na labda Mheshimiwa Waziri wa Fedha akija katika mipango yake atueleze kwamba amejipanga vipi? Kwa sababu eneo hilo linafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hata katika kurejesha pesa kwake kwa mradi ule, wao watazame zaidi kwamba ile miradi inapokuja nchini, wananchi wetu wapate ajira. Kwa mfano tu leo, Tanzania tuko nyuma sana katika viwanda vya nguo. Tuna pamba ambapo leo Mheshimiwa Waziri ametoa tamko hapa nimemsikia kwamba pamba inayotakiwa kwa viwanda vyetu ni nyngi kuliko tunayozalisha. Kwa hiyo, tayari zile kelele za watu wa maziwa kule kupiga kelele hilo jambo naona limeshapata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ili tutoke hapa, tunafanyaje? Nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mwijage alipokuwa hapa alisema kwamba anataka kila mtu awe anazalisha na kushona nguo. Vita vikubwa vya kushona nguo Tanzania ni kuruhusu mtumba. Mitumba inadumaza viwanda vya nguo. Kama hatutajipanga vizuri, naamini kwamba kuna nguo ambazo tunanunua China zinauzwa rahisi sana. Je, zikishonwa na pamba yetu wenye hapa Tanzania bila kusafirishwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya makusudi kujipanga kuhakikisha kwamba hilo eneo la viwanda linasimamiwa kwa nguvu zote na ile kodi ikawekwa ndogo sana ili wananchi waweze kunufaika na ajira na mapato ya Serikali yatakuwa makubwa sana kwa kuitia huduma mbalimbali katika eneo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, mwanzo wa kipindi hiki cha tano tulikuwa tunasimama hapa Bungeni na kupiga kelele, nami wakati ule nilikuwa niko katika Kamati ya Viwanda na Biashara, tulifanya ziara bandarini na tukasema kwamba sasa hivi watu wote wamekimbia bandari yetu kutohana na tozo zilizopangwa kwa wakati ule; mambo ya VAT na nini yaliyowekwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana ziara ile ilizaa matunda; Waziri na Serikali ambayo ni siku waliona upungufu wakajirekebisha. Sasa hivi naweza kusema kwamba Bandari ya Dar es Salaam imechangamka mia kwa mia. Nampongeza sana Mkurugenzi Mtendaji wa TPA kwa kazi kubwa anayofanya pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mwaka ule wa kwanza watu waliyachukua magari yale ya kusafirisha makontena wakapeleka nchi jirani. Hivi ninavyoongea na Bunge hili, kuna upungufu mkubwa sana wa magari ya kusafirisha *container* katika Bandari yetu ya Dar es Salaam, kwamba biashara imekubali Bandari ya Dar es Salaam. Naipongeza sana Serikali yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili biashara hiyo iwe nzuri zaldi, Serikali imejipanga kwa kujenga bandari kavu mbalimbali. Serikali hiyo hiyo ilitoa tamko kwamba zile *ICD* za watu binafsi zote ambazo ziko katika mji wetu wa Dar es Salaam zihame ziende katika umbali wa kilometra 35 nje ya Dar es Salaam ili kuondoa msongamano wa magari. Hilo ni jambo jema sana ambalo limepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta binafsi iko tayari kujenga *ICD* mbalimbali nje ya Dar es Salaam. Serikali inapanga bandari kavu sehemu mbalimbali, ni jambo jema sana, lakini naomba sana *TPA*, hao watu wanaotaka kujenga *ICD* nje ya Dar es Salaam, walipoenda kuwaomba kwamba waweke wakaambiwa kwamba tutawapa ruhusa ya miaka miwili, baada ya hapo, kama Serikali ikiwa imeshajipanga, basi itakuwa wamefeli wao. Hilo jambo limewatisha *private sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili hiyo, naiomba sana Serikali yangu itazame uwezekano kwa sababu sasa hivi tunachoongelea hapa kwamba Bandari ya Dar es Salaam inazidi kujengwa na ninaamini muda siyo mrefu nchi jirani zote mizigo yao itakuwa ikitishishiwa hapa na hasa reli itakapoanza. Kwa hiyo, makontena yatakuwa ni mengi mno. Nafikiri Serikali haina haja ya kuwa na hofu na private sector, hawa ni

partners wetu, twende nao sambamba watatusaidia kama wanavyotusaidia sasa hivi. Sasa hivi mizigo tena imejaa katika *ICD* za private kwa sababu mizigo umeshakuwa mwingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bora Serikali ikatoa tamko kuhakikisha kwamba tunapanga mipango mizuri ya kwenda pamoja. Tositanguliane *private* na *Government Sector* ni *partners*, tutembee pamoja tutashinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natokea Zanzibar na siku zote napendelea sana Zanzibar na Bara tuwe ndugu wa kupendana na kushirikiana na tusiwe washindni. Ila tunapoingia katika uchumi, tunaona kuna ushindani mkubwa sana. Ushindani gani?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Turky, muda wako umekwisha. Kengele ya pili imeshagonga. Ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa na Mheshimiwa Prof. Norman Sigalla ajiandae.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Mpango huu wa Maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018, nillisimama hapa na nikaongea na Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango kumwambia kwamba mipango tunayoipanga kama Taifa na Bunge likaridhia na tukapitisha, ni vyema Serikali ikasikia yale ambayo tumeyashauri na kuyatendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina zaidi ya asilimia 70 ya wananchi ambao ni wakulima. Cha kushangaza, bajeti iliopita tulipata shilingi bilioni 100 iende kwenye kilimo ili iweze kusaidia shughuli mbalimbali ikiwemo utafiti, shughuli za kilimo

na mambo mbalimbali ya Wizara husika. Napenda kusikitika kwamba imetoka shilingi bilioni mbili peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kilimo ni uti wa mgongo, kwa sababu najua kauli hii haijatenguliwa toka tumepata uhuru wa Taifa hili; leo hii ambapo wakulima ni wengi huko vijiji na hususan wanawake tunaowawakilisha, kama hujapeleka pesa unakuwa hujawatendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili ufanikiwe katika viwanda, tunasema kwamba sasa hivi tunaenda kwenye viwanda vya kati kama Taifa. Usipowekeza kwenye kilimo, ambapo kilimo ndiyo kinatoa malighafi kwa viwanda hivi, unakuwa bado unafanya siasa kwenye mambo ya makini ya Taifa hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika asilimia 100 ya bajeti ambayo Bunge lako Tukufu lilipitisha, asilimia 98 ya gawio la fedha Mheshimiwa Dkt. Mpango haikupelekwa. Ninaomba tunapopanga vitu na Bunge lako likaridhia, Serikali na Wizara iweze kuachia fedha kwa ajili ya watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani ni wachache. Kwa mfano, nikichukua tu kwenye Wilaya ya Rungwe, wasimamizi wa kilimo wako wachache, hawawezi kufikia wakulima wote. Tuna Chuo cha Uyole Mbeya; Chuo kile kinasaidia utafiti. Huwezi kuwa na kilimo kisichokuwa na Utafiti. Tunataka kujua ni ng'ombe gani bora wenyе mbegu bora kwa ajili ya kilimo? Utawezaje kujua pasipo utafiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuo kile takribani miaka mitatu sasa hakijapelekewa fedha za maendeleo, unawezaje kuwasaidia wasomi hawa ambao wanasmamia raslimali za Taifa na ni washauri wa kundi kubwa la wakulima? Hawana fedha. Naomba Wizara yako Mheshimiwa Dkt. Mpango iliangalie suala hili kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia pembejeo. Tumekuwa na kilio kikubwa sana juu ya pembejeo. Leo hii kuna mbegu za aina mbalimbali na nyingine hazioti,

wakulima wanalamika. Tumesema Maafisa Ugani ambao wangetusaidia, leo hii ajira ya kuwaleta na kutuongozea kule vijiji ni hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujipange na bahati mbaya sana tumbaki na mwaka mmoja kama siyo miezi sita ili tuweze kumaliza mipango tuliyokuwa tumejiwekea. Naomba tafadhali tusimame kwa yale tunayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapozungumzia mbolea, kuna sehemu nyingi sana; sehemu za Mbarali na sehemu nyingine mbalimbali ambazo mimi nawakilisha, mbolea inaenda kwa kuchelewa. Wakati mwagine Mawakala mnaowapa wamekuwa hawawatendei haki wakulima jinsi ambavyo ilipaswa wafanye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niache hapo, niende kwenye suala la elimu. Taifa lolote likitaka kukandamiza watu wake linaweka elimu kuwa ni ya hali ya chini. Usipowekeza kwenye elimu, umeandaa jeshi la watu wajinga ambao watakuwa rahisi sana kupotea. Elimu kwa bajeti ya maendeleo iliyopita tuliweka shilingi bilioni 249. Sasa mnasema elimu bure, elimu isiyokuwa na malipo. Ni kweli ukitamka shilingi bilioni 200 kwa mwananchi wa kawaida anaona ni fedha nyingi, lakini ukienda kwa Mwalimu wa Shule ya Sekondari kwa mfano, anakwambia amepewa shilingi 200,000/= *Capitation*. Shilingi 200,000/= anunue chaki, alipe mlinzi na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tunahitaji kuwekeza zaidi. Tunaposema bure, nafikiri bora turudishe kama tulivyokuwa mwanzo, kwa sababu wananchi walijitolea wakatusaidia, watoto wote walikula chakula cha mchana. Ukitamka bure, kuna wazazi wengine wamegombaa kutoa michango kwa sababu Serikali imesema elimu ni bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni nyumba za walimu. Hiki ni kilio kikubwa sana. Walimu wengi wamepanga, wanakaa mbali na maeneo ya shule. Mishahara

haijaongezeka. Mheshimiwa Waziri, hebu tuwatazame walimu, maabara na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matundu ya vyoo ni tatizo hususani kwa watoto wa kike. Nazungumzia suala la bajeti. Tunapopitisha pesa, mashirika mengi, Wizara nyingi zinapata robo ya mapato inayostahili kupata. Sasa inakuwa kama vile; aidha mtuambie Serikali haina hela, lakini Serikali ya Awamu ya Tano inasema ina hela nyingi. Sasa bajeti ya shilingi bilioni 100, unapata shilingi bilioni mbili. Tunaomba maelekezo ya kina, kwa nini Bunge linapitisha halafu fedha inayotoka inakuwa kidogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni deni la Taifa. Mwaka 2018 nilizungumza juu ya deni la Taifa. Tumevuka sasa zaidi ya shilingi trilioni 50. Naomba, na nilisema mwaka 2018 pia, tusikope pesa. Tulete sheria humu Bungeni Serikali lisikope mpaka Bunge liwe limeridhia. Hii tabia ya kukopa pesa hatujui tunalipaje, deni la Taifa limekuwa kubwa na mnasema ni deni himilivu na mna lugha zetu za kisomi, lakini mwisho wa siku wanaolipa madeni haya ni watoto ambao leo hawajazaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Dkt. Mpango ni msomi, naomba asimamie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni mifugo na uvuvi ambayo ndiyo imeajiri sekta ya watu wengi. Kwenye uvuvi tulitoa shilingi bilioni nne ya maendeleo, tunarudi pale pale kwamba ni asilimia tatu ya fedha ndiyo iliyotoka. Tuna maziwa makubwa; Ziwa Nyasa, Ziwa Victori na Ziwa Tanganyika, kama Taifa tusipojipanga juu ya kutumia maziwa haya kuleta maendeleo kwa vijana wetu, nafikiri tutakuwa tunajidanganya. Unafanyaje maendeleo pasipo kuwawezesha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna maendeleo bila demokrasia. Ndugu zangu wameongea habari ya demokrasia. Leo hii tunapanga mipango lakini kwa njia ya figisu mmewaengua watendaji ambao ndio waleta

maendeleo. Mnaendeleaje? Tukae chini kama Taifa, tuache uwoga, tufaanye kazi kama *team*. Leo hii mmeumiza watu wengi nafsi zao na kujiandikisha wameona ni kitu cha kupoteza muda. Tunaomba demokrasia ichukue nafasi yake. Wengine wameumizwa na wengine wako ndani. Hivi ni watu gani wajinga wasioona? Kwa sababu mwisho wa siku, watu wanaishi na watu kule chini. Mmetupa watu ambao sisi hatujawachagua, tunapangaje maendeleo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, demokrasia ni tunda la haki. Pasipo haki, amani haiwepo. Naomba tusimame na hilo, tuwasimamie Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono Kambi Rasmi ya Upinzani. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Mpango nilitarajia hapo ungepiga meza, hoja yako imeungwa mkono na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Waheshimiwa Wabunge, hoja huwa ni moja tu ndiyo ambayo inajadiliwa hapa. Hayo mengine ni maoni, kwa hiyo huwezi kuunga mkono maoni.

Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kwenye hoja iliyopo mbele yetu ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Nampongeza sana, amewasilisha vizuri sana utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2018/2019 na Mapendekezo ya 2021. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwenye uso wa dunia wanadamu tuko zaidi ya bilioni saba; na kadri miaka inavyosogea kwenda mbele, wanadamu tutazidi kuongezeka sana. Wanafalsafa wanasema, vitu ambavyo

vitakuwa adimu sana miaka ijayo kwa kuanzia ni viwili; maji na chakula. Kwa hiyo, wanaendelea Wanafalsafa wanasema, mtu anayetaka kuwa tajiri miaka 20 ijayo, aingie kwenye kilimo leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuweka kipaumbele kwenye uchumi wa viwanda. Naipongeza sana. Naomba kwa kuwa Tanzania tuna ardhi kubwa sana na nzuri sana, tuna mito na mabonde, naomba tuupe kipaumbele sana uchumi wa viwanda kwenye kilimo. Tuige mfano wa kile kiwanda cha sukari ambacho kitajengwa hapo Morogoro. Tuige, tuwe na uchumi wa viwanda kupitia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vyuo vya kilimo vingi sana. Tuna Chuo Kikuu cha Kilimo *SUA* ambacho kina wataalam wabobezi wengi sana ambao wanaheshimika Afrika na dunia nzima. Afrika ya Kusini wanawapenda sana wataalam wanaostaa fu kutoka hapa *SUA*. Naomba Serikali iwatumie wataalam hawa. Tuwachukue, tuwafungie ndani, watupe *Blueprint* ya namna gani tutatumia ardhi yetu hii tuweze kupata mazao ya kilimo na kuweka viwanda vya kuchakata mazao yetu. Naiomba sana Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uwekezaji, Wizara ya Viwanda, Wizara ya Fedha tuwatumie sana hawa wataalam wetu wa Chuo Kikuu cha *SUA* waweze kutupa *Blueprint* ya namna ya kutumia ardhi na maji yetu tuliyonayo tuweze kujikomboa kwa viwanda kuanzia kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu tena ametupa neema ya bandari. Naipongeza sana Serikali, sasa hivi Serikali inaboresha Bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na Tanga. Bandari zetu hizi zinahudumia nchi karibu nane au tisa za Uganda, Rwanda, Burundi, Congo, Zambia, Zimbabwe, Malawi na zinginezo. Kwa hiyo, naomba uboreshaji huu tunaokwenda nao ulenge kushindana na bandari zingine ambazo ziko kwenye ukanda wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeona nchi jirani hapa juzi imeona Bandari ya Dar es Salaam inaboreshwa na mizigo

mingi inapitia Bandari ya Dar es Salaam wakapunguza ushuru kwenye mafuta ili tuweze kushindana. Kwa hiyo, naomba uboreshaji huu wa bandari uendane na kujipanga sawasawa kwa kushindana na nchi ambazo tuanshindana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona mwaka au miaka miwili iliyopita Bandari ya Dar es Salaam *TPA* waliweka ofisi yake kwenye nchi jirani ya Congo, jambo zuri sana. Hii inasaidia kufanya *marketing* ya shughuli zetu. Naomba hii iendelee kwa nchi nyininge zote ambazo tunazihudumia kibandari, tuweke ofisi zetu kule ili tuweze kuwashudumia, tuweze kushindana na wenzetu ambao tunashindana katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona vilevile kwenye mpango, Serikali inaendeleza ujenzi wa reli ya kati (*Standard Gauge*), inaendeleza kuboresha reli iliyopo ya *meter gauge* na vilevile ina mpango wa kuanza kujenga *Standard Gauge* ya kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara na kutoka Tanga kwenda Arusha mpaka Musoma, ni jambo zuri sana hilo. Hii *Standard Gauge* ya reli ya kati mwisho wa mwaka huu itakamilika kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro na inaanza Morogoro kuja Makutupora na itaendelea huko mpaka Tabora – Mwanza – Kigoma. Wenzetu nchi jirani ya Rwanda imeingia kwenye *bandwagon* hii, imeamua nayo kutafuta njia za kujenga kutoka Kigali kuja mpaka Isaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali sasa tui-*entice* Burundi nayo iingie kwenye mpango huu ili na wao wajenge kutoka Msongati kuja mpaka Uvinza halafu wajenge kutoka Msongati – Uvira kwenye nchi ya Congo. Hii reli ya *SGR* ili ilete faida kubwa kwa nchi yetu inahitaji kusafirisha mizigo zaidi ya tani milioni 20 kwa mwaka. Sasa tusipoitumia nchi ya Congo, itakuwa ni hasara. Kwa hiyo, naomba Serikali tuwa-*engage* Burundi nao waweze kutafuta fedha wajenge kutoka Msongati mpaka Uvinza na kutoka Msongati kwenda Uvira katika nchi ya Congo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuboresha hii *SGR* na *meter gauge*, ipo hii reli ya *TAZARA* ambayo yenywewe

ni *cape gauge*. Naomba ili tuweze kuitumia vizuri bandari yetu tuiboreshe reli hii ya *TAZARA* na katika kuiboresha hii inahitaji tu kuiwekea umeme ili treni ziende kwa kasi. Naomba tuiboreshe reli hii na vilevile Serikali iwe na mpango wa kujenga Bandari Kavu pale Inyara ambapo tumekuwa tunaiongelea mara kwa mara. Bandari kavu ikiwepo Inyara unaweza kujenga reli ya mchepuko kutoka pale Inyara ikaenda mpaka *Lake Nyasa* tukatumia vizuri meli ambazo Serikali imezinunua kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Malawi na Msumbiji. Kwa hiyo, naomba reli ya *TAZARA* na yenyele iwemo katika mpango huu wa kutumia reli zetu na uchumi wetu wa jiografia kuweza kujiletea maendeleo hapa Tanzania na kuwahudumia jirani zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa hayo machache, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Norman Sigalla atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu, Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala ajiandae.

MHE. PROF. NORMAN A. S. KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa Mpango mzuri waliouleta. Hawa ni rafiki zangu na wameleta Mpango mzuri sana, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nampongeza sana Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imemfanya apate sifa Afrika na dunia nzima ya kuekeleza na kusimamia mipango ya maendeleo yetu wenyele kwa fedha zetu wenyele. Mipango ya ujenzi wa bandari, viwanja vyatundege, maji Mtware na mipango mingi mizuri inayofanywa na Rais wetu, inampa sifa na heshimia duniani kote. Mungu ambariki sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kidogo maeneo machache. Unapoongelea kukuza Pato la Taifa ni vizuri

kuangalia katika sura mbili. Sura ya kwanza ni ile inayomgusa mtu mwenyewe mmoja mmoja, fedha inayomgusa mtu mmoja mmoja. Kwa hiyo, naomba sana kwenye eneo hili, benki zetu hizi za kilimo kama *Tanzania Investment Bank* tuweke riba ndogo sana kwa wakopaji wanaomaanisha kwenda kuwekeza kwenye kilimo angalau asilimia 10 lakini sio 17 au 19, haifai kwa sababu ni kilimo. Kwa hiyo, naomba sana wawekezaji wa kilimo wanapokwenda kukopa *Tanzania Investment Bank* wakope kwa asilimia angalau 10. Tukifanya hivyo basi tutaona maparachichi yakipandwa kwa wingi kule kwetu Makete, Rungwe na kila sehemu yatapandwa kwa wingi kwa sababu ukopaji utakuwa umerahisishwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni dhahabu yetu. Kwa sisi wachimbaji wadogo wa dhahabu ni vizuri sana *Geological Survey Institute* inayoongozwa na Profesa Mruma ikapewa fedha kwenda kufanya *explosion test* ili tuwe na uokaji wa dhahabu tunayojua kiwango chake. *Geological Survey Institute* inayoongozwa na Profesa Mruma ipewe fedha ili kwenda kufanya kazi hizo za kuhakiki kiwango cha dhahabu kilichopo kwenye ardhi kwa kila mchimbaji wa dhahabu mdogo mdogo. Tukifanya hivyo, tutasaidia wananchi walio wengi kupata dhahabu yao na fedha zao kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni upande wa elimu. Kwa mfano, shule za msingi Makete ni wastani wa walimu watatu kila shule sasa wanafunzi hao watasomaje? Naomba sana Wizara ipeleke walimu wa sekondari kwa mshahara wa sekondari wakafundishe shule za msingi, wale waliomaliza wapelekwe shule za msingi kwa mshahara wa sekondari. Wanachotaka wao ni fedha (mshahara), wapelekwe kwa mshahara wa sekondari lakini wafundishe shule za msingi. Shule za msingi *orientation* yake ni ndogo, figisu figisu na michanganuo ya kusema kwamba ufanye hivi, ufanye hivi, wanapewa elimu ya mwezi mmoja, wanahamasika halafu tunajenga shule zetu vizuri kwa sababu sasa hivi ni tatizo kubwa sana kwa shule za msingi za elimu wilayani Makete. Walimu watatu ndiyo wastani wa walimu kwa shule zangu, hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nihitimishe kwa kusema kwamba kama mipango yote hii tukiifanya, upande wa elimu tukawapeleka walimu wengi katika shule za msingi, upande wa kilimo tukawapa wakulima mikopo ya asilimia ndogo, asilimia 10 kwa mfano, Upande wa dhahabu tukapeleka fedha *Geological Survey* kwa Profesa Mruma akaweza kuhakika kiwango cha dhahabu kila sehemu basi tutakuwa tumesaidia kukuza uchumi wa nchi hii. Nafahamu kwamba *Geological Survey team* walikuwa wameshapewa fedha kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, sasa hivi hazipo lakini walikuwa wameshapewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho nzungumzie kuhusu ujenzi wa reli. Ujenzi wa reli ni jambo muhimu sana lakini naomba sana, reli ninayoikazia hapa ni ya Uvinza - Msongati, kwa sababu Msongati kuna chuma tani zaidi ya 3,000,000. Watazamaji wote wa reli hili wanafikiria kwamba ile reli itakuwa inameza chuma kile kwa kusomba chuma kile ili *tonnage* yetu iwe ya maana. *Tonnage* inayopelekwa Mwanza na Bakhresa ambaye ndiye mpelekaji mkubwa, akipeleka mara moja tu Uganda *tonnage* yake yote itakuwa imeisha, meli imeenda mara moja inakuwa imeisha lakini *tonnage* ambayo ni ya uhakika ni ya Msongati kwa sababu pale pana chuma na tayari tunao mkataba walioingia Mawaziri waliopita wa Burundi na Tanzania wa jinsi ya kushirikiana na DRC-Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu awabariki sana, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Diodurus Kamala, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim ajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia Mpango huu wa Taifa ambao ni muhimu sana. Kabla sijaanza napenda kutoa pole kwa wananchi wa Muheza kwa mafuriko ambayo wameyapata pamoja na Mkoa mzima wa

Tanga na kuwahakikishia kwamba Serikali inashughulikia matatizo yao na athari zote ili kurudi kwenye hali ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri Dkt. Mpango kwa kutuletea Mpango mzuri na ambao hata ukiuona unaona kweli uko kwenye mwelekeo mzuri. Mimi sitakwenda kwenye takwimu ambapo naona tunakwenda vizuri kwenye ukuzaji wa uchumi ambao kwa sasa tuko kwenye asilimia 7.2 na tunategemea 2020/2021 tufikie asilimia 10 na hata mfumuko wa bei uko vizuri tu kwenye asilimia 3. Kwa hiyo, nitajikita kwenye miradi ambayo imeanza na inaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo limezungumzwa kwa bidii sana na wachangiaji wengi lakini na mimi napenda kuongeza kwamba tunategemea kwenye Mpango huu ambao utakuja basi suala hilli lipewe umuhimu wa kipekee. Tunaamini kabisa kwamba kilimo ambacho Watanzania wengi wanafanya na kinatoa ajira karibu asilimia 65 tunategemea kwamba kitatuinua. Ni suala la kuweka mipango vizuri kuhakikisha kwamba suala la umwagiliaji linapewa kipaumbele, suala la uanzishwaji wa mabwawa linapewa kipaumbele na naamini kabisa kwamba tukiweka fedha nyingi kwenye kilimo basi tutaweza kuendelea kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na mambo hayo, kuna masuala mengine ambayo yako kwenye kilimo kwa mfano suala la chai. Nimefarijika sana hapa nilipomsikia Naibu Waziri asubuhi akisema kwamba wana mpango wa kuanzisha mnada hapa nchini na kuondokana na suala la mnada wa Mombasa. Suala hilo sisi Muheza limetuathiri sana kwa sababu kampuni kubwa ambayo inalima chai pale inapeleka chai yake kwenye mnada Mombasa na Mombasa wanunua na wanafanya *packaging* na kurudisha tena kuuza hapa hapa nchini. Suala hili kiuchumi kwakweli linatuathiri sana na ni vizuri liangaliwe kwa uhakika na umakini kabisa ili tuanzishe mnada wetu hapa tuondokane na kupeleka haya mambo Mombasa. Vivyo hivyo ni vizuri pia kuangalia mazao mengine na kuanzisha hasa mazao ya

viungo na mazao ya machungwa ili tuweze kuwa na bei elekezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kitengo cha *TMX* ambacho Kamati ya Bajeti ilitembelea, kitengo hiki ni kizuri sana ambapo kikitumika vizuri basi Serikali inaweza ikawa na mazao mengi elekezi kwa bidhaa nyingi sana. Naomba kabisa Mheshimiwa Waziri Kitengo hiki kitumike ipasavyo. Tulikwenda pale lakini tumeona kwamba kitengo hiki hakitumiki kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile limeongelewa suala la uvuvi, Bandari ya Uvuvi ni muhimu sana. Bandari hii ilianzishwa kwenye bajeti iliyopita na ilitengewa fedha, nakumbuka mwaka 2017 kuna fedha ambazo zilitengwa lakini haijapewa umuhimu wake. Tunaamini kabisa kwamba tukifungua Bandari ya Uvuvi basi tutakuwa tumefika mbali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *PPP* ambalo nimekuwa nikiliongelea kila mara na naamini kabisa juhudhi ambazo zinafanywa na Serikali sasa hivi, miradi hii mikubwa yote, *SGR*, ndege, umeme kwenye Bwawa la Nyerere naamini kabisa haya yangeoana na *PPP* sasa hivi hapa Tanzania tungkuwa tuna-*boom*. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba tumepitisha sheria hapa mwaka jana lakini mpaka sasa hivi hatujaona utekelezaji wake. Mheshimiwa Waziri tumekuwa tukisisitiza na naomba kusisitiza kwamba tangaza hiyo miradi ambayo tumeichagua. Tuliiona hapa miradi kumi ambayo bajeti iliyopita mlitusomea, tafadhalii itangazwe ili watu wajitokeze na kama hawatajitokeza tuone tuna tatizo gani lakini ni suala ambalo linatakiwa lipewe umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *ATCL* tumepeita, nashukuru ndege zimefika lakini cha msingi hapa ni kuhakikisha kwamba tunaboresha na tunaanzisha *route* nyingi zenyetija ili kuweza kuleta watalii na wawekezaji hpa nchi kwetu. Tunataka *Airport* ya Dar es Salaam iwe *hub*, tuhakikishe kwamba hii *Terminal III* ambayo ipo inatumika

kikamilifu. Sasa *Terminal III* bado ndege ziko chache lakini tunaamini kabisa kwamba wanaohusika watafanya juhudhi kuweza kushughulikia na kuhakikisha kwamba *Airport* yetu inakuwa changamfu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bandari ni muhimu sana. Uboreshaji wa bandari umekuwa mzuri, Bandari ya Dar es Salaam inaboreshwu vizuri, vilevile ya Tanga na Mtwara. Nimefarijika sana kwamba sasa hivi Bandari ya Tanga inachimbwa ili kuweza kupata kina kikubwa na naamini baada ya kazi hiyo kukamilika basi meli kubwa zitaweza kutua pale badala ya kwenda kutua Mombasa ambapo ilikuwa zinatua kule na baadaye zinaweza kuletwa hapa nchini. Kwa hiyo, suala hili ni la kupongezwa na tunaomba kabisa muendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa bajeti nilizungumzia kiwanda kimoja kikubwa sana ambacho kinatarajiwa kujengwa na Wachina kule Tanga Hengia. Kiwanda hiki cha saruji tunategemea kitakuwa kikubwa na kuleta ajira kati ya 4,000 mpaka 8,000. Kiwanda hiki tunategemea kitoe tani karibu milioni saba kwa mwaka lakini nilipopita mara ya mwisho Tanga sioni chochote ambacho kinafanyika naambiwa tu mazungumzo bado yanaendelea kuweza kuwaruhusu Wachina hawa waweze kuweka hiki kiwanda. Kiwanda hiki ni kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapopata wawekezaji kama hawa inabidi na sisi tuchangamke wasije wakatupokonya. Kwa hiyo, naamini kabisa wakati wa *winding up* na nashukuru Waziri wa Uwekezaji yupo hapa watupe msimamo kiwanda hiki kimefikia wapi. Hawa Wachina wanazunguka karibu miaka miwili hapa na vibali mara hiki mara kile, mara *incentives* sasa tunaomba tupate uhakika nini kinaendelea. Huyu ni mwekezaji mkubwa na tunaamini kwamba atakapoweka kiwanda kile basi mambo yatakuwa vizuri sana siyo kwa nchi hii tu bali hata kwa Mkoa wa Tanga mambo *yata-boom*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia, la mwisho ni suala la Soko la Hisa pale Dar es Salaam (*Dar es Salaan Stock Exchange*) tulifika pale lakini soko hili limeonekana limeduwa kidogo haliko *very active* na tunaona haliko *very active* kwa sababu watu wengi hawajaliorodhesha, nataka Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba Sheria ilishapitisha mashirika yote haya ya *communication* kwamba wajiandikishe kwenye soko la hisa, lakini mpaka sasa hivi ni *Vodacom* tu ambao wamejiandisha, sasa haya mashirika mengine ya simu kwa nini hayajajiajandikisha? Nataka Waziri akija hapa aeleze ili tuweze kujuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kwamba Soko la Hisa la Dar es Salam lilikuwa linachangamshwa sana na haya mashirika ya kijamii. Sasa baada ya kuunganisha haya mashirika ya kijamili, tangu uunganisho huo umefanyika, shirika hili letu la sasa hivi halijajiandika tena pale wala halijapeleka kununua hisa wala kuuza hisa. Tunaomba shirika hili ambalo limejumuisha mashirika yote ya kijamii basi lijijandikishe ili liweze kufanya lile soko la hisa liweze kuwa *very active*, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono mpango huu. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Diodorus Kamala atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Andrew John Chenge ajiandae.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naomba nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja iliyo mbele yetu. Naunga mkono hoja kwa sababu mbalimbali na nitazitaja chache. Hoja iliyo mbele yetu imeeleza vizuri katika *paragraph* ya kwanza kwamba tunatarajia kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Tatoo wa Miaka Mitano kwa sababu sasa tunamalizia huu tunaoutekeleza kwa sasa. Sasa kilichonivutia zaidi kuunga mkono hoja hii ni kwamba dhima inayotarajija katika mpango wa tatoo utakaoandaliiwa ambao inabidi sasa katika mapendekezo tunayoyapitisha leo tuanje sasa kuweka mambo ya msingi yatakayotusaidia

kuwa na mpango mzuri wa miaka mitano mingine; na dhima hiyo inasema kama ilivyobainishwa katika *paragraph* ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza mauzo nje na uwezo wa ushindani Kikanda na Kimataifa. Hili ni jambo jema na dhima hiyo itatusaidia kwa sababu tunapokamilisha huu mpango wa miaka mitano ambao tulijelekeza katika kujenga Tanzania ya viwanda, sasa tukielekea sasa kuongeza mpango wa tatu ukijikita kwenye kuongeza mauzo nje na uwezo wa ushindani Kikanda na Kimataifa itakuwa ni jambo jema. Kuna mambo ya msingi ambayo itabidi yawepo kwenye mpango wetu wa mapendekezo sjayaona na ningependa Mheshimiwa Waziri baadaye angalie ni jinsi gani anaweza akachukua mapendekezo hayo nitakayoyapendekeza kuwa sehemu ya mpango wetu tutakaoupokea na kuupitisha katika Bunge hilli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo ni muhimu sana kama tikitaka kujenga, kuongeza uwezo wa mauzo ya nje na kujenga ushindani lazima tuanze kwa kujenga ushindani wa ndani. Kwa nini ushindani wa ndani ni muhimu? Ni muhimu kwa sababu huwezi ukauza nje, huwezi ukajenga uwezo wa ushindani kama hujajenga uwezo mkubwa wa ushindani wa ndani, nitatumia mfano mmoja tu, mfano wa *wine*, uzalishaji wa *wine*; ukiangalia Sekta ya *Wine* kidunia kwa mfano ukiangalia Italy wao wanazalisha chupa za *wine* bilioni sita. Tanzania ukichukua kwa makadirio ya juu kabisa tunazalisha chupa za *wine* laki mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiwa unazalisha chupa za *wine* laki mbili, ukitaka kujenga uwezo wa ushindani kwamba tuwezeshe sasa *wine* yetu iweze kushindana hata ndani ya Afrika Mashariki, basi lazima tuanze kujenga ushindani wa ndani kwanza. Sasa kujenga ushindani wa ndani wa *wine* peke yake ukiangalia kwa mfano *wine* tulizonazo hapa Dodoma ukiangalia chupa sitataja aina ya *wine* na kampuni kwa sababu unaweza ukajikuta labda kampuni ukiitaja kwamba haifanyi vizuri inaweza isijisikie vizuri, kwa hiyo sitataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukiangalia hizi chupa utakuta kuna nyingine ina lebo ambayo ni *water proof* hapa hapa Dodoma, lakini utakuta *wine* nyingine ina lebo ambayo mvua ikinyesha hiyo lebo inaloana hapo hapo. Sasa namna hiyo, ukiangalia Sekta ya *Wine* tu kwa hapa Dodoma ni kwamba, ukisema unataka kusaidia *wine* iweze kushindana maana yake uangalie je unawezeshaje hii Sekta ya *Wine* kwa mfano, kuwawezesha kupata lebo ambazo zinaweza zikajenga ushindani, lakini kwa kuanzia lazima ujenge ushindani wa ndani wakishindana ndani ndiyo unaweza ukapata mtu wa kuweza kushindani nje kwenda kwenye soko la nje. Kwa hiyo huo ni mfano mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mwingine mdogo, kuhusu soko la kahawa la ndani na soko la pamba la ndani, lazima tujenge ushindani wa ndani, kwa mfano, kwenye kahawa ushindani wa ndani maana yake ni nini? Lazima tuangalie katika mpango huu tunaokuja nao tuangalie nini tunaweza tukafanya kujenga ushindani wa ndani wa ununuzi wa mazao yetu, kushindana ndani. Kwa mfano, mkulima wa kahawa yeye anapenda akiiza kahawa yake apate fedha yake pale pale. Natambua kuna hii dhana kwamba hela itapitia kwenye akaunti, watu wafungue akaunti, lakini mkulima anaangalia, yeye kama anazalisha kilo 10 au 20, unapomwambia utalipwa kuititia benki anakushangaa kwa sababu anaona gharama ya kufuatilia hiyo hela ni kubwa kuliko kile ambacho atakuwa anakifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna uwezekano wa kuweka mazingira ya ushindani ndani. Kwa hiyo ili tufanye hivyo mkulima huyu angependa awezeshwe aweze kuzalisha kwa tija, akiweza kuzalisha kwa tija utaweza kujenga ushindani. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba katika mapendekezo haya siaona vizuri inavyoweka mazingira ya kujenga ushindani wa ndani kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa nilizungumzie kwa haraka haraka ili kujenga ushindani tunahitaji mkulima kumwezesha kwa mfano, kupata viuatalifu. Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba Wizara

yake walitenga bilioni kumi nafahamu, lakini baada ya kutenga bilioni kumi *LC* ikafunguliwa pale *BOT*, Kampuni ya *TFC* ikapewa jukumu la kuagiza hiyo viuatilifu. Viuatilifu hivyo mpaka ninavyozungumza hivi sasa viko pale bandarini, bilioni kumi zimetoka lakini viuatilifu mpaka sasa hivi vinaozea bandarini na bilioni kumi zimetumika. Sasa mambo ya namna hiyo hayajengi ushindani, kwa nini? Kwa sababu hivyo viuatilifu vikitoka bandarini vimekuja havijatoka bandarini maana yake tunaendelea kumkwamishwa mkulima na hilo siyo lengo letu. Kwa hiyo Mheshimiwa labda atapokuwa anatoa ufanuzi nitaomba atueleze hizo bilioni kumi alizotoa na mpaka sasa hivyo viuatilifu viko pale bandarini vimelala pale ni jitihada zipi ambazo amezichukua za makusudi, fedha alitoa lakini viuatilifu vinaozea pale bandarini mambo ya namna hiyo hayatusaidii kujenga ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuzungumzia kwa ufupi kwenye kujenga ushindani kuhusu kilimo. Natambua pale tuna Mkulazi *one* na Mkulazi *two*, lakini ukisoma kwenye mapitio ya utekelezaji kwenye vitabu alivyotupa Mheshimiwa Waziri, ukisoma pale huoni kama kuna kitu kinachoendelea kwenye Mkulazi *one* na Mkulazi *two* kuhusu uzalishaji wa miwa. Ukisoma pale unaambiwa ekari 3,500 zimelimwa na ekari 750 zimepandwa. Sasa unajiuiliza kama umelima 3,500 umepanda 750 maana baada ya miezi sita na zile ulizolima zitakuwa zimeshaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi unapolima miwa halafu kiwanda hakijajengwa wala mitambo hajaja, baada ya miezi 12 miwa iko tayari kiwanda hakipo, maana yake hiyo miwa huwezi kuitumia tena. Ningeshauri kwa kweli Mheshimiwa Waziri umefika wakati Serikali ikajiondoa masuala ya kujenga viwanda badala yake iachie *Private Sector*. Hapa Tanzania tuna viwanda ambavyo vinafanya vizuri sana katika sukari sitaki kutaja ni kipi, lakini ni vizuri tungeiachia *Private Sector* ikafanya hivyo na hii Mifuko ya Hifadhi tuiachie iendelee na shughuli zake za mambo ya hifadhi, kwa sababu kwa kuendelea kuiambia Mifuko ya Hifadhi ifanye shughuli za uzalishaji wa miwa tunajenga mazingira ambayo hayana tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tunajenga Tanzania ya viwanda lazima tuweke mazingira mazuri ya kuwa na mikopo ya uhakika, natambua tunayo *TIB* lakini ukiangalia unakuta kwamba hii *Tanzania Investment Bank* uwezo wake ni mdogo, lakini tunayo mabenki mengi huko ya nje ya nchi ambayo yako tayari kuja Tanzania kuwekeza. Nadhani katika Mpango huu wa Maendeleo ujao tungeweka vivutio vya kuwezesha kuvutia *investment banks* kuja hapa Tanzania kuwekeza na kwa kufanya hivyo tutasaidia kuweka mazingira mazuri ya kuendelea kujenga Tanzania ya viwanda na pia kujipanga vizuri katika kutekeleza ule mpango wa tatu tutakaouanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika taarifa tuliyopewa ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo uliopita, utaona kwamba tulitenga bilioni 123.9 kwa ajili ya kilimo, lakini zillizotoka ni bilioni 56.5 ambazo ni sawasawa na asilimia 45.46. Pamoja na kutenga fedha kidogo na tukatoa kidogo, lakini kilimo ndicho kimechangia kwa asilimia kubwa kwenye pato la Taifa, kimechangia asilimia 28.6. Hii maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba tukitenga fedha nyingi zaidi kwenye kilimo tunaweza tukapata matokeo makubwa zaidi na uchumi wa nchi unaweza ukarufaika zaidi, hiyo ndiyo maana yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hivyo ndivyo ilivyo, nimejaribu kusoma kwenye mapendekezo ya Mwongozo, sioni popote ambapo mapendekezo yametolewa moja kwa moja kuagiza sekta mbalimbali, kuagiza Idara mbalimbali, kuagiza halmashauri zetu ili kutenga fedha za kutosha kuelekea kwenye kilimo, sioni ikijitokeza moja kwa moja. Kwa hiyo katika mpango wetu lingekuwa ni jambo jema kama jambo hilo lingeangaliwa na likajitokeza moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge ambayo ningependa niongelee kabla muda wangu haujawkwisha, tunayo *East Africa Master Railway Network* natambua kwamba tunazungumza hii *SGR* tunaendelea kujengwa ni jambo jema, natambua kwamba itatoka Isaka itaenda Kigari,

Iakini ningeshauri ikifika maeneo ya Runzewe au Bihamulo *i-branch* pale ielekee Kagera, ikifika Kagera ielekee Kampala, ikifika Kampala ielekee South Sudan. Tukifanya hivyo tutakuwa tumejenga uchumi nzuri kwa nchi yetu, pia tutawezesha hata Mkoa wa Kagera kuuandaa kushiriki katika uchumi shindani na kuongeza mauzo yetu ya nje ya nchi na tufikie hata viwanda vyetu mbalimbali vilivyo katika Mkoa wa Kagera viweze kuibuka na kufanya vizuri zaidi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mheshimiwa David Ernest Silinde, ajiandae.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyezekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* aliyetujalia uzima na afya njema ya kuweza kuchangia mapendekezo ya mpango huu tulionao leo mbele yetu. Nianze na mwenendo wa viashiria vyta umaskini kama ambavyo wenyewe waliotuletea Madaktari wetu mabingwa kama hivi vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyezekiti, walituambia kwamba, mapato na matumizi ya Kaya binafsi yamepungua na umaskini umepungua kutoka asilimia 9.7 hadi asilimia 8.0 kutoka mwaka 2011 – 2017. Kwa hivyo umaskini unaelekea umepungua kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, najiuliza umaskini huu uliopungua ni kwa kiasi gani wameangalia Watanzania hawa wanakula milo mingapi, mwaka 2011 walikuwa wanakula milo mingapi, 2012, 2013, 2014, 2015, 2016 na 2017 kama wanatembea kweli vijijini na kama wataalam hawawadanganyi umaskini hata kipindi hicho haujapungua na haujapungua kwa sababu bei za bidhaa zimekuwa zikipanda. Mwaka 2011 debe la mahindi lilikuwa Sh.5,000 mpaka 6,000; debe la mahindi mwaka 2017 lilikuwa Sh.12,000, sasa debe la mahindi limefika Sh.18,000 na kuendelea, wanasema umaskini umepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye unga wa sembe wenyewe, mwaka 2011 bei yake ilikuwa ni ndogo kwenye Sh.700, 800 hadi 1,000 leo 2019 bei ya unga wa sembe ni aibu imefika hivi sasa hadi Sh.1,500, umasikini umepungua! Jamani wataalam wetu madaktari hebu tuambieni ukweli, waliowaambia maneno haya, utaalam huu ni akina nani hata mtuambie hivi maana sisi wengine si Madaktari kama nyie, ni watu wa kawaida tu, ni Walimu tu wa shule za sekondari, lakini tunataka watuambie kupungua kwa umaskini huu na kupanda kwa bei; sukari, 2011 kama kweli kutoka asilimia 9.7 hadi asilimia 8.0 bei ya sukari mwaka 2011, 2012, 2013 na sasa waangalie 2017 sikuambii hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wanasesma kwamba mfumuko wa bei kwanza kutoka Januari 2019 hadi Septemba 2019 umetoka kwenye asilimia 2.3 hadi asilimia 3.2, wao wenyewe wamekiri kama kuna mfumuko wa bei, sijui madaktari wetu wanatuambia nini ningeomba niwashauri; kwamba bado hali ya umaskini nchini kwetu unaongezeka, wanaokula milo mitatu sasa wamepungua, kunakuwa na pasi ndefu, sasa wanasesma ni pasi ndefu, wanakunywa tu chai mchana wakitoka hapo usiku kidogo, basi wanalala. Hiyo ndio hali halisi ilivyo, tembeeni vijijini muone hiyo ndio hali ya umaskini ulivyo msidanganywe na wataalam wanaoleta kwenye makaratasi, twende kwenye uhalisia mtembee vijijini muone shughuli, ni kizaa zaa, mwaka huu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumza kwenye umaskini ule mwingine wa kipato, kwamba nao umaskini wa kipato umepungua hapa ni sawa na utaalam wao, lakini hasa waangalie hasa na hali ya umaskini inavyoongezeka kwenye Jiji la biashara tuje Dar es Salaam ambapo ndio linaitwa Jiji la biashara, ukienda pale Kariakoo maduka yamefungwa, mpango huu hauna jibu, hauna jibu, hautoi tija yoyote kuonesha mkakati gani ambapo wataboresha maisha ya wafanyabiashara katika Jiji la biashara la Dar es Salam, maduka pale Kariakoo yamefungwa, mpango huu hauoneshi jambo lolote, hakuna mpango hakuna mpangilio. Watuambie wana mpango gani au wana mpangilio gani

wa kufufua Jiji la kibashara la Dar es Salam. Shughuli ipo kweli! Watuambie madaktari wetu sisi ni wadogo sana kwao, wao wamesoma zaidi sisi ndiyo hivyo tena, watuambie madaktari hawasomeki, hawaeleweki waliwandikia sijui ni akina nani, shauri yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, kwenye ukurasa huu wa 43 wamezungumza habari ya utawala bora. Hasa utawala bora umo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Ibara ya 29 na 30 yaani majukumu yake. Sasa wamezungumzia moja kwenye utawala bora, mkakati wa Serikali kuhamia Dodoma, kwani utawala bora ni hilo tu? Katiba ya Jamhuri ya Muungano inasema ukienda kwenye Ibara ya 3(1) inazungumzia Tanzania ni nchi ya kidemokrasia yenye kufuata mfumo wa vyama vingi na ni nchi ya kijamaa. Ibara ya 5(1) inazungumzia haki ya kupiga kura yaani kuchagua na kuchaguliwa hawajagusa kitu hawa Madaktari, kule kwetu wanasema tawileni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida, katika hili la kupiga kura kuchagua na kuchaguliwa, tunaelekea kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa demokrasia imeminywa, demokrasia imepuuza, leo ni malalamiko kila kona, vyombo vya habari kila kona ndani na nje ya nchi kwamba hali ya demokrasia Tanzania imeminywa, wagombea wote wa Upinzani wameondolewa, matatizo yamekuwa ni makubwa na kwangu mimi kama mdau wa ulinzi na usalama ambaye napenda amani na utulivu wa kweli naona hicho ni kiashiria kibaya cha ulinzi na usalama lazima niseme kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani watu kufanya madudu yao waliyoyafanya ukaondoa wagombea wa Upinzani kwenye demokrasia ya mfumo wa vyama vingi, iko ndani ya Katiba, leo ukasema na sisi tunataka amani na utulivu. Jamani, Madaktari Serikali nzima inisikie, Mheshimiwa Jafo kasema kwamba watu waendelee kupeleka pingamizi hapa na pale, imeelezwa na Mheshimiwa Mbunge mmoja hapa, kwamba hao wanaopelekewa wamekimbia hawapo.

Huu ni mfumo wa vyama vingi, kama hamtaki mfumo wa vyama vingi, futeni vyama vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu najiuliza mambo ambayo kila siku ninyi mko kwenye redio masaa 24, mmefanya hiki, mmefanya hiki, anakuja Polepole anasema, mko peke yenu siku saba tu ambazo ni kampeni, waachseni watu wachague na kuchaguliwa, raha ya kushinda ni kushindana, msiende peke yenu muone mambo mengi mliyokwishafanya mnatutangazia wananchi watapima, lakini tunakwenda kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa, ni aibu na fedheha kubwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali Mheshimiwa Jafo katoa tamko lake lakini pamoja na hayo hebu jamani angallieni hilli, warudisheni hawa wagombea nchi hili twende kwenye amani na utulivu wa kweli lakini kilio kila kona hawa ni binadamu. Kumbe viashiria hivi vinavyofanywa najiuliza je, Serikali ya kijiji ndio inataka amani itoweke? Ni Serikali za kwenye kata au za kwenye wilaya au kuna baraza gani najiuliza mimi mwenyewe binafsi kwa sababu unapowanyima fursa watu kuchagua na kuchaguliwa hili ni tatizo ni kiashiria kibaya kwenye amani na utulivu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri wanaohusika na vyombo vyा ulinzi na usalama waliomo ndani na nje ya humu ndani niwaombe sana suala hili si la kulifumbia macho ni lazima wahakishe kwamba watoe tamko la wagombea hawa wa upinzani kurejesha kugombea, nchi hili twenda vizuri tuko katika mfumo wa vyama vingi. Ama kama sikio la kufa halisikii dawa shauri yenu mimi nishasema na kwa sababu lugha yangu hii naizungumza mnaifahamu vizuri ni Kiswahili cha kawaida. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema haya nirudie tena kwa sababu mimi binafsi ni mdau mkubwa wa ulinzi na usalama, ukataka usitake huwezi kuzungumza masuala ya ulinzi na usalama humu ndani Bungeni usimtaje Masoud. Kwa hiyo, lazima niseme kwamba dawa mfumo wa

vyama vingi tuangalie viashiria ambavyo vinaweza kuleta tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie mzungumzaji huku niko peke yangu dakika zangu mlizonipa hizo nimeongea na wenzangu kwamba niendelee na shughuli, nashukuru haya sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie mpango huu pia hautojibu hamna chochote mtazungumzia habari ya jibu la milioni 50 kila kijiji umaskini utapungua wapi. Serikali iliahidi kwamba mtatoa bilioni 50 kwa kila kijiji hamna kitu, mpango hauna jibu lolote kama kweli mnataka kukuza uchumi na kupunguza umaskini mpango hauna jibu lolote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mnaposema milioni 50 kwa kila kijiji mwaka wanne huu si mngetuacha tu tukaenda kwenye vijiji tukawaambia wananchi hiyo ndio hali kumbe mnaogopa kweli mfumo wa vyama vingi, shughuli ipo mwaka huu, hakuna jibu milioni 50 kila kijiji imekufa hivi hivi waziwazi. Madaktari mngekuja mtuambie milioni 50 kila kijiji uko wapi mpango bado mnao? Mpango huu hauonyeshi mkakati wa kuboresha maendeleo ya wafanyakazi, mishahara ya wafanyakazi *annual increment* nyongeza hata ya kila mwaka nayo ni tatizo shagalabagala mwaka! Mtuambie madaktari nini mmekusudia mnataka kuipeleka wapi Tanzania? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri bahari kuu humu hakuna mpangilio maalum *deep sea fishing* ambao duniani kote tuna bahari ya kutosha, *deep sea fishing* humu mtueleze ukubwa wake mna maelezo kidogo tu. Uvuvi wa bahari kuu uko wapi watu wanakuja hapa na meli zao wanachukua samaki wanakwenda kuuza, sisi katika hali kama hiyo tuangalie mkakati wa kuboresha uvuvi wa bahari kuu, lakini Mheshimiwa Mpango huu haoneshi madaktari mtuambie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala zima la kilimo mmegusia sehemu ndogo ya uhitaji wa masoko lakini katika mwaka uliopita wakulima wa mbaazi walathirika sana hadi leo wakulima wa mbaazi wana wasiwasi kupata soko

la uhakika kwa sababu walikuwa wanalamika wakauza kilo ya mbaazi shilingi 200 mpaka 300 mtuambie mkakati wa Serikali wa kuboresha soko la uhakika la wakulima wa mbaazi uko wapi, mpango unaonesha mtuambie na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anaangalia kwelikweli kumekucha kweli katika mkakati huu mimi nafikiri mtupe majibu mazuri. Kwa sisi wengine mwezi huu unaitwa mwezi wa mfungo sita mwezi ambao *Mtume Muhammad Sallallahu alayhi wa sallam* tupo wataratibu wapole tukimaliza hii tena uko mbele lakini tunataka Serikali itoe majibu sahihi ituambie mkakati madhubuti na endelevu wa kuboresha masoko ya uhakika ya mazao ya kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache kwa sababu nilibamizwa na mambo mengine hapa niseme hayo yanatosha lakini nisisitize suala zima la utawala bora lifanyiwe kazi isiwe bora utawala. Kama tunataka utawala bora twende kwenye utawala bora kama unataka bora utawala endeleeni kwa sababu mna nguvu. Narudia tena kusema kama kuna utawala bora kama mlivyoandika ukurasa 43 twendeni kwenye utawala bora tuwe na chaguzi ya mfumo wa vyama vingi watu wachague wachaguliwe, kama mnataka bora utawala endeleeni kwa sababu mna nguvu. Lakini hii ina athari kubwa utawala bora nyie mnataka bora utawala, tatizo ni nini kuna hofu ya nini nyie ni watu wazima humu ndani katika Bunge hili upande huu wa upinzani huu mimi ndio mtu mzima wao na ukiona mtu mzima analia kuna jambo. Kama mnataka kusikia sikieni kama hamsikii shauri yenu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asanteni sana nashukuru (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge tukumbuke tu kwamba huu mpango ni sehemu ya ule mpango wa miaka mitano ambao Bunge hili lilishaupitisha likajadili wakatoa mawazo. Kwa hiyo, ni vizuri tujikite pale ili tusifikiri kwamba huu mpango kwa namna yoyote ile unaweza kutoka kwenye kile ambacho Bunge tulishasema

kule nyuma. Kwa hiyo, ni vizuri tuwe nayo yote miwili tuwe tunatazama ni mambo gani yameshakwisha na yepi tunaona kwamba ni muhimu yaendelee kuwepo humo ndio kazi yetu.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Andrew John Chenge atafatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Dkt. Lemomo Kiruswa ajiandae

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia kidogo kuhusiana na mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2020/2021 ambaao ndio utakuwa umefika ukomo wa kipindi cha miaka mitano kwa huu mpango wa pili ambaao tumeanza kuutekeleza tangu 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake kwa kutuletea mapendekezo haya na wewe umesema sasa hivi vizuri sana huu ni mwendelezo katika utekelezaji wa mpango wa pili wa maendeleo ya Taifa ambaao tumeingia sasa huu mwaka wa nne. Ni kweli lazima *tu-take stock* na ndio maana Serikali inakuja hapa na mapendekezo haya. Sisi kama wadau kama sehemu ya uongozi wa Taifa hili ambaao tumeaminiwa na watanzania wema katika nyumba yao hii tuweze kuona namna ya kuboresha, kuishauri Serikali ndio kazi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliotangulia katika kuchangia tuisaidie Serikali maana nikilalamika nikishamaliza kulalamika kwani itakuwa imesaidia? Saidia kuonyesha njia, mimi nadhani tukienda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa haya makubwa inayoyafanya sasa unaweza usione muunganiko wa moja kwa moja kwa maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja kwa Bwawa la Nyerere la kufua umeme. *SGR* inayojengwa hata ndege hizi zinazonunuliwa lakini nawaambieni miradi hii itakapokamilika

suala tunalosema la tija, ufanisi kwenye viwanda vyetu, umeme ndio kichocheo kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia reli hii ambayo nitaisemea sasa hivi reli ya kati ndio kiini ni injini ya ukuaji wa uchumi wa mataifa yote na ndege hizi utalii watanzania Mwenyezi Mungu ametujalia kitu ambacho lazima tuendelee kukinufaika, tunufaike nacho sasa na kesho na kesho kutwa. Pesa hiyo ndio inayoenda kusaidia kuboresha huduma za jamii kama afya, maji yote haya ambayo tunayaongelea kwa faida ya watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuchukua muda mwingu kwa hilo lakini sisi kazi yetu tuishauri Serikali katika maeneo ambayo tunadhani tunaweza tukafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la kilimo, limesemwa vizuri sana kwenye taarifa ya waziri aliyowasilisha; niseme pia ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti tumeyasema sana lakini nashukuru taarifa ya Kamati ya Bajeti. Waheshimiwa Wabunge isomeni lakini tumeongea sana na Serikali kwenye kamati kusaidia haya mawazo na sisi tunabaliana na wengi mnaosema kwenye kilimo, kwenye uvuvi, kwenye mifugo huko tukiweza kuboresha hayo maana ndio sekta ambazo ukinyanya hizo ndio zinaunganisha na zinachochea ukuaji wa sekta nyininge ifanyiwe vizuri kwenye kilimo nasema kilimo cha Tanzania kama tutafanikiwa kikuwe kwa kasi asilimia sita na tukawa *persisted* kwa kipindi kirefu miaka 10, 20 utaona mchango wake kwa Pato la Taifa tulikuwa kubwa sana na ndio itabeba wananchi wengi kuwaondoa katika lindi la umasikini, mipango ndio hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimia naomba sana katika vipaumbele vyta mwaka kesho tuweke *intervention* kubwa tupeleke kwenye kilimo pia kwenye mifugo, kwenye uvuvi ionekane kwenye bajeti yetu kwenye sekta hizo kupitia mpango huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa Serikali maana tunamaliza mpango huu wa pili mwakani ndio tutakuwa

Bunge litakuwa karibu linakaribia kuvunjwa lakini Tanania ipo itaendelea kuwepo wananchi wa Tanzania watakuwepo na Serikali itaendelea kuwepo na Bunge la Tanzania litaendelea kuwepo, kwa hiyo watakaorejea tunataka tuje tuone angalau ifanyike tathimini ya kipindi tuone mpango wa pili wa miaka mitano ambao tulikuwa tumemaliza kuutekeleza kipindi hicho tunapoenda kwenye mpango wa tatu wa maendeleo ya Taifa letu tuone ni nini ambacho tumefanikiwa sana, nini maeneo gani hatukufanikiwa sana, nini kifanyike ili tunapoenda kwenye mpango huo wa tatu na wa mwisho tuwe kweli *confidence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali hata katika hatua hii kwa sababu kupanga mwalimu alikuwa anatukumbusha kupanga ni kuchagua tungkuwa na rasilimali nyingi ambayo unaweza kutekeleza yote haya kwa wakati mmoja tungeweza kufanya hivyo lakini hatuna lazima kile kidogo ambacho tumekubaliana kukifanya tukifanye kwa ufanisi na ndio maana mimi nasema naelewa baadhi yetu tungependa tuone mambo tunasema haya ni mengi mno tuliyoyabeba, lakini utafanyaje Tanzania hii nchi ni kubwa tuna wananchi milioni karibu 53,000,000 lazima uende hivyo unaumia hapa kidogo lakini huko mbele wengine panaenda vizri, ukifanya *stock* nzima unasema Tanzania inasonga mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa reli *concern* yangu iko kwenye taarifa ya bajeti kama ripoti ya taarifa ya bajeti Kamati ya Bajeti tunafanya vizuri tumetumia pesa ya ndani jasho la Watanzania kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro heshima kubwa kwa nchi hii heshima ehee! Tujivunie wananchi pesa ya ndani tumekopa kutoka Morogoro kuja Makutupora ndio lakini ni mkopo wetu wa Watanzania. Na tunajiandaa sasa tutafute pesa nyingine kutoka Makutupora kwenda Tabora, kwenda Isaka, kwenda Mwanza na baadae kwenda Tabora, kwenda Kigoma, Uvinza Msongati tutatoka Kaliuwa, Mpanda tuende mpaka Kalema, ndio mipango yetu hii kalema kwenye *Lake Tanganyika* tuna mipango tunaiona Tanzania na majirani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini *concern* yetu na ndio imo kwenye taarifa ni kwamba tunachukua mikopo hii bahati mbaya ni ya muda mfupi, masharti yake ingependeza kama tungeshambulia reli hii, ujenzi wa reli hii kwa wakati mmoja kwa sababu tunajua pesa hizi kwa kupata mkopo wa muda mrefu itakuwa ni ngumu sana lakini tukiweza vipande hivi tukavishambulia kwa wakati mmoja tutakuwa tumekamilisha ujenzi wa reli hii na matawi yake muhimu haraka sana na ndio tutaona faida, ndio ushauri wetu huo kwa Serikali. Naelewa misaada imepungua sana, mikopo ya masharti nafuu imepungua sana, eneo ambalo tunaweza tukapiga hodi na nadhani tumekaa vizuri ni kwenye *export credits* iwe ni ya Waingereza ya Wafaransa ya Wajerumanii angalau ukipata mkopo ule mpaka miaka 21 *window* hiyo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri naiomba Serikali tuangalie *option* hizo tutafanya vizuri na kwenye reli nasema reli hii tuikamilishe naomba sana Serikali reli hii ya Kati tuikamilishe na ningependa sana ndoto aliyonayo Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli aikamilishe reli hii wakati wa uongozi wake heshima kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tuna miradi mikubwa kwanza nipongeze kazi nzuri ya Dar es Salaam Bandari Port Gati moja mpaka namba 7 ile kazi inaenda vizuri, tunapanua lango pale kuingilia kazi nzuri. Mtwara inaenda vizuri sana *is the natural Port* Mtwara *is the deep sea Port* ehee nashukuru sana Magati yale yanaongezeka. Tanga ya sasa na sawa tunawekeza kwenda toka mita *depth* ya mita 4 kwenda 15 lakini Mwambani ndio yenyewe Tanga Mwambani ndio kwenyewe eehe tuangalie huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini narudia kama kwa Bagamoyo tumeona muwekezaji huyo hafai haimaanishi kwamba mradi wa Bandari ya Bagamoyo haufai hapana, tutafute muwekezaji mwingine ambaye ataendana na matakwa yetu ili bandari ya Bagamoyo ijengwe ndio matumaini ya Taifa hili Dar es Salaam pamoja na maboresho yanayoendelea hatutawenza kupata meli zile kubwa za tani

kuanzia 50,600 yale yanaitwa *ports kwanama* yale hayawezi kuingia kwenye lango la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba Liganga na Mchuchuma tukamilishe mazungumzo kama imeshindikana na muwekezaji huyo tutafute mwingine lakini hii taarifa hii kila mwaka tunarudi nayo mpaka tunataka kumaliza miaka mitano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu ndio huo lakini mimi naipongeza sana Serikali Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yako hongereni sana tuwaunge mkono najua changamoto ni mapato tuwasaide ni maeneo yapi tunadhani tunaweza tukaongeza *to argument* mapato ya Serikali ya ndani hasa mapato ya ndani ya kodi ya siyo ya kodi mnaona tangu tuanze matumizi ya ufanisi wa electroniki, mapato yanaongezeka ya kodi lakini pia na yasiyo ya kodi. Nadhani likisimamiwa vizuri tutaweza kupanda kutoka kwenye triliioni 1.2 ambaao tumegota kidogo sasa na tukaweza kuongeza mapato yetu. Tuangalie maeneo mengine ameyasema vizuri Mheshimiwa Masoud eeh! Bahari ya Hindi tutumie, *blue economy* ya Tanzania hiyo hiyo tuichukue vizuri tufanye mambo makubwa, inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umenipa heshima umenivumilia mchango wangu ni huo tuhimize tufanye maamuzi ya haraka katika maeneo ya vipaumbele ambayo tumejiwekea sisi wenyewe nakushukuru sana ubarikiwe sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Masoud alikuwa anasikiliza kwa makini sana kwa hiyo, nikaona ngoja umalize Mheshimiwa Chenge. Mheshimiwa David Ernest Silinde tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Lemomo Kiluswa.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana ambaye ndio Mwenyekiti wetu wa kikao kwa siku ya leo, kunipa fursa kujadili mapendekezo ya mpango wa maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza michango mingi na mingi ni mizuri. Kwa sababu mpango wetu huu ni wa mwisho, mimi nitajielekeza kwenye Kitabu cha Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano ambacho Bunge lako Tukufu lilipitisha na miradi ambayo mpaka sasa haijatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa 2016 tulipokuwa tunajadili kitabu hiki kuna miradi ya kielelezo ambayo sisi kama Taifa tulipanga itekelezwe. Katika miradi ya kielelezo, ipo ambayo tumefanikiwa kwa kiwango fulani na ipo ambayo tumeiondoa kabisa na Serikali inashindwa kuleta majibu ya msingi kulileza Bunge lako Tukufu kwa nini tumeshindwa kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi Na.1, ukisoma ukurasa wa 83, miradi ya kielelezo inayohusiana na Kanda za Maendeleo, kuna ujenzi wa Bandari Mpya ya Bagamoyo, amezungumza Mheshimiwa Mtemi Chenge hapa. Ni kwamba bandari hii, lile eneo lote ilikuwa lina uwezo wa kuongeza ajira zile zisizo rasmi na kufikia 100,000. Sasa hebu fikiria leo katika nchi ambayo wananchi wanalamika hakuna ajira, hii bandari ambayo ilipaswa iwe tayari imetekelawa, tangu mpango wa pili tumeanza kuuandika, mpaka leo hakuna majibu ya kutosha, Serikali inashindwa kutueleza ni kwa nini jambo hili linashindwa kutekelezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni uanzishaji wa Kituo cha Biashara na Huduma Kurasini. Hii ipo kwenye Mpango ukurasa huo huo wa 83(e). Jambo hili mpaka leo halipo popote na Serikali imelipa fidia lile eneo, limekaa pale halina kazi yoyote. Maana yake tulipitisha Mpango ambao tumeshindwa kuutekeleza na leo Serikali hajatoa majibu. Mradi huu vilevile ulikuwa unaongeza ajira ambazo zinafikia walau zile zisizo za moja kwa moja pale, zaidi ya 100,000 zingeweza kupatikana kwa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa Mji wa Kilimo Mkulazi. Tuliandika kwenye Mpango huu wa Miaka Mitano na mpaka leo tunakwenda kwenye mpango wetu wa mwisho, huwezi kuona Serikali inakuja kutoa maelezo, huo

mradi wetu wa ujenzi wa Mji wa Kilimo wa Mkulazi mpaka sasa tumefikia wapi na matokeo yake ni nini kulingana na mpango tulivyoupitisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine tulioipitisha kwenye Mpango ambao mpaka sasa hivi haujatekelezwa ni uanzishaji wa viwanda vya vipuri na kuunda magari. Hii ipo kwenye kitabu hiki cha Mpango wetu ukurasa wa 84. Mpaka leo huo mradi haujatekelezwa, hakuna viwanda vya vipuri vya kutengeneza magari hapa ambavyo vimeanzishwa; wala viwanda vya kuunda magari ambayo tulikuwa tunahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya uchimbaji wa makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma, hii imekuwa *story*. Mimi tangu nasoma sekondari miaka ya 1990 mpaka nimeingia Bungeni, sasa nafanana na akina Mheshimiwa Mkuchika sasa hivi, bado *story* ni ile ile ya Liganga na Mchuchuma. Mheshimiwa Mtemi Chenge amezungumza, tunashindwa kuingia mikataba ambayo inaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliweka malengo sisi kama Taifa letu; malengo na viashiria kwa ajili ya utulivu wa kufanya biashara katika Taifa letu. Kwa mfano, mwaka 2015/2016 urahisi wa kufanya biashara Tanzania ilikuwa katika nafasi ya 139 kati ya nchi 189 na malengo tuliyoweuka katika mpango tulisema inapofika mwaka 2020/2021 tuwe katika nafasi ya 100. Yapo kwenye vitabu hivi, lakini unapozungumzia leo, nchi yetu iko nafasi ya 144. Lengo lilikuwa nafasi ya 100, lakini mpaka sasa tuko wa 144 kati ya nchi 190. Ni malengo tuliyojiwekea ambayo mpaka leo katika huu Mpango hayajateklezwa. Sasa unaweza...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):
Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde kuna Taarifa.

Mheshimiwa Angella Kairuki.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo anapotosha. Ukiangalia kwenye nafasi ambayo Tanzania kwa sasa tumeishikilia kwa ripoti iliyotoka mwezi wa Kumi, tumetoka nafasi ya 144 kwenda nafasi ya 141. Nami nilitarajia angeweza kupongeza kwa sababu, ukiangalia siyo nchi nydingi ambazo zimeweza kupata mafanikio hayo; na hii ni hatua katika kuelekea katika maboresho makubwa kwa ajili ya kuweza kuboresha nafasi ya Tanzania katika tathmini hii ya Benki ya Dunia. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde, unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa hiyo Taarifa. Labda nimweleze tu. Ndiyo maana nimezungumzia Mpango. Mpango wetu tulisema tunavyozungumza leo, tuwe nafasi ya 100. Uko nafasi ya 141. Au unataka tukupongeze wakati Mpango huu tumeandika sisi wenyewe? *Issue* ni malengo. Tumesema mwisho wa mwaka utafanya mtihani utapata *marks* 90, umepata 54, unataka upongezwe. Wewe uko ume-*underscore*. Sijui kama umenielewa! (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ndiyo upungufu wa kutokukubaliana na hali halisi. Mwaka 2010 Tanzania ndiyo ilikuwa katika nafasi bora kabisa ambayo yumewahi kufikia. Mwaka 2010 tulikuwa nafasi ya 125 ya urahisi wa kufanya biashara katika nchi 189. Kwa hiyo, tumerudi nyuma, hatuwezi kujipongeza katika vitu ambavyo hatujafanya vizuri sana. Kwa hiyo, nasi haya tumeyatoa ili Serikali iweze kuyafanyia kazi, sio ku-*counter attack* tu kila kitu, hamwezi kufanikiwa katika hicho kitu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mapendeleko yangu ya Mpango, nini ambacho Serikali sasa inapaswa kukifanya ili kuhakikisha baadhi ya mambo wanaweza kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo namba moja kama Taifa ambalo tunapaswa sana kuliwekea mkazo ni kutumia nafasi yetu ya kijigrafia kuhakikisha tunatumia huu ukanda wetu, kwa maana sisi kama Tanzania tunazungukwa na nchi zaidi ya nane. Hizi nchi ndiyo tunapaswa kuzifanya biashara kuliko hizi porojo ambazo tumekuwa tukifanya hivi sasa. Hiyo ndiyo namba moja. Nilitegemea kwenye Mpango, Serikali ingekuja na Mpango huu unaokuja watueleze ni namna gani tutafanya biashara na nchi zote zinazotuzunguka kwa kutumia Tanzania kama sehemu ambayo ndiyo itakuwa kituo kikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa nasoma ripoti ya wiki iliyopita, Kenya peke yake kwa kutumia bandari yao tu wamesema wamepunguza asilimia 50 ya ushuru kwa wafanyabiashara wote watakaotumia Bandari ya Mombasa. Hao Kenya, yaani wameshaweka *incentives* ya kuhakikisha wanatunyang'anya hata hizi biashara tunazofanya na nchi nyingine. Sasa Serikali na Mheshimiwa Dkt. Mpango hapa, nataka aieleze nchi kwamba nasi tunafanya nini kuvutia hizi nchi wanachama zinazotuzunguka kuhakikisha tunapata faida ya kuwa katika nafasi bora kabisa katika...

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde kuna Taarifa.
Mheshimiwa *Eng.* Isack Kamwelwe.

TAARIFA

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa Taarifa mzungumzaji kuhusiana na uwongo ambao umetembea kwamba Bandari ya Mombasa imepunguza ushuru kwa asilimia 50. Jambo hilo halipo, illikuwa ni uwongo, uchochezi tu wa wafanyabiashara. Bei iko pale pale kule Mombasa. Dar es Salaam ndiyo tunaendelea kupunguza bei ili tuwe na meli nyingi na ndiyo maana sasa hivi zinaanza kuingia meli

kubwa za mita mpaka 300 zinazobeba ma-*container* mpaka 5,000. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silinde unaipokea Taarifa hiyo?

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri huwa tukizungumza tunapowapa *data* huwa wanaelewa na wanafuatilia na huwa hawayatolei majibu mpaka tuwakumbushe humu ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kuhakikisha tunatumia nafasi, *geographical position advantage* tuliyonayo kuhakikisha tunafanya kuwa *incentives* ya ku-*promote* biashara kushirikiana na nchi nydingine. Hiyo ndiyo hoja yangu kubwa. Hata kama Mheshimiwa Waziri hapa anasema ni *speculation*, lakini hiyo halondoi mantiki ya kwa nini watu wamepeleka hizo *speculations* Kenya badala ya kuzileta hapa Tanzania, kwamba kwa kufanya biashara hapa Tanzania, maana yake unaweza ukapata hizo *benefits* na kuondoa hiyo migogoro inayoendelea? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tuwe wa kweli. Nchi yetu kwa sasa bado tunashindwa kuwekeza katika mifumo ya *PPP*. Hii tumeieleza muda mrefu sana, nami nitaaeleza kwa kifupi sana. Mheshimiwa Mtemi hapa amejaribu kuzungumzia, lakini sisi nchi yetu tukiruhusu *PPP* ninaamini mambo mengi makubwa yanaweza kufanikiwa kuliko tunavyofanya sasa hivi. Nami ninachokitaka hapa, *PPP* ielekezwe kwenye miundombinu na wala siyo kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi unapoleta sekta binafsi ikashirikiana na Serikali, ikajenga barabara kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro, *Dar Express Way*, muundombinu ukakaa pale, ile sifa inakwenda kwa Serikali, haiendi kwenye sekta binafsi kwa kujenga ile barabara. Ukichukua hela hizo hizo, kwa mfano reli tumeigawanya maeneo mengi, fedha hizi hizi ukachukua *PPP* ukajenga reli, faida ya ile reli inakwenda kwa wananchi na wala siyo kwa ile sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi sana, ukiangalia wenzetu wa Malaysia walipokuwa wanaanza huu mfumo wa *PPP*, katika *phase* ya kwanza waliingia mikataba ya hovyo ambavyo na wao wenyewe wanakiri, lakini pamoja na kwamba walifanya mikataba ya hovyo wakasema *phase* ya pili walirekebisha *phase* ya kwanza. Sasa sisi hapa kama uling'atwa na nyoka zamani, unasema sasa hiyo njia sisi hatutaki kuelekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hoja yangu kwa Serikali katika huu Mpango, tujikite kuwekeza kwenye *PPP* katika miradi ya miundombinu. Ukijenga reli hapa hakuna mwekezaji ataondokanayo, mtu akijenga barabara hapa hata akiingia hasara hakuna mtu ataondokanayo, lakini kitu pekee ambacho nisingekubalianananacho, *PPP* isifanyike kwenye masuala ya *service only*. Yaani kwenye upande wa huduma, nchi ijitegemee yenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa sababu sasa hivi tuna ndege, tunataka tuone sasa katika Mpango wetu hapa, *service industry* tunaiwekeza kwa kiwango gani katika nchi yetu? Tufanye kama wanavyofanya wenzetu wa Rwanda pale, yaani wana *Conference Tourism*, wana *Business Tourism*. Sasa hivi dunia nzima iwe ni vikao vya *FIFA*, iwe ni vikao vya Mabunge ya Afrika, iwe ni vikao vya Mabunge ya Dunia, wote wanakwenda Rwanda kuwekeza kwa sababu wanaona kanchi kao ni kadogo, hawana rasilimali za kutosha kwa hiyo, wana-*promote* watu kwenda Rwanda kufanya mikutano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, shirika lao la ndege linapata faida, lakini na nchi vilevile inapata mapato kwa sababu, watu wengi wanakwenda pale. Sasa hayo ndio mambo ambayo tulitegemea Mpango wetu uwekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo tu cha mwisho, tumenunua *Dreamliner* mbili ambazo nafikiri ninyi wenyewe mmeziona. Tusingependa kuziona zinakaa pale, tunataka tuone kwenye Mpango hapa *route* za Kimataifa. *Route* kubwa ziwe zinaainisha kama ambavyo wale wote wanaopanda ndege kwenda Kimataifa ukisoma vile vitabu

vyao vinakuonesha *destination* ambazo wanatarajia kwenda, *destination* za sasa. Sasa na haya tuyaone hapa ili walau hizi ndege zisiwe hasara kwa Taifa, badala yake zilete faida. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Lemomo Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka wa 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia kwenye Mpango na nimetazama baadhi ya maeneo mahususi kama maeneo ya vipaumbele na hasa nikavutiwa na mirdi mikubwa ya kielelezo, ni mingi, lakini napenda kutaja umeme wa maji wa *Nyerere National Park*, reli ya *standard gauge*, Shirika la Ndege kuimarishwa, bomba la mafuta, gesi asilia na huu mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi ambayo sasa hivi yanasantabisha kuweko kwa upungufu mkubwa wa rasilimali ya nishati mbadala kama kuni na uhalisia wa kuhitaji uhifadhi mazingira na haja ya sisi kupiga marufuku ukataji wa mkaa hovyo, napenda kuishauri Serikali kwamba, hii miradi miwili mikubwa ya nishati mbadala, gesi asilia pamoja makaa ya mawe ingepewa kipaumbele kikubwa kabisa. Serikali ingefanya kila liwezekanalo hata kama ni kukopa fedha hii miradi itekelezwe kwa kasi Watanzania waanze kubadilika sasa na kutumia gesi kwa wingi zaidi na makaa ya mawe ili tuondokane na athari za kuharibu mazingira, kuchangia katika hali mbaya ambayo tayari tunayo inayoletwa na mabadiliko ya tabianchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipengele kingine nilipoangalia ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, nimeguswa sana kutaka kusemea maeneo mawili; eneo la kilimo cha mazao na mifugo na eneo la wanyamapori. Kwa

upande wa kilimo cha mazao, katika karne hii ya 21 tuliyopo kwa kweli matamano yangu ni kuona Tanzania ikiondokana na kutegemea kilimo cha jembe la mkono na jembe la kukokotwa na wanyama. Tuondokane sasa katika hiyo sayansi ya karne zilizopita tuwekeze na Serikali ifanye kila liwezekanalo katika kilimo cha kisasa zaidi kinachotegemea matrektta na *power tillers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuishauri Serikali waanze tena kama zamani nilipokuwa mdogo, kuna wakati matrektta ya vijiji yalikuwa yanatolewa. Wapeleke matrektta vijijini hata wakopeshwe vijiji matrektta na *power tiller* stuweze ku-*phase out* kilimo cha jembe la mkono na jembe la kukokotwa na wanyama ili kilimo chetu kiweze kuwa na tija zaidi tuzalishe kwa wingi zaidi. Sambamba na hilo, Serikali iwekeze kwa kila hali katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika sekta ya mifugo nimeona kwamba kuna mipango mizuri inayowekwa ya kuongeza tija, masoko, uzalishaji, maeneo ya malisho, lakini naomba suala la maji lizingatiwe. Asilimia kubwa ya mifugo ambayo ndiyo inabeba uchumi wa wafugaji katika nchi hii ni mifugo ya asili ambayo mingi ndiyo ambayo inaiingizia Serikali mapato kwa mifugo inayouzwa ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta hii ya mifugo, naishauri Serikali kwamba, waangalie katika zile nyanda za malisho za wafugaji, waweke kabisa nguvu katika kuweka maji; maji ya mabwawa, visima virefu, sambamba na kuhakikisha masoko yetu ambayo nimeona wameweka mkazo kwamba, kuna uboreshaji wa masoko na viwanda vyaa kuchakata nyama na bidhaa za mifugo, masoko yetu yahakikiwe yaweze kutoa bei yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mifugo mingi ya nchi yetu inapelekwa nchi za jirani na hasa Kenya. Endapo tutakuja kutengeneza viwanda, tusipokuwa na mkakati wa kuweka bei inayofanana na ile ambayo wenzetu wanaopeleka mifugo Kenya wanaipata, tutaendelea

kupoteza mazao ya mifugo kwa sababu wafanyabiashara wa mifugo wataendelea kutamani kupeleka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itendee Sekta ya Mifugo kama kile kinachofanyika kwenye Sekta ya Mazao ya nafaka kama korosho, kahawa na chai, wawe wanawekewa bei elekezi ambayo ninaamini huwa inatengenezwa kitaalam kwa kuangalia hali halisi ya bei za mazao hayo katika Soko la Dunia. Mifugo pia ifanyie hivyo ili mfugaji aweze naye kupata bei ambayo inamvutia, apende kuuza kwenye masoko ya ndani na apate faida ambayo ataipata tu popote atakapokwenda na asiwe na hamu ya kutaka kupeleka mifugo nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa nimeangalia katika suala la kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu, nikatamani sana nitoe maoni kwa Serikali na nilikuwa niishauri Serikali kwenye suala la ardhi. Ardhi ndijo mama yetu sisi wote, ndijo chimbuko la kila kitu; na ardhi ya Tanzania haiongezeki, sisi tu binadamu ndio tunaongezeka na viumbe wengine walioko katika hii ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itilie mkazo sana suala la upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi kuhakikisha kwamba tunawasomesha wataalam wa kutosha, tunawekeza katika kuweka vifaa vya kutosha na kuhakikisha kwamba hii ardhi inapangwa na ipangwe mapema kuepuka adha tunayopata ya makazi holela na migogoro ya ardhi isiyoisha. Hii itatusaidia sana kuondokana na migogoro na katika kuhakikisha kwamba Watanzania wa kesho watakuta ardhi iliyopangiliwa na ambayo matumizi yake yameshabainishwa na tutaondokana na adha kubwa tuliyonayo kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la wanyamapor, kwa kuwa naona muda wangu umeisha, nilikuwa naomba kwa sababu wanyamapor wameongezeka baada ya uhifadhi kuimarika, Serikali sasa iwekeze katika kuweka *packages*, mafungu yenye kuvutia ya kufidia au kutoa vifuta machozi na vifuta jasho vitakavyowafanya Watanzania

waendelee kuthamini rasilimali yawanyamapori tuliyonayo. Hilo likifanyika, uhifadhi wa wanyama utaweza kuwa guaranteed. Kwa sababu sasa hivi mgongano wa wanyamapori na binadamu unazidi kwa sababu wanyama wamehifadhiwa na sisi pia tunaongezeka; na suluhisho la hilo ni kuwafanya wananchi wawe wavumilivu kwa kuwapa mafao mazuri kutokana na hifadhi ya wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, napenda kusema kwamba naunga Mpango mkono na ninaipongeza Serikali yangu kwa kazi kubwa inayoendelea kufanya katika kutekeleza Mpango wetu wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, niwataje Wabunge tutakaoanzanao mchana. Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua na wengine tutaendelea kuwataja kadiri mjadala wetu utakavyoendelea.

Bunge linarejea.

(*Bunge lilitrudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni leo.

(*Saa 7.02 mchana, Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na majadiliano, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimetaja majina yao, tutaanza na Mheshimiwa Lucia Mloe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwalongo.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote niunge mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie mambo yafuatayo. Jambo la kwanza ni bajeti isiyotosheleza. Kumekuwa na tatizo kubwa la upelekaji wa bajeti za maendeleo karibu kila mwaka, maeneo mengine imekuwa inapelekwa pungufu au haipelekwi kabisa. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo katika mwaka wa fedha 2016/2017 pesa za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 100.25, zilikuwa zimetengwa lakini hadi kufikia mwaka 2017 zilizotolewa zilikuwa shilingi bilioni 2.2 tu sawa na asilimia 2.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeona katika mwaka 2017/2018, Wizara hii iliidhinishiwa na Bunge pesa za maendeleo shilingi bilioni 100.2 lakini hadi kufikia mwezi Machi ni shilingi bilioni 16.5 tu zilikuwa zimetolewa sawa na asilimia 11. Tukija katika mwaka wa fedha 2018/2019 fedha iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika sekta ya kilimo ilikuwa shilingi bilioni 98.119 lakini fedha iliyotolewa ilikuwa ni shilingi bilioni 41 sawa na asilimia 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeona huu mtiririko wote wa bajeti ya miradi ya maendeleo kwa jinsi ambavyo imekuwa ikisusua na kwamba haipelekwi kwa wakati au

inapelekwa pungufu hata pungufu ya asilimia 50. Napenda kuishauri Serikali kutokana na tatizo hilo la kutoweza kupeleka bajeti za kutosha kwenye miradi ya maendeleo au kutopeleka kabisa ni vema basi Serikali ikaona namna gani tunawekeza au tunaweka mazingira wezeshi au mazuri kwa wawekezaji ili waweze kutusaidia katika miradi mbalimbali ya maendeleo kama maji, miundombinu na miradi mingine. Hii ingeisaidia sana Serikali angalau kutokuwa na mapengo makubwa kama ilivyo sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee suala la miradi ya maji. Miradi ya maji imekuwa ni tatizo nchi nzima katika utekelezaji wake. Kwanza miradi mingi imekuwa ikiripotiwa imekamilika lakini kwa uhalisia haifanyi kazi na wakandarasi wamekuwa tatizo. Naishauri Serikali na Wizara ya Fedha tuone namna gani pesa zinazokuwa zimetengwa zipelekwe kwa wakandarasi kwa wakati unaotakiwa lakini wakati huo huo tuwapime hawa wakandarasi maana wakandarasi wengine siyo waadilifu kabisa. Inapogundulika kwamba hawa wakandarasi siyo waadilifu basi watolewe mara moja wasilelewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la maji limekuwa ni tatizo hata maeneo yale ambayo yana vyanzo vya maji vingi tu vya kutosha. Naiomba Serikali tuone namna ya kuwapata wataalamu wanaokuwa wabunifu katika miradi mbalimbali ya maji. Nitoe mfano tu katika Mkoa wa Njombe, ule mji umezungukwa na maji lakini pale Njombe Mjini hakuna maji na tuna wataalamu, kwa nini hao wataalamu wasiwe na ubunifu na kutumia njia nyingine kuhakikisha maji yanaingia pale mjini ukiacha vijijini au ukiacha maeneo mengine ambayo yana ukame. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia suala la maji katika nchi yetu tumeona kipindi cha mvua kunakuwa kuna maji mengi sana na mafuriko. Hivi hatuwezi kupata wataalamu ambao wanaweza wakatuelekeza namna kuvuna haya maji na kuweza kuyatumia wakati wa ukame? Naishauri sana Serikali tuone namna gani tunaweza kuelekeza nguvu zetu kwenye vitu tulivyonyavyo kwa sababu haya maji ya mvua

tunakuwa nayo na hata sasa hivi kuna maeneo mvua zinanyesha sana lakini haya maji hayavunwi mwisho wa siku maeneo haya yanakujakuwa makame lakini wakati huo huo kulikuwa kuna mvua. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni watumishi. Suala la watumishi kwa kweli ni changamoto kubwa. Naiomba Serikali ione namna gani angalau kipindi kilichobakia maana toka tumeingia mwaka 2015 hadi sasa watumishi hawajapandishiwa mishahara angalau hata ya kudanganyishia tu. Watumishi wako katika hali ngumu sana. Nikitoa mfano wa walimu hata nyumba wanazokaa zinatia huruma. Kwa mfano, sasa hivi kuna shule ambazo zinakarabatiwa vizuri sana lakini nyumba za walimu hakuna. Sasa hata kama shule zimekarabatiwa vizuri walimu wanaweza kwenda kufundisha lakini kama wao hawana nyumba nzuri bado haitasaidia. Niombe Wizara ya Fedha tuone namna gani tunawasaidia hawa watumishi hasa walimu kuwajengea nyumba kama tulivokarabati shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni madini. Naomba kuongelea suala la madini Mchuchuma na Liganga umekuwa wimbo wa taifa. Tumekuwa tukiongea juu ya Liganga na Mchuchuma, tulifiki kufikia kipindi hiki tungekuwa tayari tumeshaanza kufaidika na mradi ule. Ule mradi ungekuwa na faida kubwa sana kwa Taifa letu, haya mambo tunayohangaika nayo sasa hivi ya pesa pengine ingekeuwa ni msaada mkubwa sana mradi ule. Naiomba Serikali kwa kweli ichukue hatua ya haraka kutekeleza ule mradi wa Liganga na Mchuchuma kusudi uweze kusaidia kuinua uchumi wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni barabara. Maeneo mengi barabara zimetengenezwa lakini mengine kwa kweli ni tatizo, barabara zimeanza kutengenezwa muda mrefu lakini hadi sasa hazijaisha. Mfano katika Mkoa wa Njombe barabara inayounganisha Ludewa na Njombe Mjini maana ya Itoni –Ludewa, barabara ile kwa kweli ni tatizo, kama ingefanikiwa kwisha ingekeuwa msaada mkubwa sana. Hadi sasa hivi ni asilimia 30 tu na tunaambiwa kwamba

mpaka mwakani inatakiwa iwe imekamilika. Sasa naijuliza kama mpaka sasa hivi imetekelezeka asilimia 30, je, mwakani inaweza kumalizika kwa hizo asilimia 70 zilizobaki? Niombe Serikali mtusaidie fedha kwa ajili ya kukamilishia ile barabara. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mheshimiwa Peter Msigwa ajiandae.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia zawadi ya uzima. Nitumie fursa hii kwanza kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Wizara yake na watendaji wote wa Wizara ya Fedha. Pia niwashukuru na kuwapongeza sana Serikali yetu chini ya Rais wetu John Pombe Magufuli na watendaji wote, tumefanya kazi vizuri kwa pamoja katika Mpango uliopita na matokeo yameonekana na sasa tunaenda kujadili mpango kwa ajili ya mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la kilimo. Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu na Waziri katika kitabu chake ameeleza kwamba mafanikio ya kilimo yamekwenda zaidi ya asilimia 100 lakini kusema kweli ni jambo la kusikitisha sana. Kilimo hiki ambacho kimetuifisha hapa tulipo kwamba nchi ina chakula cha kutosha na kimekwenda zaidi ya asilimia 100 si kilimo kile ambacho kimezalisha kwa nafasi ambayo tunasema ni sahihi, ni kwamba watu wamefyeka sana misitu, wamepanua sana mashamba lakini mashamba yenyewe tija kwa eka iko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hali iko namna hii? Hali iko namna hii kwa sababu, moja, udongo wa nchi yetu haujapimwa. Wananchi wanatibu udongo kwa maana ya

kutia mbolea ya kukuzia mazao yao lakini hawajui kama hitaji la udongo ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mbili wananchi hawa hawana Maafisa Ugani. Wizara ya Kilimo kama sikosei kuna kipindi haikuajiri Mabwana Shamba zaidi ya miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni zana za kufanya kazi. Tumeshuhudia makampuni mbalimbali ya matrekta mengine ya umma yameleta matreka katika nchi yetu matrekta yale mabovu, yamewatia hasara wananchi. Haiwezekani trekta unalimia msimu mmoja halafu inakufa. Tunashuhudia kabisa matrekta ya siku za nyuma yamekuwa imara na yamekuwa yakisaidia sana katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tunapokwenda kuandaa Mpango mwingine, tujipange vizuri tuhakikishe kwamba tunapata Maafisa Ugani wa kutosha katika maeneo yetu ya kilimo ili kusudi wananchi wapate wataalamu wa kutosha. Ni jambo muhimu sana wakulima wapate wataalamu wa kutosha tujipange tupime udongo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye kitabu inaeleza kwamba kutakuwa na upimaji wa matabaka ya udongo basi hilo jambo lifanyike kwa sababu litaenda kuwasaidia wakulima. Mafanikio yake tuyalone kwamba wakulima sasa watumie eneo dogo halafu wazalishe zaidi lakini wanafyeka sana misitu na wanapanua sana mashamba ili kusudi wapate mazao mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwa taasisi zinazoleta vitendea kazi kama matrekta naomba Serikali iangalie. Kama kweli tunataka kuinua kilimo na kusaidia wakulima tuhakikishe kwamba zana za kilimo zinazoletwa kwenye nchi yetu ni imara na zinaweza zikawasaidia wananchi kwa muda mrefu kuliko sasa leo hii ni kilio, madeni waliyokopeshwa wananchi kwa ajili ya yale matrekta hayalipiki, taasisi zilizoleta matrekta zinalia hasara, mabenki yanalia hasara lakini matrekta ni mabovu. Huu ndiyo ukweli wenyewe, yale matrekta ni mabovu. Najua nayasema haya

kuna watu watachukia lakini wacha wachukie tu, matrekta yale ni mabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la masoko. Tutakapokuwa tumewawezesha wakulima tujitahidi kuongeza masoko. Leo hii tunazungumza habari ya soko la Congo lakini tunalenga upande mmoja zaidi upande wa kusafirisha mizigo tu lakini tukumbuke kabisa kwamba mazao ya kilimo vilevile yana soko Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tunaomba sana ile bandari ikamilike. Mtakapokuwa mnapanga mipango hiyo sasa tunawashauri mkamilishe bandari ile na iweze kufanya kazi vizuri kusudi tuanze kupeleka mazao Congo. Siku mzigoto wa Congo utakapokuwa haupo, mazao yetu ya kilimo yatakwenda Congo na kwa idadi ya watu ina maana wao ni wengi kuliko sisi kwa hiyo ina maana wanahitaji kula kuliko sisi ni soko mojawapo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni Mchuchuma na Liganga. Mchuchuma na Liganga hata ukiangalia kwenye *Hansard* za Bunge sidhani kama kuna kipindi cha Bunge kiliwahi kupita bila kuongelea Mchuchuma na Liganga. Hebu sasa Serikali ifanye maamuzi ambayo yataifanya Mchuchuma na Liganga iweze kufanya kazi. Mmesema mmetenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi lakini vilevile mnasema mnataka kulipa fidia sehemu ya kupitisha njia ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke umeme utakuwa ni zao la Mchuchuma ili uende Liganga lakini kuna barabara zinazokwenda kule, iko barabara ya Itoni - Manda mpaka leo tunasema kilometra 30 tunapanga mpango wa maendeleo hapa naomba basi tukamilishe hii barabara kuanzia Itoni - Manda barabara ikamilike. Tunachoambiwa kila siku ni kwamba ile barabara ni ndefu sana ya zege nchi nzima hakuna barabara ndefu kama ile, haiwezi kutusaidia kama hii barabara haijaanza Itoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa kama tunataka kufanya uwezeshaji migodi ile iweze kufanya kazi basi tujipange tuweze kutengeneza na barabara iweze kufika maeneo yale. Imekuwa ni bahati mbaya sana wataalamu wetu wanapopanga mipango unasikitika kuona kwamba wanaweza wakapanga kujenga, nichukulie mfano mmoja tu pale Njombe wamejenga Mahakama ya Mkoa lakini mradi ule ulikuwa ni wa kujenga Mahakama tu hakuna hata barabara kuifikia hiyo Mahakama yenewe. Mkandarasi anapita porini mpaka kuifikia hiyo Mahakama yenewe, hata itakapokuwa imekamilika hakuna fungu la kutengeneza barabara. Kwa hiyo, nafikiri tunapopanga mipango tuhakikisha kwamba kama tunajenga mradi kama Mahakama basi na mipango yake ya kujenga barabara kuifikia Mahakama hiyo iwepo kusudi itakapokuwa imekamilika iweze kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hata Mchuchuma, tunaiendea Mchuchuma tutakapokuwa tunakamilisha kumpata huyo mbia ambaye atashiriki katika kuchimba madini haya basi aikute na barabara iko tayari lakini barabara hii ni barabara ya kiuchumi itasaidia sana kuhakikisha kwamba Mkoa wa Njombe unazidi kuleta uchumi wa kutosha ndani ya nchi. Huu ni mkoa unaozalisha chakula kwa wingi na itasaidia wananchi kufanya kazi zao vizuri lakini ndiyo maendeleo yenewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine kwenye suala la barabara ambalo napenda kuishauri Serikali ni kwamba tunaposema tunataka barabara za kuunganisha mikoa kwanza tujulize tunaunganisha huo mkoa na mkoa ili tupitishe kitu gani? Wakati mwingine tunaunganisha barabara mkoa na mkoa kwa wiki linapita gari moja tu lakini tumeacha barabara inayounga wilaya na wilaya na inapitisha mazao ya kutosha, inachangia uchumi wa nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mtizamo huo tuuangalie upya kwamba tunajenga barabara ambazo zitapitisha mazao, tuuangalie zinapitisha nini. Tusijenge tu

barabara sababu tu watu wapite, waseme tu kwamba tumeunganisha mkoa na mkoa, mmeunganisha *so what*, ili kifanyike nini? Itakuwa siyo msaada. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kuishauri Serikali ni suala la huduma za matibabu ya UKIMWI. Leo hii asilimia kubwa sana ya fedha au ya dawa wanazotumia waathirika wa UKIMWI ni za msaada. Tutambue moja huu msaada iko siku utakuwa na ukomo, ni lazima kwenye mipango yetu tuhakikishe kwamba tunajiwekea utaratibu wa namna gani tutajimudu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pekee kabisa kwenye suala la UKIMWI liko suala la watoto waliojikuta wamezaliwa na maambukizi ya UKIMWI, watoto hawa wana hali mbaya sana ya lishe. Kama Serikali kwenye mipango yetu ambayo tunaenda kuipanga sasa kwa ajili ya bajeti ijayo tulione hilo na tuhakikishe kwamba tunatenda kiwango kwa ajili ya kusaidia watoto ambao wameathirika na UKIMWI kwa sababu wamepata UKIMWI kutoka kwa wazazi wao. Watoto hawa wanapokuwa shulenii lishe ni duni sana na wanashindwa kusoma vizuri na magonjwa nyemelezi yanawasumbua sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutokuwa na bajeti ya Serikali kwenye jambo la kuhudumia watoto waliothirika na UKIMWI watoto hao wengi sana tunawapoteza. Leo hii wagonjwa pekee wallobaki wanaumwa zaidi kutokana na tatizo la UKIMWI ni watoto ambao wamejikuta wana maambukizi kutokana na kuzaliwa na wazazi ambao walikuwa na maambukizi.

Kwa hiyo, ni ushauri wangu kwa Serikali itakapokuwa inapanga bajeti ihakikishe kwamba inaangalia kwa jicho la pekee kwamba tuwe na fedha ya kuweza kusaidia watoto hawa ili kusudi waweze kupata huduma bora ya chakula ili afya zao ziweze kuimarika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nashukuru sana kwa fursa. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni ajiandae.

MHE. DAIMU I. MPAKATE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi jioni hii kuchangia hoja mahususi, naomba kwanza niunge mkono hoja hii. Pili, naomba niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutimiza dhamira ya kuunganisha Mtwara na Mkoa wa Ruvuma kwa maana ya Mtwara *Corridor*kuhakikisha kipande kile cha Mbanga kwenda Nyasa kimeanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba jambo hili haliwezi kukamilika kama hatutaweza kuzungumzia suala la reli ya kusini ambayo inaunganisha kati ya Mtwara na Mbambabay. Ukweli uzalishaji wa makaa ya mawe Ngaka, tunapozungumzia Mchuchuma na Liganga jambo hili haliwezi kwenda sawasawa bila kuzungumzia suala la reli ya kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali, nimeona kwenye maelezo ya Mheshimiwa Waziri lakini hayaleti matumaini kwa sababu wameendelea kutafuta wawekezaji wa reli hii lakini bado tunaona *speed* ya kuweza kuwekeza katika reli hii bado ni ndogo. Tunaomba, tunapofikiria suala la kujenga kiwanda cha Mchuchuma na Liganga iende sambamba na ujenzi wa reli ya kutoka Mtwara mpaka Mbambabay ili kusukuma maendeleo katika ukanda wa kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu kwa sasa hivi kwa kweli zinaharibika sana, kwa mfano kuna malori makubwa sana yanayobeba makaa ya mawe kutoka Ngaka kwenda Dar es Salaam yanapita Songea – Tunduru –Lindi na kufika Dar es Salaam, lakini bado mengine yanapita Songea – Njombe mpaka Arusha. Jambo hili kidogo kama tungekuwa tuna reli basi barabara hizi zingeweza kudumu kwa muda mrefu, ukiona barabara ya Songea – Njombe ina hali mbaya sana, kama ni mgeni unaendesha barabara ile basi

utegemee kupata ajali wakati wowote kwa sababu barabara ile ina hali mbaya, inatokana na kwamba inabeba mizigo mizito ya makaa ya mawe kutoka Ngaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nilidhani katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri angeweza angalau kuingiza suala la ujenzi wa meli katika mwambao wa bahari. Kwa kweli barabara ya Mtwara – Lindi mpaka Dar es Salaam imeharibika sana; Dangote peke yake ana magari 600 ambayo kila siku yanabeba simenti kupeleka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *solution* ya jambo hili ilikuwa ni Serikali angalau kuweka msisitizo wa kuwa na meli ya mizigo kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam ambayo ingeweza kupunguza adha hii. Naomba Mheshimiwa Waziri aende kutoka Mtwara kuja Dar es Salaam ataona barabara ile jinsi illiyoharibika kwa hali ya juu, kitu ambacho kingeweza kupunguzwa na usafirishaji wa simenti kwa kutumia meli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naomba kulizungumzia ni suala la umeme vijiji. Naipongeza Serikali kwa jitihada kubwa inayoifanya. Pamoja na pongezi hizi, umeme vijiji una dosari kidogo; baadhi ya maeneo vijiji kwa kweli vina hali mbaya, umeme haujafika. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu mpaka sasa nina vijiji vitano tu kati ya vijiji 65, kwenye awamu hii nilipewa vijiji 23 lakini mkandarasi bado hajaweza kufikisha hata vijiji nne, ukimuulizia ni suala la nguzo ambalo linasumbua. Jambo lingine ambalo linasumbua wanadai mkandarasi hajalipwa kwa muda mrefu anafanya kazi, *invoice* *ime- raise* lakini pesa bado hajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, suala la umeme kwenye Halmashauri ambayo ina majimbo mawili ina shida kidogo, utakuta Halmashauri hiyo hiyo mwenzako ana vijiji 20 wewe una vijiji viwili. Jambo hili watu wa REA wanavyopanga mipango yao ya kupeleka umeme vijiji basi waangalie maeneo ambayo yana Majimbo mawili, basi waangalie maeneo hayo wawe wanagawa vijiji kadiri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tunapiga kelele sana kwamba viji na vitongoji vyote vitakuwa na umeme lakini shida iliyokuwepo wakandarasi wanapewa *scope* endogo sana, ukiangalia *high tension* inaenda kilometra 30 mpaka 40, katikati anavyopita kuna vitongoji ambavyo havijatajwa kwenye hiyo *scope*. Kwa hiyo, naomba sana kwa awamu ijayo basi waangalie *scope* wanayopewa wakandarasi kwa ajili ya kusambaza umeme katika vitongoji mbalimbali basi iongezwe angalau vile vitongoji vilivyo katika *line* ile viweze kupata umeme kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuliongelea ni suala la kilimo, kama wenzangu walivyoongea, kilimo ni uti wa mgongo lakini kilimo kwa upande wa kusini (upande wa korosho) tunategemea sana mfumo wa stakabadhi ghalani. Mfumo wa stakabadhi ghalani hauwezi kufanyika bila maghala, kuna maghala ya Bodi ya Korosho yana muda mrefu sasa hivi ni mwaka wa tatu yalianza kujengwa lakini mpaka leo yale maghala hayajaweza kukamilika. Naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa jicho la huruma, tuna shida sana ya maghala katika maeneo yetu hasa upande wa Tunduru hatuna ghala la kudumu ambalo lina uwezo wa kuhifadhi korosho kwa wakati mmoja ili biashara ya mfumo wa stakabadhi ghalani iweze kufanyika kama inavyofanyika kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la maghala hata ukiangalia kwenye vyama vya msingi kwa maana ya vijiji, maghala yao mengi ni mabovu, yanavuja, yanahatarisha usalama na ubora wa mazao hasa korosho pamoja na mazao mengine mpunga, mahindi, ufuta na kadhalika. Kwa hiyo, naomba sana bajeti ijayo iangalie namna ya kusaidia angalau ujenzi wa maghala katika vijiji mbalimbali ili kupunguza adha hii ambayo inawakumba wakulima wetu kukosa mahali pa kuhifadhi mazao yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda nilizungumzie ni suala la maji; maji ni uhai. Kuna siku moja nilicheka kidogo, Mheshimiwa Diwani mmoja alisema hivi tusipooga wote hapa wiki nzima tutakuwaje?

Jambo hili ni zito sana kwa sababu vijiji maeneo mengi ukame umeathiri maji, maji yamekuwa ni tatizo. Naomba angalau tuweze kuhakikisha kwamba tunapata fedha nyingi zinazoweza kuchimba visima angalau kila kijiji kipate visima vitano ama vinne, tujinyime kwa maana ya aina yoyote ile kwa sababu bila maji maisha kwa kweli yanakuwa ni magumu kwa sababu wote tunaishi kwa kutegemea maji na magonjwa mengi yanapungua kama maji yatakuwepo ya uhakika na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana pamoja na Waziri anayehusika basi waliangalie suala la maji katika maeneo mbalimbali ya vijiji vyetu kutilia mkazo ili kuhakikisha kwamba angalau asilimia ile ya maji iongezeke ili wananchi waweze kupata maji salama ambayo ni ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo napenda nilizungumzie ni suala la TARURA. TARURA kwa kweli wana kazi kubwa lakini kazi yao inakwamishwa kwa sababu pesa wanayopewa ni kidogo ambayo haikidhi barabara ambazo tunazo/TARURA wanazimiliki. Ukichukulia mfano Wilaya ya Tunduru, ina kilometra 1,200 za barabara za vijiji ambazo zinamilikiwa na TARURA, lakini pesa wanayopewa inaweza kutengeneza kilometra 100 mpaka 200 tu, sasa sijui tutachukua miaka mingapi kuzipitia barabara hizi mpaka kumaliza maeneo yote. Kwa hiyo, naomba sana Serikali waangalie namna ambavyo wanaweza kuwaongezea pesa TARURA waweze kufanya kazi yao vizuri na waweze kuwashudumia wananchi kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni suala la afya. Naishukuru Serikali imefanya jambo jema la kuongeza vituo vya afya ambavyo vimeleta tija na matumaini kwa wananchi wetu. Jambo hili linaenda sambamba na idadi ya watumishi, mimi Jimboni kwangu tuna vituo vya afya viwili lakini kila kituo kina wafanyakazi sita/saba, jambo ambalo linakwamisha juhudii hizi za kujenga vituo vya afya vipya na vizuri na utoaji wa huduma haulingani na hadhi ya

vituo nya afya ambavyo vipo kwa sasa. Kwa hiyo, naomba Serikali ifikirie suala la ajira la watumishi wa afya kuongeza ili kuhakikisha kwamba tunapunguza kero ya watumishi wa afya katika zahanati zetu, vituo nya afya pamoja na hospitali zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni suala la watumishi upande wa elimu. Halmashauri yetu ya Wilaya ya Tunduru ina zaidi ya shule 157, ina upungufu wa Walimu zaidi ya asilimia 40 ambayo ni zaidi ya Walimu 600. Naomba Serikali iangalie namna pekee ya kuongeza idadi ya Walimu hasa kwenye shule za msingi na sekondari ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata elimu iliyo bora na ambayo inaweza kuwafanya waweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hili ya kuongea. Ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilikuwa nimewita Mheshimiwa Peter Msigwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni na Mheshimiwa Boniface Mwita Getere ajiandae.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Mpango, wakati anatuletea Mpango wa Miaka Mitano mara tu baada ya Serikali kuinggia madarakani, mojawapo ya mambo ambayo Serikali ilikuwa imetutangazia na kutuahidi kwamba itayafanya ni pamoja na masuala ya demokrasia na utawala bora ambayo yanapatikana katika ukurasa wa 111 katika kitabu hiki cha Mpango wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya mambo ambayo aliyasema alisema kuhakikisha usawa wa kiuchumi, demokrasia na uvumilivu wa kisasa katika jamii. Ukomavu wa demokrasia na ushiriki wa wananchi utazidi kuimarishwa kupidia, akaelekeza mambo gani yatapitia jinsi gani itakavyoimarishwa. Mojawapo alisema kuwekeza zaidi katika kuboresha mfumo wa uchaguzi na kufanya kuwa wa kisasa

zaidi pamoja na kuzidi kupanua uhuru wa kujieleza, uwazi, upatikanaji wa habari; kuna mambo mengi sana alizungumza katika mpango wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapozungumza tunakwenda kumaliza kipindi chetu kama Wabunge, Madiwani na kama Mheshimiwa Rais, lakini haya mambo yote ambayo Mheshimiwa Mpango alikuwa ameahidi katika mpango, Serikali ilituhakikishia kwamba itaimarisha demokrasia tukianza moja baada ya jingine katika kipindi cha miaka mitano, kila kitu hapa kimedorora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uwazi wa vyombo vya habari, hakuna mfumo mzuri wa uchaguzi, hakuna mfumo wa kidemokrasia. Mara tu tulipoingia Bungeni hapa, kitu cha kwanza tulizuiwa mikutano, tukazuiwa *Bunge live*. nataka nimuulize Mheshimiwa Mpango huko ndio kuimarisha ambako alikuwa anatuambia wakati akituambia miaka mitano? Kwa sababu wamezuia *Bunge Live*, wamezuia mikutano wakasema Wabunge sehemu tunazotoka tutaruhusiwa kufanya mikutano na yenyewe wamezuia. Kibaya zaidi walisema wataimarisha chaguzi na hiki tunachokiona sasa katika nchi yetu ya Tanzania ambacho hakijawahi kutokea ni ishara tosha kwamba Serikali yenu haina mpango wa kuimarisha demokrasia na chaguzi huru katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa bahati mbaya Mheshimiwa Jaffo hayupo hapa, kinachofanyika sasa hivi kwenye Serikali za Mitaa kimsingi Chama cha Mapinduzi wanakunywa sumu. *You are just drinking poison*, inawezekana isiwaue leo lakini itawaua kidogo kidogo. Hamuwezi kusimama hapa mka-*claim* kwamba ninyi ni ma-*champion* and you don't want to compete; victory inatokana na ushindani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajiitaje washindi na hawataki kushindana? Katiba yetu inasema kila baada ya miaka mitano tutapambana uwanjani na viongozi bora

wanapatikana baada ya ku-*compete*, hawataki *competition*, huo ni utawala bora wa aina gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunapozungumza, Wenyevit wa Mitaa wote karibu nchi nzima wamefunga ofisi wamekimbia, hawataki kupokea mapingamizi, watendaji wote wamekimbia kwenye ofisi za umma, tunasema tunataka tuzungumzie utawala bora, hawapo wanakimbia... (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waitara.

TAARIFA

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpe taarifa mchangiaji kwamba hili jambo limezungumzwa jana na leo. Mheshimiwa Spika jana alitoa maelekezo, leo wewe umetoa maelekezo na hapa tunapozungumza Mheshimiwa Waziri hayupo hapa lakini amekwenda Singida akakuta mambo sio kama walivyozungumza humu ndani, ameenda Manyara; tumetuma maafisa wetu wamekwenda kule Moshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampa taarifa kwamba Mheshimiwa Msigwa tunayo kuanzia jana tarehe 5 na tarehe 6 ya mapingamizi, tunayo tarehe 6, 7 mpaka 9 ya Kamati ya Rufaa; maelekezo yaliyotolewa na Serikali ni kwamba kuna mtu amelalamika kama inavyozungumzwa waandike barua za malalamiko na malalamiko yatafanyiwa kazi, tunao muda mpaka tarehe 9. Kwa hiyo, usianue kwanza matanga kabla msiba haujaisha. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa unaipokea taarifa hiyo?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii taarifa siipokei, inaonekana Mheshimiwa Waziri anataka kupotosha na hana *information*. Mimi kwenvye Jimbo langu nina mitaa 192, wameenguliwa watu 185, sasa hivi wapo kwenvye Ofisi za Kata zote zimefungwa; *what are you talking about?* Halafu mnataka kusema mnashinda, mnashindaje? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano, wakati wa *segregation* kule Marekani Malcom X anatoa hotuba moja naomba ukaisikilize, kulikuwa kuna *field negro* na *house negro*. Humu ndani inawezekana wengine ni *house negro* hawajui tunacho-*feel*/sisi ambao ni *field negro* kwenvye *field*. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hamjui madhira tunayoyapata, kufanya siasa katika nchi hii imekuwa ni *criminal*, unahesabiwa kama ni mhalifu kufanya siasa ya nchi hii wakati Katiba inanipa mamlaka/uhuru wa kujieleza (*freedom of expression*). Ninyi mmekuwa ni *house negro* kwa sababu ni *beneficiary* wa mambo haya ndio maana hamuwezi kuyaona. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuongea na wapiga kura wangu kwenvye Jimbo langu na Wabunge wengi wenzangu wa upinzani ni uhalifu katika nchi hii. Tunaambiwa sisi lazima tuombe ridhaa ya kufanya mikutano, wengi wenu ninyi huwa mnaenda kufanya mikutano huko wala hamuulizwi na mtu yejote. Kwa hiyo, tunaongea mambo ambayo tuna-*feel*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nchi hii mnaasema tushindane, Katiba inataka kila baada ya miaka mitano tushindane na nyie mnaasema chama chenu kimeimarishwa; miaka minne hatujaongea, hatujafanya mikutano, Wenyevit wa vyama vyetu hawajasafiri, mmesafiri ninyi peke yetu. *Television* mmezishika nyinyi peke yenu, unasema utawala bora; huo ndio utawala bora mnaotuambia hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *television, radio*, mikutano ninyi, tunakuja kwenvye mikutano *seven days, you are running*

away, halafu mnakuja hapa mnasema tunatengeneza demokrasia, *what kind of democracy is this?* Mkifika uchaguzi mnakimbia mnasema kuna *democracy*, *what democracy is this?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja hapa kama tunataka tutengeneze nchi yetu tukubaliane kama tumeamua kufuta mfumo wa vyama vingi *its well and good*, mpo wengi, leteni Muswada wa Sheria hapa kwamba tumefuta mfumo wa vyama vingi tutabana hukohuko si itakuwa ni sheria, tutabana hukohuko kwenye majimbo yenu maana yake itakuwa ni sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya nchi yetu inatupa uhuru kwamba, mtu ana mawazo tofauti na mwagine wala hatugombani, wewe una mawazo yako na mimi nina mawazo yangu, tunashindana kwa hoja, baadaye tunaenda kwa wananchi, huo uhuru uko wapi katika maelezo ya Mheshimiwa Mpango aliyoandika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kitabu hicho hicho Mheshimiwa Waziri amesema kuhikisha kuwepo kwa mgawanyo wa madaraka na ufasaha wa mipaka baina ya mihimili mitatu ya Serikali kwa kuimarisha uwezo wa taasisi na rasilimali watu kwa kila mmoja kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *democracy ilivyoanza, separation inahitaji balance*, tunahitaji *ku-balance*, mhimili unaojitegemea wenge mamlaka na nguvu. Tunapozungumza, nimezungumza hapa leo *Bunge Live* lilitimwa, huu ni mkutano wa wananchi wa Tanzania, tunakuja kutunga/ tunapoingia Bungeni hapa tunapanga bajeti ya wananchi milioni 50 waliotutuma tuje tuwatenge hela zao katika bajeti hii, tunazungumzia kuhusu afya zao, kilimo, shule na afya zao, leo tunapozungumza Wabunge tuliotumwa tunakuja hapa tupo gizani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya ambapo Mheshimiwa Spika alikwenda, wao mpaka kamati zipo *live*.

Tunazungumza *separation of powers*, nguvu ya mhimili wa Bunge, hawa tunaowasemea mimi sijaja peke yangu na kila mmoja hajaja peke yake, anawawakilisha watu wake. Tumekuja hapa ili wananchi wale waliotutuma wasikilize tunachosema, tunafanya gizani; hiyo ndio *separation of power?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasiasa tunashinda mahakamani kwa kosa la kufanya siasa, sisi sio wezi, hatujavunja nyumba. Ninyi Serikali ya Chama cha Mapinduzi mnapata wapi *legitimacy* ya kusema watu wasiwe wezi kama nyie wenyewe mnaiba kura, *where do you get that?* Kama nyie wenyewe mna-rob kura mnapata wapi kwamba watu wasiibe mitihani, mnawaambia watoto wasiibe mitihani kama ninyi wenyewe hizi kura mnanyang'anya kwa nguvu, mnapata wapi kwamba watoto wasiibe mitihani? (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

MHE. MICH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, *where do you get that, where do you get that power?*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU ENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

MBUNGE FULANI: Wanatengeneza hao.

MHE. MICH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Naibu Spika, mnapata wapi hiyo nguvu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa. Mheshimiwa Jenista Mhagama, Utaratibu Kanuni.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa

Naibu Spika, ninaomba nitumie Kanuni ya 68 lakini naomba niende 68(1) lakini niende Kanuni ya 64(1) Kanuni ndogo ya (a) hiyo inakataza kabisa ndani ya Bunge mtu kutokutoa taarifa ambazo hazina ukweli lakini nitakwenda mpaka Kanuni ya 65. Naomba Mheshimiwa Mbunge kwa kweli asiendelee kulipotosha Bunge kwamba uwepo wetu sisi hapa ndani na uwepo wa Serikali yetu unatokana na vitendo vyatizisho wa kura na ndivyo vinavyotufanya tuendelee kuwepo madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhuma hii, ni tuhuma kubwa na ni tuhuma ambayo sisi tunaojua Sheria na taratibu ushindi wa mgombea yoyote unatawaliwa na Sheria tulizonazo, Sheria za uchaguzi Katiba ya Nchi yetu na hapa ndani ya Bunge tunatawaliwa na Kanuni katika kuyaeleza hayo. Mgombea yoyote ambaye hajashinda ana uhuru wa kwenda Mahakamani na kwenda kueleza Mahakamani na kule Mahakamani wanaweza wakatoa nafasi ya mgombea yoyote kuthibitisha ama kuweka wazi kile kinachomkera. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, si kweli na nadhani anataka kutudhalilisha anapotutuhumu sisi wote, Serikali nzima, Wawakilishi wote wa Wananchi na hasa kuitia Chama cha Mapinduzi kwamba uwepo wetu hapa ni uwepo ambao si halali jambo hili si sahihi na anavunja Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, tunamuomba sana Mheshimiwa Msigwa ama afute kauli hizi ama ajielekeze katika mjadala bila ya kuwa na tuhuma ambazo si za sahihi na hazina ukweli kwa mujibu wa Sheria tulizonazo kwa mujibu wa Kanuni na kwa mujibu wa Katiba.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge alikuwa akichangia Mheshimiwa Msigwa, ametoa maelezo marefu ambayo Mheshimiwa Waziri wa Nchi amesimama kuhusu utaratibu akataja Kanuni ya 68 na akataja Kanuni iliyokuwa ikivunjwa na Mheshimiwa Msigwa Kanuni ya 64(1)(a) ambayo Kanuni ya 64 kwa ujumla wake inazungumzia mambo yasiyoruhuswa Bungeni na (1)(a) inazungumzia kutokutoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Msigwa kwa muktadha wa Kanuni zetu ukisoma hii kanuni ya 64 ukizungumzia taarifa ambazo hazina ukweli itatupeleka kwenye Kanuni ya 63 inayozuia kusema uwongo Bungeni. Sasa kwa muktadha wa Kanuni hizo hizo zinataka hizo taarifa kama hazina uwezo wa kuthibitishwa basi Mbunge apewe fursa ya kufuta hayo maneno yake ili aendelee kuchangia. Kwa hiyo, na wewe nitakupa hiyo fursa ya kufuta hayo maneno yako halafu tutaangalia utaratibu mwingine kama utakubali kufuta, utakuwa umefuta kama hukukubali maana yake nitasimama tena.

Mheshimiwa Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza suala hilo ukienda Ndarambo kule kwenye Jimbo la Silinde kura ziliibiwa kabisa mpaka tukaenda...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, hapo unataka kueleza maelezo mengine, umepewa fursa ya kufuta kauli uliyokuwa ukizungumza, kama hukubali kufuta hiyo kauli uliyokuwa unasema, wewe sema ili nitoe maamuzi, umepewa fursa ya kufuta kauli uliyokuwa ukizungumza kama hukubali kufuta unao ushahidi, wewe utasema, mimi nitaendelea na utaratibu wetu wa Kikanuni. (*Kicheko*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi wa kuibiwa kura tunao, ninao.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa hizi Kanuni zetu na mambo ambayo tunaweza kuzungumza humu ndani na sasa tunaelekea kukamilisha hili Bunge letu nataka kuamini kila mtu anaelewa Kanuni zetu matakwa yake ni yapi?

Kwa kuwa Mheshimiwa Msigwa unao ushahidi wa kuibiwa kura, na kwa kuwa huo ushahidi mimi hata ungeniletea hapa sina uwezo wa kujua kama ni wa kweli ama siyo utaenda kwenye Kamati ya Haki na Maadili ili ukathibishe kule hiki ulichokisema hapa.

Kwa hiyo, kwa mchango wako wa sasa hayo maneno ya kuibwa hutarudia mpaka utakapoenda kuthibitisha kule ile Kamati Italeta taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

MWENYEKITI: Nadhani tumeelewana vizuri, maneno ya kuhusu kuibwa kura utaenda uthibitishe kule kwenye Kamati.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema tunapata wapi *legitimacy* kama sisi wenye katuwezi kuishi yale tunayoyasema, Mheshimiwa Mpango kwenye Mpango wako.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Taarifa.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *democracy*...

MHE. DKT. GODWIN O MOLLEL: Taarifa ...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Democracy* ni kitu cha msingi ambacho...

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Taarifa ...

MBUNGE FULANI: Taarifa ya nini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa kuna taarifa. Mheshimiwa Dkt. Mollel.

TAARIFA

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi mwenzangu hapa anajaribu kuzungumzia *legitimacy* ya kuzungumza mambo ya kiadilifu na kufanya mambo ya kiadilifu. Lakini ye ye kwenye Kambi yake, kwa maana ya Chama cha Chadema Wabunge wote

sasa hizi wamegoma kuchangia chama kwa sababu ya Mwenyekiti wao kuiba milioni mia sita akiwa yeye ni mbeba mkoba, akiwa yeye ni mmoja wapo wa wabeba mkoba kwenye wizi huo na hata ruzuku haionekani na siasa ndani ya chama chake, ndani ya chama chake haiwezekani kwa sababu hakuna *resources* na watu wote wamegoma kuchangia na kusaidia chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anasema hata huo wizi alitumwa na Chama cha Mapinduzi ufanyike na kwenda kununua hizo shamba Morogoro na vitu vingine ambavyo ni vyta kibadhirifu vilivyoumiza chama chake.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa unaipokea taarifa hiyo?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea utasema naye athibitishe kwa sababu anatuhuma watu kwamba wameiba.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa unazifahamu Kanuni ametoa taarifa, Kanuni inayohusu taarifa ni Kanuni ya 68 na uzuri tumeletewa na Mheshimiwa Spika hapa huna haja ya kubeba makaratasi, fungua Kanuni yako soma ya 68 amesimama kuhusu taarifa, unaipokea taarifa hiyo?

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei, *his house kneegrow anyway.*

MWENYEKITI: Eeeh! Halafu Mheshimiwa Msigwa, unajua tangu mwanzo nilikuwa nimekuacha na wewe unafahamu hayo maneno huko kwenye nchi unayoisema yana maanisha nini. Na wewe unasoma vizuri huwezi kuita Mbunge mwingine kama *kneegrow*, kama wewe unataka kuiita *kneegrow* ni suala lako wewe.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Haja-*complain*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Haja-*complain*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Ehehe! Hamna aliyelalamika.

MWENYEKITI: Natoa maelezo kuhusu jambo unalotakiwa kulifanya ndio ninacho...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Haja-*complain*...

MWENYEKITI: Naomba ukae, naomba ukae. Siyo suala la yeye ku-*complain* kazi yangu mimi kusimamia utaratibu hakuna Mbunge anayeweza kuitwa *kneegrow* humu ndani hayupo.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kasema Mbowe mwizi, kasema Mbowe mwizi, kasema Mbowe mwizi, umenyamaza,

MBUNGE FULANI: Mwizi.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, si umenyamaza alivyosema Mbowe mwizi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa, Mheshimiwa Msigwa tusibishane, nimesema nakuelekeza utaratibu, kama unataka kuusikiliza, sikiliza usijibizane na mimi. Nasema hizi maneno hayo kule yanakotumika yana maanisha kitu kibaya sana na wala hakuna mtu anataka kuitwa hayo maneno. Humu ndani hawezi kuitwa Mbunge mwingine hayo maneno kama mtu amelalamika, ama hajalalamika kazi yangu kusimamia utaratibu na nilikuwa nimekuacha tangu mwanzo ili umalize mchango wako halafu nije niseme mwisho ana maanisha nini, sasa kwa kuwa unaendelea kuyasisitiza hakuna Mtu anayeitwa jina hilo humu ndani, naomba uendelee na mchango wako. (*Makofi*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mpango ninachokisema kwenye kitabu chako ulituambia utasimamia *democracy*, tunaongea miaka mitano sasa tunamaliza kipindi chetu *democracy* ya nchi hii sasa hivi iko /CU, uhuru wa Vyombo vya habari ni *disaster*, waandishi wa habari wamekamatwa, wengine wamepotea, wengine hawawezi kujieleza, vyombo vingine vimekamatwa, Wabunge hawawezi kufanya mikutano kwenye majimbo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea kwa mfano miaka miwili hawezi kufanya Mkutano, Mheshimiwa Halima hawezi kufanya Mkutano, Mheshimiwa Sugu hawezi kufanya Mkutano, Wabunge tunakatazwa, hii ndiyo *democracy* inayosema kwenye Mipango ya miaka yako mitano, na ulivyokuwa unazungumza Bajeti ya mwisho hapa ulinukuu mpaka maneno ya Mungu, ukasema Mungu atusaidie, ukanukuu na vifungu vya Biblia, halafu ukasema wananchi wakachague wagombea wa Serikali za Mitaa wanaotokana na Chama cha Mapinduzi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo huu uchaguzi ambao unasema wakachague huu wa kupora, wa kupora kwa nguvu, katika nchi ya kidemokrasia, hebu vaeni vitu vyetu nimesema mna hiari mko wengi, leteni Muswada hapa kwamba tunafuta mfumo wa Vyama vingi tusijidhalilishe Duniani kwamba tuna *democracy* wakati hakuna *democracy*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaogopa, mnaweka mpira kwapani halafu mnashangilia, tumeshinda, tumeshinda... Unaweza kuwa *champion* bila kushindana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *the finishing line is for the winners, you cannot be a winner without competition*, ingizeni mpira hapa, tuweke Wagombea wetu na ninyi muweke, tuone mziki wananchi wanamtaka nani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka mitano mmetuzuia, mmetuzuia muone tutakavyocheza mpira uwanjani, *how do you call you self that you're a champions*. Watu wa Turkey, Waturuki wanasesma *when the fish is rocking it is start from the head*. Hizi zote vurugu za Watendaji wa Mitaa na nini, ni matatizo ya Wizara, ni matatizo ya Serikali yenye, hiki kiburi cha kufunga Ofisi cha kufanya nini, msitudanganye, ni kwamba mmeona huko nje hali ni mbaya mlisema tumekufa, hatujafa, *we are still standing*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnajiaminisha mnaweza njooni uwanjani tucheze mpira, ili hayo uliyoyasema yathibitike tuweze kuendesha nchi nzuri ambayo Mungu ametupa, tусidanganye hapa, nakushukuru sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere. Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, napenda niungane na wenzangu wote kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, pamoja na timu yote ambayo wameandaa Mpango huu vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana hapa tuna ongea lugha ambayo haieleweki tu, lakini Watanzania sasa wanaelewa, hata Mheshimiwa ambaye amemaliza kuzungumza sasa hivi anasema kwamba eti kwamba tunaua demokrasia, demokrasia ni historia katika nchi yoyote ile, Watanzania sasa hivi naomba niwapeleke kwa *statistics*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2015/2016 Uwekezaji kwa wananchi ilikuwa ni zaidi ya triliioni 29.5 .

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 ukafika triliioni 48.5, 2017/2018 triliioni 55.17, na sasa hivi hadi Juni 2019 ni triliioni 59. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake nini, *translation* yake Mheshimiwa ambaye alikuwa anazungumza hapa ni kwamba Watanzania sasa wameanza kuelewa demokrasia ni maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Watanzania wameelewa kwamba kuitia maendeleo haya sasa walichagua Serikali halali ya chama cha halali na ndiyo maana sasa hivi hata wagombea wengi hawajajitokeza kwa sababu hiyo. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Eehhe!

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua tuseme kitu ambacho Watanzania wanataka, hatutaki maneno na porojo, tunataka *translation* ya uchumi katika maisha ya Mtanzania, na sasa hivi nchi inavyokwenda chini Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ndani ya miaka minne, tumeona mambo mengi yamefanyika na ndiyo watu walikuwa wanahitaji hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo, mnapotsema kwamba hakuna demokrasia, jamani, hivi demokrasia maana yake nini? Demokrasia ni kwa ajili ya watu, ni kwa ajili ya watu na kwa mahitaji ya watu, sasa leo Watanzania wameridhika na maendeleo yanayoendelea sasa hivi hapa nchini, tumesema ujenzi wa misingi ya uchumi. (*Makofii*)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MBUNGE FULANI: Taarifa ya nini wewe....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Chegeni kuna taarifa. Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa mzungumzaji anasema wananchi wameridhika na ndiyo maana hawajajitokeza, lakini tunataka tumkumbushe tu kwamba sisi tumesimamisha

vitongoji vyote, Mitaa yote na Vijiji vyote nchi nzima, lakini pia hatutaki demokrasia anayosema kama ile ambayo walikuwa wananyang'anyana matokea na Mheshimiwa Kamani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji demokrasia ya haki ambayo Mtanzania anataka kwenda kupiga kura, ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Chegeni unaipokea taarifa hiyo?

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naona siipokei. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nazungumzia hapa ni maendeleo ya Watanzania. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba leo hii, kama umewekeza kwa kiwango hicho, maana yake ni kwamba Watanzania walichokitamani wanakipata, leo ukizungumzia suala la maendeleo, tunazungumzia katika Mpango huu kwamba lazima tujenge misingi ya uchumi wa viwanda, maana yake nini, maana yake kwamba tujielekeze Watanzania sasa kumboresha Mtanzania na aweze kufikia kiwango cha kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tupunguze porojo na maneno, Watanzania tumeongea sana, miaka nenda rudi, lakini ndani ya minne, tumefanya mambo makubwa sana, ambayo kila mmoja ana historia nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninyi Wabunge wote, pamoja na mimi tukienda Majimboni kwetu tunaona miundombinu iliyopo, hii ya Afya, Elimu, Maji, Barabara na vyote vile, ni kwa sababu gani kumekuwa na usimamizi mzuri wa utekelezaji wa Mipango ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wananchi wanachagua nini, wanachagua maendeleo, hawachagui

maneno, Watanzania wanachagua maendeleo, sasa mnapoanza kulalamika kwamba hakuna demokrasia, nawashangaa wakati mwininge, hebu muanzie nyumbani kwenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi mna demokrasia gani? Kwa sababu katika baadhi ya vyama hapa hakuna demokrasia ndani ya vyama vyenu, lakini hamlalamiki, sasa niseme kwamba hebu tuji-*focus* kwenye Mpango wa maendeleo ambao una tija zaidi kwa Watanzania.

MBUNGE FULANI: Una demokrasia!

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu ukiangalia mwaka huu peke yake wa fedha tumetenga asilimia 37 ya Bajeti yote kwa shughuli za maendeleo, hao ni Watanzania wanataka hayo, leo umepanga trillioni 12.2 kwa ajili ya Miradi ya maendeleo, na hii ni kwa Watanzania wote bila kujali wa chama gani, na maendeleo hayana chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu-*translate* ndoto ya Mheshimiwa Rais na hii naomba Watendaji na Wasaidizi wote, ndoto ya Mheshimiwa Rais kutokana na Watanzania sasa wanapata maisha bora, wanapata maendeleo ya kiuchumi, wanasonga mbele, haya yote utayafanya ikiwa sisi sote tutaenda katika mwendo ule ambao Mheshimiwa Rais anautazama, na mimi niseme kwamba lazima tufike Watanzania tujifunze tufanye namna hiyo, lakini vilevile Miradi ya Mikakati ambayo leo Watanzania tunaifanya, tumeona Miradi mbalimbali haijafanyika, lakini tumeanzisha Miradi mikubwa ambayo hatukuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Mashirika mengi ya Umma, tuliweza, na mengine yalikufa, mengine hayakufanya vizuri, leo hii kupitia Wizara ya fedha, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina na Kamati ya Uwekezaji tumeweka vigezo, KPI ili kusudi uweze kupima mwenendo wa kila Shirika na Taasisi ya Serikali aidha inatoa huduma au inafanya

biashara, na lengo lake ni kwamba tuongeze mapato katika mapato yasiyotokana na Kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba Watanzania tukiimba wimbo mmoja tutafika safari yetu tunayoitaka, lakini tukienda kwa safari hii ambayo kila mmoja anataka aimbe anavyotaka mwenyewe tutashindwa kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie, naomba tuangalie kwamba tunapaswa tujenge kesho, kesho ilio bora kwa Watanzania, unaijengaje kesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kujenga kupitia Miradi ambayo lazima Watanzania tuisimamie, lakini katika Mpango huu naomba tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba tujipange kidogo, hasa kwa Wakulima, Mkulima analima zao lake akijua kwamba akishavuna aweze kuuza, na ndiyo maana ya kuweka mnyororo wa thamani, lakini vilevile kumfanya Mkulima apate tija na Kilimo chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mkulima anapolima na ningeomba sana liingie hili katika Mpango unaokuja, Mkulima anapolima awe na hakika ya kupata bei ya mazao yake ili hii Mkulima imtie moyo wa kuweza kuzalisha zaidi na tuongeze tija katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mkulima wa pamba ameuza pamba toka mwezi wa tano mpaka leo hii hajalipwa pesa yake, halafu unataka mwaka aanze kufanya Kilimo tena kwa ajili ya mwaka kesho, hii si dalili njema, ninaomba sana wasimamizi ndani ya Serikali lisimamieni hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuna suala la soko huria lakini kama Serikali lazima itoe *guarantee* kwa Mkulima huyu au mazao yote, iwe ni Pamba, Korosho, Katani, Chai na mazao mengine yote ili Mkulima apate tija kile ambacho anataka kukizalisha, lakini pili Viwanda hivi vitajiendeze namna gani. Lazima na *guarantee* ya mazao yanayotokana na Kilimo chetu, lazima tufungamanishe sasa ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lazima tulifanye kwa nguvu zote kwamba sasa hivi Mtanzania yule yule afungamanishwe na maendeleo ili aweze kupata maisha ambayo tunayohitaji, leo hii mkulima tumemsaidia sana kumwekea miundombinu ya barabara, umeme, maji, upande wa afya, sekta ya afya, upande wa elimu, Serikali inatoa fedha nyingi kila mwaka, lakini yote haya sasa lazima yasimamiwe vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mwanzoni nilikuwa sikuelewi elewi, lakini nimeanza kwamba sasa kumbe wewe ni msimamizi mzuri sana wa raslimali za Watanzania na ni mzaalendo, na hata Katibu Mkuu wako wa Fedha na Naibu wa Waziri wako kweli mnafanya ya kizalendo. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Mwambie shikamoo...

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na ninaambiwa hapa niseme shikamoo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nakwambia hapa niseme shikamoo Mheshimiwa Waziri wa Fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Ofisi ya Msajili wa Hazina, endelea kuimarisha, inachangia pato lisilotokana na kodi zaidi ya shilingi trilioni moja sasa hivi kwa mwaka. Ninaomba iwe ni ofisi ambayo inapewa kila aina ya *support* kusudi itekeleze majukumu yake inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma, yafuate misingi ambayo imewekwa na kufanya hivyo nina imani tutawenza kufufua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema kwamba Watanzania tunaanza kumwelewa Mheshimiwa Rais, tuendelee kumwelewa. Makandokando mengine haya, naomba Watanzania tupate fursa ya

kuyazunguza, lakini kama ni Mpango, tuuzungumzie Mpango kwa malengo na maslahi mapana ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, hayupo; Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, ajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu wa mapendekezo ya Mpango kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na jambo moja ambalo ni la msingi sana, kutoa pongezi kwa Rais wetu mpPENDWA Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa maelekezo kwa zile Halmashauri mpya kuhamia kwa wananchi ili kutoa huduma kwa wananchi kwa ujirani sana na hatua hizo zimeshaanza kutekelezwa. Nampngeza sana, nami Halmashauri yangu imeshahama tayari na wanafanya kazi vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nawapongeza wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kwa kujandikisha kupiga kura. Wananchi wamejiandikisha vizuri kabisa na uchaguzi ambao wenzangu wanaongelea wa kidemokrasia, nadhani kwenye Jimbo langu hakuna tatizo na tunakwenda vizuri kabisa. Nawapongeza sana wananchi wa Jimbo langu la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni mapendekezo ya Mpango, nami napenda nitoe mapendekezo yangu. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri sana. Wameandaa Mpango sana. Nimesoma Mpango wiki nzima na bahati nzuri niko kwenye Kamati ya Bajeti, tulikuwa tunajadili pamoja, hakuna kitu walichoacha, kila kitu

kimeandikwa vizuri na ukisoma vizuri, maana kuna utekelezaji wa miaka mitatu iliyopita na kuna mapendekezo ya Mpango kwa miaka inayokuja, wamefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mapendekezo kwa *TARURA*. *TARURA* wanafanya kazi vizuri na ukiangalia tafsri ya *TARURA* ni Wakala wa Barabara Vijijiini na Mijini; na ukiangalia kazi zao wanavyofanya, kwa upande wa mijini na wenyewe wanajenga hata barabara za lami. Ukienda vijijiini wanajenga barabara zile za kokoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ile bajeti, tukisema tunawapa asilimia 30, fedha ile haitoshi. Sasa hivi nchi nzima barabara zinazoangaliwa ni zile ambazo ziko chini ya *TARURA*. Wenzetu wa *TANROADS* walifanya kazi vizuri, kutekeleza ile sera ya kuungalisha barabara za mikoa na mikoa na wilaya na wilaya. Walifanya kazi nzuri sana na barabara nyingi sana zimejengwa. Ukiangalia Tanzania nzima sasa hivi barabara za mikoa na wilaya zinapitika vizuri, lakini tuna tatizo kubwa kwa barabara za vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye Mpango huu mpya, naiomba Serikali ijielekeze sana kuiangalia *TARURA* kuweza kuiongezea uwezo ili wafanye kazi vizuri sana na tuhakikishe kwamba barabara za vijijiini zile zinapitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa hospitali katika wilaya 67. Ni jambo jema sana. Hizi hospitali zitasaidia sana wananchi na zimeenda kasi. Sasa zile hospitali ambazo Serikali ilitoa fedha, naweza nikasema kwamba wameshafikia asilimia kuanzia 80 mpaka 90 kwa kujenga, lakini wakimaliza tu kujenga, naiomba Serikali itazame, zile hospitali zianze kutumika mara moja haraka sana ili *value for money* ioneokane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijenga hospitali zikakaa muda mrefu bila kutumika, itakuwa ni kazi bure. Kwa *speed* hiyo tulijojenga, iende sambamba sasa na ununuzi wa vifaa vyta hospitali, kuwaandaa watumishi ili waweze kufanya kazi katika hospitali zile. Kuna hospitali nyingi sana tuna tatizo la

vifaa vya hospitali. Kwa mfano, hata pale Mjini Mafinga, tuna tatizo moja la *X-Ray*, hospitali haina *X-Ray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hospitali mpya hizi maandalizi ya vifaa yawepo ili kuhakikisha tunapomaliza majengo yote, watumishi na vifaa viwepo ili hospitali ianze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu. Serikali mwaka huu mmefanya vizuri sana. Kila ukimwuliza mwanafunzi anasema nimepata asilimia 100, asilimia 80, asilimia 90, Serikali imefanya vizuri, mikopo imeongezeka sana kwa wanafunzi. Nilikuwa nasoma hapa, hao wanafunzi wa mwaka wa kwanza karibu 41,000 wameshapata mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe pendekezo moja, kuna wanafunzi ambao wako mwaka wa pili na wa tatu, kuna wengi walikosa mikopa na mwaka huu hawajaomba; sasa wameona wenzao wamepata mikopo ambao wamekuja kwa mwaka huu na wale wa mwaka wa pili na wa tatu wana vigezo vya kupata mkopo; sasa kufuatana na bajeti ilikuwa kidogo, hawakupata mikopo. Naiomba Serikali, basi wale wa mwaka wa pili na wa tatu waruhusiwe sasa, wafungue dirisha ili waombe na wenyewe ili wale ambao walikopa waweze kukopeshwa tena. Kuna wanafunzi wanapata taabu sana wa mwaka wa pili na wa tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni changamoto hasa na tumejadili sana hata kwenye Kamati ni kumiliki akaunti za benki. Wananchi, hasa kwenye vikundi, imetuletea shida sana kwenye vikundi. Unaweza ukaona kikundi kina akaunti au kijiji kina akaunti, sasa kwa sababu wanaweka fedha kwa msimu, akiwa na fedha ndiyo anakwenda kuweka, kama hawana fedha wanaweza wakakaa hata miezi sita hawajaweka fedha. Kwa hiyo, akaunti yao inaonekana iko *dormant*. Sasa ikiwa *dormant*, wakipata fedha, wakitaka kwenda kuweka tena kwa mara

ya pili (hata kwenye Vyama vya Ushirika hili tumeliona), wanasema akaunti yako imefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni tatizo kubwa sana, naomba, Waziri wa Fedha, awaambie mabenki, mtu akiweka akaunti yake, kwa nini ifungwe? Kwa sababu akianza *process* upya, anasema nenda kachukue barua kwa Mwenyekiti, nenda sijui kwa Mtendaji, anaanza *process* upya. Hiyo inawakatika tamaa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi Wabunge kwa mfano hata kwenye Mfuko wetu wa Jimbo ukitaka kupeleka fedha kijijini kwa ajili ya maandalizi ya kununua vifaa kule kijijini, utasikia akaunti imefungwa. Kwa hiyo, unashindwa kupeleka fedha. Wananchi kule kuji-*organize* kuanza upya *process* inachukua muda mrefu na vijiji vyetu viko mbali sana na benki. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko kwamba benki vile kusema kwamba akaunti ziko *dormant*, hilo neno lisiwepo. Mtu ameonyesha *ID number* tu, akaunti inakuwa *active*; akiweka hata shilingi 10,000/= au shilingi 20,000/=, akaunti inakuwa *active* kwa sababu *details* zote zinakuwepo pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine, Benki Kuu walifanya kitu kizuri sana katika kupunguza riba kwa mabenki. Ile ilikuwa kwamba, wanapunguza riba kwa mabenki ili mabenki yale yaweze kukopesha wananchi. Tunajua kule kwa wananchi kuna wafanyabiashara wadogo, wafanyabiashara wakubwa na wafanyabiashara mtu mmoja mmoja. Sasa *impact* kwa wananchi bado haijaonekana, yaani ile juhudhi ya Serikali kuwaambia kwamba wapunguze riba kwa mabeki ili ilete *impact* kwa wananchi na wenywewe wale mabenki ya biashara yapunguze kwa wananchi, hayajafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi bado wanalamika, riba ni kubwa sana, kubwa sana. Sasa na hilo naomba Serikali ifuatilie ili kuondoa malalamiko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine, nimeona kwenye Mpango, umekaa vizuri kuhusu masuala ya

umeme vijiji. Serikali imefanya kazi vizuri sana. Hata kwenye vijiji vyangu vyote, upimaji, *survey* imeshafanyika, ingawa kuna vijiji vingine bado kupeleka nguzo. Kuna sehemu nyingine nguzo zimelala tu chini, wananchi wanalamika. Naomba twende *speed*. Tumesema mwaka 2021 vijiji vyote vitakuwa vimepata umeme, vitongoji vyote vitakuwa vimepata umeme. Sasa ile kasi tuliyokuwa tumeanza nayo mwanzo iendelee, maana tunaona sasa Makandarasi kama wanafifia hivi, wananchi wanashindwa kuelewa vizuri. Tuwahamasishe wafanye kazi vizuri, kwa sababu Serikali ina lengo zuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanasema kwamba, kuna vijiji wanapita bila kupingwa kwenye uchaguzi. Kwa nini wasipite bila kupingwa kama wanaona umeme uko tayari pale? Wananchi wanachotaka ni huduma kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaona mtandao wana maji, wako wako *site*. Ingawa kuna chagamoto ya maji, lakini watu wako *site*, sasa mtu atapinga nini? Wanaona majengo ya shule ambayo yalikuwa hayajaisha yanamalizika, wanaona Vituo vya Afya vinajengwa, Hospitali za Wilaya zipo; sasa mtu atalalamika nini? Barabara zinajengwa, sasa utalalamika kitu gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa, tuishauri Serikali kuongeza *speed* ya kuhakikisha kwamba mazingira bora kwa wananchi yanakuwepo kujenga hospitali, kujenga Vitu vya Afya, kujenga Zahanati, barabara, umeme; tukiimarisha haya, ndio maisha bora kwa jamii tunayoyataka. Tukisema kupunguza umasikini, maana yake tunaangalia vitu kwa jamii viro? Hospitali zipo? Madawa yapo? Hivi vitu vinafanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ni *process*, usije ukasema utafika siku moja, ukasema sasa tumetosheka kila kitu tunacho. Hata ukienda nchi za wenzetu zilizoendelea, barabara wanajenga mpaka leo. Hata ukienda pale Uingereza, London penyewe pale mjini, barabara mpaka leo

hii wanajenga. Ukienda hata Marekani, barabara mpaka leo hii wanajenga. Kwa hiyo, hii ni *process* ya muda mrefu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda wangu umeisha, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, atafuatiwa na Martha Umbulla, Mheshimiwa Salum Rehani, ajandae.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mionganini mwa wanaochangia Mpango. Awali ya yote naishukuru sana Serikali, namshukuru Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa kuleta Mpango mzuri ambao unaonyesha dira ya maendeleo yetu. Katika mpango huu yapo ambayo yametekelezwa na Serikali, kimsingi tunaipongeza sana Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada kubwa sana ambazo amezifanya za kuboresha vitu vingi ambavyo amevileta katika nchi yetu. Kwenye Mpango amezungumzia suala la miundombinu. Tumeshuhudia Serikali ikiboresha eneo la miundombinu kwa ujenzi wa barabara karibu nchi nzima. Haya ni maendeleo makubwa sana na unapotaka maendeleo, kwanza rahisisha shughuli za kuwafikia wananchi, lakini bado Serikali tumeona ikitekeleza miradi mikubwa, wameboresha viwanja vya ndege karibu 11 ambavyo tunategemea vitarahisha sana shughuli ya uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali imenunua ndege ili ziweze kukuza Sekta ya Utalii, lakini kutoa huduma kwa wananchi. Serikali bado imeendelea kuwaona wananchi hasa wale wa chini, imekuja na Mpango wa kununua au kujenga meli mpya kwenye maziwa makuu; Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Haya ni maendeleo makubwa sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Ziwa Victoria kuna ujenzi wa meli mpya itakayokuwa na uwezo wa kuchukua abiria 1,200 na karibu tani 400 za mizigo. Eneo hili watakuwa wamewasaidia sana wananchi wa kanda ya ziwa, ambao kwa kipindi kirefu walikuwa wana shida kubwa ya usafiri wa majini. Vile vile kuna ukarabati wa meli ya *MV. Victoria*, haya ni maendeleo makubwa sana katika kipindi kifupi. Tunaona mipango ambayo iliwasilishwa na Serikali ikitekelezwa kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, bado kwenye hiyo hiyo Sekta ya Uchukuzi, Serikali imeamua kusaidia au kupanua ujenzi wa bandari pale Dar es Salaam. Bandari yetu ilikuwa na uwezo mdogo, leo hii tunashuhudia maendeleo makubwa sana ya upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam na tumeshuhudia nchi yetu ikipokea sasa meli kubwa ambazo zinatua kwenye bandari yetu na kupakua mizigo ambayo haikutegemewa huko nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna Bandari ya kule Mtwara, imepanuliwa. Tunaamini eneo lile la Kusini nalo litakuwa katika huduma kubwa ya maendeleo katika nchi yetu. Bado kuna upanuzi wa Bandari ya Tanga, ambayo nayo ipo katika Mpango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la Kanda ya Ziwa Victoria, kuna ujenzi wa kivuko kikubwa karibu kilomita tatu kutoka Busisi ambacho kitatoa huduma kubwa sana kwa wananchi. Maeneo haya ni Serikali inatekeleza kwa ajili ya kusaidia wananchi kukuza uchumi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali, lakini tumeona mapinduzi makubwa sana katika nchi yetu. Ili uweze kuendelea, tunahitaji miundombinu na nishati ya umeme. Mheshimiwa Rais kwa nia nzuri ameamua kujenga bwawa kubwa la umeme katika Mto Rufiji; bwawa lile maarufu kwa kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Hili litakuwa ni eneo ambalo litawasaidia wananchi wote katika nchi yetu. Ninaomba hizi jitihada tuziunge mkono na tuangalie maeneo

mengine ambayo yalisaha ulika yaweze kupelekewa miradi ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kilimo. Tukitaka kuwasaidia wananchi walio wengi, baada ya Serikali kuweka miundombinu, karibu maeneo yote, sasa Mheshimiwa Dkt. Mpango elekeza mawazo yako ukuze Sekta ya Kilimo ambayo inawaguza wananchi wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili natoa ushauri, kwanza Serikali ianze kufikiria kutoa ruzuku kwenye mazao ya korosho, pamba, chai, tumbaku na yale mazao makubwa ambayo yanatuletea fedha za kigeni kwa wingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ye yote ile iliyoendelea inawasaidia sana wananchi hasa wakulima kuweza kushindana kwenye ushindani. Pale mazao yanapokuwa yameanguka, lazima Serikali iweze kuwasaidia hawa wananchi wapate nguvu, lakini wasiposaidiwa watakuwa na maeneo mabaya ambayo yatawafikisha kutokufanya kazi na kuachana na hayo mazao ambayo yalikuwa yakiwaingizia kipato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zao la pamba ambalo linazalishwa wilayani kwangu. Zao la pamba wananchi walilichukulia kwamba ni zao ambalo ni sasa lingewatoa kwenye umasikini na wamezalisha kwa kiwango kikubwa na pamba nzuri, kuzidi hata ile iliyokuwa inazalishwa ambako imetoka mbegu zake maeneo ya ukanda wa ziwa, lakini mpaka sasa wakulima bado hawajauza pamba, iko majumbani kwao. Naomba eneo hili mkalifanyie kazi, mboreshe ili wananchi waweze kupata huduma inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao lingine ni tumbaku. Nchi yetu ilikuwa inapata fedha nyingi kuititia zao la tumbaku. Kwa bahati mbaya sana mwaka huu yapo makampuni ambayo yalikuwa yananunua tumbaku kwenye nchi yetu kampuni kama *TLC* lakini imeacha kununua zao hili. Tuna mikoa zaidi ya 12 inayozalisha zao la Tumbaku ukiwemo na Mkoa wa

Kigoma ambapo Mheshimiwa Waziri ametoka wananchi hawana mahali ambapo watauza tumbaku walizokuwa wanazalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashauri sasa Serikali iangalie eneo la Kitengo cha Masoko, kwenye masoko bado hamjapaangalia. Tunahamasisha kilimo lakini kuwatafutia wakulima masoko bado Serikali haiajawekeza kwa kiasi cha kutosha. Niombe eneo hili nendeni mkalifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuboresha eneo la masoko pia ni muhimu kuboresha mazao ya chakula ambapo mkiwasaidia hawa wakulima na mkawawekea mazingira mazuri ya masoko kilimo ni eneo ambalo litaajiri wananchi wengi na Serikali itakuwa inanufaika kupitia huduma mbalimbali na kodi zitakazokuwa zinatokana na upatikanaji wa fedha. Tunaomba sana hapa Serikali mkapafanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tunapenda kushauri Serikali ni kwenye ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Muda umekwisha, ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Salum Rehani atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu, Mheshimiwa *Engineer Gerson Lwenge* ajiandae.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika Mpango huu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Menejimenti yote ya Wizara kwa kuleta huu Mpango ambao tunataka tuone ni dira ambayo inaweza ikatuondoa tulipo na kuelekea kwingine ambako tutakuwa na taswira mpya ya kuifanya Tanzania hii iwe ni nchi ya uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nataka nizungumzie maeneo yale ambayo tunayaita *economic tools* ambapo tukiyatumia tunaweza kufikia kwenye huo uchumi wa kati mbali na miundombinu na miradi ya kimkakati ambayo inatekelezwa na Taifa. Sina tatizo na miradi yote ya Serikali iliyokuwa imeipanga ya kimkakati, ile miradi mikubwa kwamba itakuwa ni sehemu ya kuifanya Taifa hili liweze kuelekea huko kwenye uchumi wa kati lakini napenda zaidi niishauri Serikali kwani kuna maeneo lazima tutoe lawama kwa kitu ambacho hakijafanyika ili Serikali wasikilize ushauri ambapo utasaidia kutoka kuliko kuendelea kubaki kama tulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya mifugo, Tanzania mbali ya kuwa ni nchi ya pili kwa mifugo lakini bado sekta hii hajifanikiwa. Nimepitia Mpango huu hapa sijaona maeneo thabiti ambayo tunaweza kufaidika na mifugo lakini na fursa ya ufugaji hapa nchini. Kuchunga tunakochunga hakutusaidii chochote *hardly* pengine tunakwenda kwenye 2% or 3%. Tunataka tuone Wizara ya Mifugo imejikita katika kuhakikisha kwamba inapeleka mfumo wa *artificial insemination* vijijini ili kubadilisha aina ya ufugaji kwanza, ili kubadilisha ng'ombe waliokuwepo kule ambao wana uwezo wa kutoa nusu lita na lita moja ya maziwa na waende kuwa ng'ombe ambao wanatoa zaidi ya lita 20 na kuendelea, hilo linawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunataka kuona maziwa haya ambayo yanaweza kuzalishwa ndani ya nchi yanafaidisha nchi. Biashara ya maziwa wenzetu wa Zimbabwe ni sehemu ya uchumi wao mkubwa sana na kwa kipindi kile ilikuwa unachangia zaidi ya asilimia 12 lakini sisi Watanzania tumekuwa ni sehemu ya wanunuzi wakubwa

wa maziwa kutoka maeneo ya Zimbabwe na sehemu nyingine wakati ndani ya nchi hapa tunaweza kuzalisha maziwa na kuuza na kuyatumia kwa matumizi yetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali na Wizara ya Mipango tuwe na Mpango madhubuti na maalum wa kuhakikisha kwamba tunaweza ku-*handle* maziwa ambayo yako zaidi ya lita milioni mbili kwa siku yanayozalishwa yageuzwe kuwa bidhaa ambazo zinatumika katika maeneo yetu mbalimbali. Mimi niseme wazi nasikitika sana na mfumo wa biashara ya kupokea maziwa mengi sana kutoka kwa majirani zetu kuingizwa ndani ya nchi kuliko maziwa yanayozalishwa hapa nchini. Ni kitu gani ambacho kinatushinda kuweza kuwa na viwanda ambavyo vinaweza kuchakata maziwa ambayo yako hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu *handling* yake ni gharama, sasa Serikali pamoja na miradi mikubwa ambayo inaifanya ielekeze nguvu sasa katika eneo hili ambapo *raw material* yake ipo ndani ya nchi ya kutosha na tuache mfumo huu uliopo sasa. Nafikiri iwekwe kodi maalum kubwa ya kudhibiti uingizwaji wa maziwa kutoka nje ili watu waweze kutumia maziwa yaliyoko hapa nchini. Mkiwaliza watu wa Mifugo, hata jana nilionana na Profesa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo bado anasema hakujawa na *engagement* ya fedha ambazo zinakwenda kutengeneza mitamba ya kutosha ambapo tutaisambaza katika maeneo yetu mbalimbali na kubadilisha taswira ya ufugaji kuwa wa kisasa zaidi kuliko kuendelea kuchunga ambapo tunasababisha ugomvi wa wakulima na wafugaji uliokuwa hauna sababu wakati njia rahisi ya kutumia teknolojia ya kisasa ya ufugaji ipo na hatujaitumia. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, vilevile nilikuwa naangalia Mpango Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa mara ya tatu niseme kwamba bado hatujatumia bahari iliyokuwepo ndani ya nchi hii. Katika dunia hii watu wote wanatushangaa, Mheshimiwa Dkt. Mpango kinachonuma zaidi nilipata fursa ya kwenda Comoro kama miezi mitatu iliyopita. Comoro wao kama kisiwa wameanza kufaidika na *blue sea* sisi kwetu bado.

Tuna sufferna 0.4 imekimbiza meli zote, tuna fursa ya kuifanya *SUMATRA* iweze kukusanya karibu shilingi milioni 40 kwa kila meli iliyokuja kufanyiwa *inspection* ya kwenda kwenye uvuvi wa bahari kuu na zaidi ya meli 200 hapa duniani zinataka kuja kuchukua leseni lakini kuna kikwazo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niombe Serikali badala ya kuelekeza nguvu zaidi katika maeneo ya uwekezaji wa reli, umeme na uwekezaji mwingine wowote mkubwa i-*engage* pesa maalum kwa ajili ya *blue sea*. *I will promise* Bunge hili ndani ya miaka miwili *break even* ambayo itapatikana kutoka katika bahari hakuna sehemu yoyote ya uchumi ambayo itaweza ku-*compete*. Fedha ziko nyingi na ziko nje nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunachosema hapa *demand/inaendelea* kuongezeka na kinachofanyika duniani tunatengenewa *artificial fish* siyo samaki halisi tunaoletewa kwenye makontena hapa na Watanzania tunakula wakati tuna bahari ya kutosha na bado tumeomba kuongezewa eneo la *nautical miles* 150 la nini sasa kama hatuvekezi? Kama tumeomba tuongezewe eneo basi tuiombe Serikali iwekeze katika bahari ile tuoneshe kwamba na sisi tunayo *potential/ya kuitumia* bahari hii iliyokuwepo hapa na Mungu aliyotujalia tuweze kuleta mabadiliko chanya na tuende kwenye uchumi wa viwanda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana kama wanavyoweza kufaidika watu wa Namibia kwa zaidi ya asilimia 11 ya uchumi wao *GDP* wanategemea samaki ambaao wanapenya tu katika mlango mmoja wa *Mozambique Current* kwenda katika eneo la Namibia na wanaweza kupata fedha ambazo zinaweza kuongezea *GDP* zaidi ya asilimia 11. *South Africa* pamoja na uchumi wao mkubwa lakini 8% wanapata fedha kutoka bahari, tunachoshindwa Tanzania ni nini? Mimi nimeuona Mpango halisi huu hapa lakini sijaona mkakati ambaao tunaelekea kwenye bahari kuu na kuifanya nchi hii ni sehemu ya nchi ambazo zinauza samaki nchi za nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala zima la kilimo. Nchi hii tumejaliwa kuwa na maeneo mengi mengi ya kilimo lakini pamoja na kuwepo na miradi ya *SPD*// ambayo mpaka sasa hivi hatujaona uendelezwaji wake na kufanya kazi katika maeneo ambayo yanaweza kuleta mabadiliko hayo chanya. Bado mwendo wake nauona unasuasua ingawaje mradi sasa hivi umeshafikia miaka miwili. Ushauri wangu uko hapa, Serikali inatakiwa iwekeze kwenye kilimo cha umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niombe Serikali kitu kimoja, mfumo uliopo hivi sasa wa kujenga *canal irrigation* hautusaidii kitu, unakula fedha nyingi na unachukua muda kumalizika na wakandarasi ndiyo sehemu ambayo wanaweza kupata pesa bila ya sababu.

Kwa ushauri wangu mimi tuzuie fedha zote zinazokwendwa kwenye *canal irrigation* ambapo tunaweza tuka-save zaidi ya asilimia 70 kwa kutumia *pipe irrigation* ambazo unaweza kuwekeza kwa muda mfupi tu. Wiki mbili tu unajenga zaidi ya hekta 200 au 100 kwa kutandika mabomba ukaweza kuhifadhi maji na akatumia maji ambayo hayawezi kupotea. Tukutumia mfumo huo tuaweza ku-control ile wanaita *Evapo-transpiration* lakini vilevile *contamination* ya wadudu, maradhi, magugu na vitu vingine vyote tutaeppuka. Hiyo ndiyo teknolojia tunayotaka twende na dunia huko ndiko iliko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuendelea kujenga mitaro kwa mawe na saruji ambayo baada ya muda wakandarasi wanapiga hiyo pesa na hakuna kinachoendelea, niseme wazi kwamba huko sioni kama kuna tija na hakuwezi kutufikisha. Tutumie njia rahisi ambapo tutaweza kuzalisha na kuyatumia maji *effectively* kuliko hivi sasa. Kwa hiyo, niiombe sana Serikali katika mipango yetu yote hizi *billions of money* zinazokwenda kwa ajili ya kutengeneza *canal* za *irrigation* tuelekeze kwenye *pipe irrigation* ambacho ndicho kilimo cha kileo zaidi kuliko huku tunakokwenda.

MWENYEKITI: Muda wako umeisha Mheshimiwa.

MHE. SALUM MWINYI REHANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Miraji Mtaturu atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Gerson Lwenge, Mheshimiwa Justin Monko ajiandae.

MHE. MIRAJI J. MTATURU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ambayo iko mezani. Kwa sababu leo itakuwa ni siku ya kwanza kuchangia naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na uhai wa kuweza kuchangia hoja hii ambapo naishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake ya Wizara nzima, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kuandaa na kutuletea Mpango huu ambao kwa kweli ni Mpango ambao umeendelea kutuonesha dhamira ya dhati ya Serikali katika kuwaletea Watanzania maendeleo. Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza na naomba niseme tu kwamba tutaendelea kutoa ushauri ambao utakuwa na tija kwa ajili ya kuleta maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mpango wenyewe huu unakwenda kumalizia katika Mpango wa Miaka Mitano ninajua mambo mengi yako dhahiri ambayo yameonekana yameshafanyika. Zaidi niseme tu kwamba kuwa na Mpango ni jambo moja lakini kuusimamia na kuutekeleza ni jambo la pili. Kwa hiyo, sisi kwenye hili tunawapongeza kwa sababu tumekuwa na Mpango na sasa tunaona namna ambavyo kwa muda huu unaenda kumalizika mwaka wa tano mafanikio makubwa katika maendeleo ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwa kweli kwa dhati kabisa kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa namna ambavyo ameonesha dhamira ya dhati katika kuhakikisha kwamba anawaletea

wananchi maendeleo. Najua kwamba utashi wake ndiyo ambao unatupa hata jeuri au inaipa jeuri Serikali kuhakikisha inafanya kazi vizuri kwa sababu tumekuwa tukipata fedha ya kuweza kutekeleza miradi hiyo. Tunaweza tukawa na mipango mizuri sana isipowezeshwa itakuwa ni kazi bure na itakuwa inabaki kwenye vitabu kama ambavyo tumekuwa tukiona baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba maeneo mengi ambayo naweza kuyasema ni yale ambayo nasema kwamba tumeanza kuona dhamira ya Serikali katika kukusanya mapato. Unaweza ukawa na mpango mzuri lakini ukawa hauna fedha lakini ukiwa na mpango mzuri ikiwa ni pamoja na kukusanya mapato inakusaidia wewe kuhakikisha kwamba unatimiza malengo ambayo yako mbele yetu. Jambo kubwa ambalo ni vizuri tukalisema ni dhamira ile ya kusimamia na kuzuia mlanya yote ya kukwepa kodi katika nchi yetu. Siyo hivyo tu ni pamoja na kusimamia na kutokomeza kabisa rushwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya maeneo ambayo tulikuwa tunateseka sana ni pale ambapo baadhi ya watumishi ambao hawana dhamira njema wamekuwa hawafanyi vizuri sana katika kusimamia mapato yetu. Kwenye hili, naomba niipongeze Serikali kwa namna ambavyo imesimamia na imeendelea kuongeza mapato katika nchi yetu yanayonifanya tuweze kutekeleza mipango ambao tunajipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote nieleze sasa yale ambayo yanaonekana waziwazi. Tumeona namna ambavyo tunaboresha sana miundombinu ya barabara ambayo kwa kweli imekuwa ndiyo nguzo kuu ya uchumi wa nchi yetu. Niseme hapa katika mpango nimeona namna ambavyo mwaka huu ambapo tunaelekea kwenye bajeti tutaenda kujikita katika kuongeza fedha ambazo zinakwenda kuongeza uwezo wa kujenga barabara zetu ikiwa ni barabara za lami na madaraja makubwa na kadhalika. Niombe tu kwamba haya ambayo yamepangwa

basi yawekwe vizuri kwa ajili ya kutoa fedha ili tuweze kuona miradi hiyo inaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tumeona reli ya *SGR* inajengwa. Ni dhamira ya dhati tuliamua kama Taifa na leo tunavyoona *speed* ni kubwa sana tuko zaidi ya asilimia 60 ya utekelezaji wa mradi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba hii nayo itakuwa ni kichocheo muhimu katika uchumi na usafirishaji wa mizigo ikiwa ni pamoja na kupunguza bei ya bidhaa sokoni. Bei ya bidhaa ikipungua maana yake itamsaidia mwananchi wa kawaida kuweza kupunguza mfumuko wa bei kwa sababu bei itakuwa chini katika usafirishaji wa mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote hatutaacha kusema maneno machache kwenye sehemu ya uboreshaji wa ununuzi wa ndege. Hili jambo tusipolisema na dhamira ya dhati ikaonekana maana wengine wamekuwa wakipotosha eti wanathaminisha ndege wanasema vingejengwa vituo vya afya kadhaa. Niseme tu kama Taifa lazima tuamue nini cha kufanya, huwezi kusema unaogopa kununua shati jipya kwa sababu huna utoshelevu wa kubadilisha kula mboga, huwezi kuogopa hilo, lazima uamue kwamba ndege zinazonunuliwa zinaenda kuongeza uwezo wetu wa kuweza kuhudumia sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tumekuwa tukiona na tukilalamika na mimi nimekuwa nikiwaona Waheshimiwa Wabunge wanasema ndani ya Bunge kwamba haiwezekani watalii washukie Kenya waletwe kwa magari kuja kwenye mbuga zetu na baadaye warudi wakapandie Kenya kwa shirika lingine la ndege. Leo tunapata ndege maana yake tuna uwezo sasa wa watalii wale wote kushuka kwenye viwanja vyetu ndani ya nchi yetu na wanakwenda moja kwa moja kwenye utalii. Utalii ndiyo sekta ambayo inaongoza katika mapato katika nchi yetu. Kwa hiyo, tunapoboresha Shirika la Ndege maana yake moja kwa moja tunaiboresha hii sekta ya utalii ambayo ndiyo inaleta fedha nydingi ambapo mwisho wa siku itajenga vituo vya afya, shule, itaboresha elimu bure pamoja na mambo mengine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa lazima tujivunie kwa sababu lazima nchi isonge mbele kwa kuwekeza kwenye mambo makubwa. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa sisi wenyewe tunafanya mambo makubwa lakini hatujui kama tunafanya mambo makubwa. Hii haitatujenga kama Taifa, Watanzania tuipende nchi yetu kwa yale makubwa mazuri tunayoyafanya. Tofauti ya vyama vya siasa isitufanye tuondoke kwenye reli, lazima tujivunie na sasa hivi tunaona *ATCL* wanafanya vizuri, Mheshimiwa Waziri anayehusika na sekte hii yupo pale kwa kweli kazi inafanyika vizuri na sisi kama Waheshimiwa Wabunge ni lazima tuunge mkono juhudui kubwa hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza maelezo haya, kabla muda wangu haujaisha, nitoe maneno machache ya ushauri kwenye suala la kilimo. Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, lakini naomba na mimi nileze kidogo, asilimia 80 ya wananchi wetu wanafanya kilimo. Kama kweli tutaweza kuwekeza kwa dhamira ya dhati katika kilimo itasaidia sana kutuungezea pato la Taifa lakini itasaidia uchumi wa mwananchi mdogo kule chini chini, wakati wa kutegemea msimu wa mvua umepitwa na wakati, tuungeze nguvu katika kilimo cha umwagiliaji na zaidi tuungeze uwezo wetu wa kusimamia miradi hiyo na itoe matokeo, katika baadhi ya maeneo tuweze kuvuna zaidi ya mara mbili ili tukipata mapato ya kutosha kwenye eneo hili itasaidia hata mapato ya ndani katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri zetu nydingi zinategemea mazao katika mapato, tukiwekeza kwenye kilimo naamini kabisa tutaenda kuongeza uwezo wa wananchi wetu na kipato chao katika kaya. Kipato cha kaya kikifanikiwa ndiyo tutasaidia kwenda kwenye huo uchumi wa kati ambao tunausema kwa sababu tunaangalia na tunatathimini namna ambavyo mwananchi anajipatia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka kwenye eneo hilo, niende sasa kwenye eneo la pili la miundombinu. Tunaamini zile barabara kubwa zile *trunk roads* zinajengwa

kwa kiwango cha lami, lakini nieleze kidogo kwenye barabara ambazo ziko chini ya *TARURA*. *TARURA* wamekuwa wakitengewa fedha kidogo sana naamini wanataka kujenga madaraja, wanataka kuongeza uwezo wa ujengaji wa barabara zao, lakini fedha wanazopata ni ndogo sana hazina uwezo wa kututoa pale na ile dhamira ya kuanzisha hii *agency* haitakuwepo kama hatutawapa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana kwenye mpango huu naona imeguswa na imewekwa, lakini naona kabisa namna ambavyo mfano kama Wilaya ya Ikungi pale, zipo barabara ndevu lakini nyingi hazijawahih kutengenezwa, ni barabara za asili kama mapalio, naamini kabisa Mheshimiwa Waziri ananielewa ninavyoeeleza hayo, kwa sababu *TARURA* huwa wanaleta maombi yao na yamekuwa wakipata fedha kidogo sana, wakati ambapo barabara hizi zikijengwa zitasaidia kusogeza mbele suala la kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimalizia kwenye eneo la umeme juhudzi naziona ni nzuri sana, nipongeze sana Serikali kwa namna ambavyo wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa umeme kwa kupitia miradi ya *REA*, tatizo kubwa ambalo naliona lipo kwa wakandarasi, wakandarasi wamekuwa hawatekelezi miradi kulingana na mikataba yao, wakandarasi wengine wanalamikiwa hata na wafanyakazi wao, hivyo inasababisha kufifisha juhudzi za kuwapelekeea wananchi umeme, kwenye eneo hili ni vizuri Serikali kupitia Wizara husika waweze kusaidia kuhakikisha kwamba wananchi wanapatiwa umeme mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ndogo ambayo ipo pia ni maeneo yale ambayo wanasema kwamba wanapelekewa umeme kwenye vijiji lakini wanapelekewa vijiji ambavyo viko pale pale *centre*, umeme hauendi mpaka kwenye vitongoji. Inawezekana dhamira ya Serikali ni hiyo, lakini imekuwa tunavuka baadhi ya vitongoji, jambo hili linatuweka kwenye wakati mgumu ambapo tunakosa majibu, wakati hamu ya wananchi ya kupata umeme ni ya hali ya juu. Baada ya maneno haya, naomba

tu niendelee kusema CCM hatujakataa kuingia uwanjani, tuko tayari, lakini naomba pia na wao wafuate mwongozo uliowekwa ili waingle uwanjani wakiwa salama. Huwezi kuingia uwanjani huna viatu wakati wenzako wanaingia na viatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer Gerson Lwenge* atafuatiwa na Mheshimiwa Justin Monki, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele ajiandae.

MHE. ENG. GERSON H. LWENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa hotuba yake nzuri na kwa kuwasilisha Mpango mzuri ambao ni sehemu wa miaka mitano ambao tulipitisha Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nampongeza sana. Pia naomba nipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ambayo kila moja anaona. Kwabhiyo hata kama yupo anayebeza, anabeza kwa sababu zake, lakini vitu vinavyofanyika vinaonekana wazi wazi. Kwa hiyo niwapongezeni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitajikita zaidi kwenye suala la miundombinu. Katika Mpango ambao umewasilishwa, vipaumbele vimewekwa lakini katika hivi vipaumbele kuna eneo la ujenzi wa barabara za lami na nchi nzima tumeona barabara za lami zinajengwa, barabara za mkoa na barabara kuu zinazounganisha kati ya mkoa na mkoa. Naomba sana kwamba ili kusudi barabara hizi ziweze kudumu ni lazima tuweke mkakati mzuri wa matengenezo yake, tuongeze bajeti ya matengenezo ya barabara hizi ili isiwe barabara inajengwa baada ya miaka miwili inafumuliwa tena inajengwa nyingine. Ili tuweze kufikia maeneo yote ya nch, tuwe na mkakati mzuri wa matengenezo. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iongeze fedha kwenye fuel levy kwa ajili ya kupeleka Wakala wa *TANROADS* na *TARURA* ili barabara zetu ziweze kujengwa. Tumeanzisha *TARURA*

tukiamini kwamba *TANROADS*ilifanya kazi nzuri, lakini ilifanya kazi nzuri kwa sababu tuliweka fedha ya kutosha ya matengenezo, kwa hiyo tuweke nguvu sana kwenye matengenezo ya barabara zetu hizi ili ziwe *sustained*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba Mkoa wetu wa Njombe ukumbukwe kwenye barabara kuu ambazo ni muhimu ambazo hazijawekwa kujengwa kwa lami, kwa mfano, kwa barabara inayotoka Njombe Makete ifike mpaka Mbeya na barabara kutoka pale Ramadhani ifike mpaka Lyai iunganishe na barabara kuu ya *Tazam highway*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba sana katika mpango huu tumeona kwamba kuna usambazaji wa umeme vijiini na kazi nzuri sana inafanyika. Mwaka jana nimechangia, nilisema katika usambazaji wa umeme maeneo mengi ambayo hata yameshajengewa miundombinu yamekuwa siyo *sustained* kwa sababu kwa muda mfupi unakuta nguzo zimeanguka au *transform* zimeungua, lakini sababu kubwa kwamba hatuweki bajeti kubwa ya matengeneo. Kwa hiyo naomba sana tuweke bajeti kubwa ya matengenezo katika miundombinu ya umeme ili kwamba hivi viji vyote zaidi ya 8,000 vimepata umeme, basi tufurahie kwamba tumeshapata maendeleo unajua mambo ya miundombinu ni kama mishipa ya damu ndiyo uhai wa mwili wa mwanadamu, basi miundombinu hiyo tuliyoijenga kwenye Taifa letu ni lazima iwe imewezeshwa sana hasa kwenye eneo hili la matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nichangie ni suala la Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Mwaka jana pia wengi wamechangia, mradi huu tumezungumza miaka mingi toka mwaka wa kwanza wa Mpango huu tumezungumza Mradi wa Liganga na Mchuchuma lakini mpaka leo hakuoneshi *progress* naamini katika hii sehemu ya mwisho ya mpango huu tutaweka nguvu kubwa, kama ni mradi wa kielelezo, kama ni mradi wa kipaumbele tuone utekelezaji wake tusiishie kusikia bado hatujalipwa hata fidia, sasa huu mradi kama kweli tumeamua kuujenga tuweke nguvu. Taifa lolote haliwezi kuendelea

kama hakuna chuma, chuma ndiyo malighafi mama ya viwanda na sisi ndiyo tunasema tunajenga uchumi wa viwanda, kwa hiyo lazima tuweke nguvu katika kutekeleza Mradi huu wa Liganga na mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka nilizungumzie, ni sekta ya afya. Ni kweli Rais wetu ameamua kwa nguvu kubwa kujenga vituo vya afya 352 na hospitali za wilaya 69, ni jambo jema mimi nampongeza sana. Naamini kabisa Taifa lolote lazima na watu wenyewe afya uwe na mpango mzuri kwa ajili ya kuhakikisha Watanzania wanapata tiba iliyoboreka, kwa hiyo naomba sana awamu hii katika Mpango huu pia tuweke nguvu kujenga vituo vingi zaidi. Wananchi wetu katika maeneo mengi tuliwhamasisha, wamejenga zahanati kila kijiji na maeneo mengi kila kata wamejenga vituo vya afya, lakini wamefika mahali wamekwama, yale maboma yamebaki mpaka leo miaka mitano, miaka sita, basi katika mpango huu naomba sana Serikali iangalie namna ya kukamilisha hata angalau hizo zahanati wananchi wamechangia waendelee kuwa na imani na Serikali ili angalau kila kijiji wawe wanaweza kupata huduma ya msingi katika hili suala la afya. Pia huu mpango wa bima ya afya kwa wote, naomba uletwe haraka, ni jambo moja nzuri litakalowasaidia Watanzania kupata afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kuongelea, ni suala la kujenga uwezo wa makandarasi wetu ndani najua miradi mingi inatekelezwa na makandarasi na miradi mikubwa mingi tunatoa kandarasi kwa makandarasi kutoka nje. Tulianzisha Bodi ya Usajili wa Makandarasi ili tuweze kuinua uwezo wa wakandarasi wetu. Ile bodi ina kazi ya kusajili pia na kufuta, kama kuna wakandarasi hawaendi sawasawa na maadili ya ukandarasi ile bodi ina uwezo wa kufuta, kwa hiyo tusiogope kuwawezesha wakandarasi wetu kupata kazi. Suala kubwa ni kwamba kwa sababu naamini kabisa wapo wakandarasi ambao wapo daraja la kwanza, kwa maana kwamba kazi yoyote ile inaweza hata ile *Stiegler's gorge* lingeweza kujengwa kujengwa na wakandarasi wetu wa daraja la kwanza, kinachohitajika ni kuwasimamia na kwamba pale ambapo

wakandarasi wamefanya kazi, wawe wanalipwa kwa wakati. Wengi wameshindwa kuendelea na kazi ya ukandarasi ni kwa sababu Serikali imekuwa inachelewa kuwalipa kwa kazi ambazo wamekuwa wamefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama anakaa miaka miwili, miaka mitatu hajalipwa baadaye tunaanza kusema yule mkandarasi ni mwizi kumbe hajalipwa, kwa hiyo naomba Serikali jambo hili ijaribu kuangalia ili wakandarasi wetu na kwa kweli tutafurahi sana kama kila kazi itafanywa na wakandarasi wetu wa ndani. Nadhani hata ukienda China sehemu kubwa ya wakandarasi wanaofanya kazi kwao kule ni wao wenyeche wa China, hakuna Watanzania wanafanya kazi kule China. Sasa na sisi Taifa letu la uchumi wa viwanda lazima tufike mahali kazi zote zifanywe na wakandarasi wetu wa wazalendo ili tuwezeshe Mfuko huu utoke kutoka Serikalini uende kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni suala la kilimo. Ni kweli tunajenga uchumi wa viwanda, lakini uchumi wa viwanda kama hatujainua kilimo, hautakuwa na manufaa kwa sababu tunajenga reli sawa, lakini mazao ya kupitisha pale yatatoka wapi. Kwa hiyo ni lazima tuwe na mkakati wa kutosha kuhakikisha kwamba kilimo chetu kinakua. Tuwe na pamba ya kutosha ya kuitoa Mwanza kuleta bandarini na tukauza nje, tuwe na chai ya kutosha na mazao mengine ambayo tumeweka ni ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nafikiri jambo lingine la kuangalia ni katika kuwezesha wakulima wetu wapate mbolea kwa wakati, lakini mbolea kwa bei elekezi ambayo Serikali imeshaianzisha, naipongeza mpaka sasa wanakwenda vizuri lakini nafikiri tufanye vizuri zaidi, tuangalie yale maeneo ambayo yalikuwa ni matatizo basi sasa hivi tuweze kuyaboresha ili wananchi wetu wapate mbolea kwa wakati na mbegu ili kilimo hiki kiweze kukua. Pia tusaidie wakulima hawa kupata soko kama wenzangu walivyosema, soko limekuwa ni tatizo, mwaka juzi mahindi yalikuwa yanauzwa kwa Sh.20,000 kwa gunia leo yanauzwa kwa

Sh.80,000 kwa gunia, napongeza sana hali hiyo. Hii inatokana na masuala ya tabia nchi, kwamba mikoa mingi haikuweza kupata mavuno ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuweke nguvu katika kujenga miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji, hatutaweza kukuza kilimo kwa kutegemea mvua na miaka hii nimeona mvua inapungua mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, niombe Serikali katika Mpango huu tuweke fedha za kutosha kwenye kilimo cha umwagiliaji, tumekuwa tunaweka fedha lakini hazitoki, naomba awamu hii ya mwisho wa Mpango huu zitoke fedha za kutosha, tuone utekelezaji wa kilimo cha umwagiliaji, naamini kabisa ndiyo mkombozi mkubwa wa kutufikisha katika uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii.
(*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Justin Monko, tutamalizia na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi ya kuweza kuchangia katika mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka wa 2020/2021. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri pamoja na timu yote na nipongeze Serikali kwa ujumla wake ikiongozwa na Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna ambavyo imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo katika bajeti iliyopitia na bajeti hii ambayo inaendelea sasa ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona yako mafanikio mengi katika miradi mingi ya kielelezo ukiwepo Mradi wa umeme wa *Stiegler's Gorge* au bwawa la Mwalimu Nyerere, tumeona kwenye *standard gauge*, ununuzi wa ndege, uboreshaji wa miundombinu, lakini zaidi sana katika sekta ya afya tumeona juhudu kubwa sana za ujenzi wa hospitali za

wilaya, lakini na vituo vingi vya afya ambavyo kwa kweli vitakwenda kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi pia tumeona mchango wa Serikali hii katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali ambayo yameongezeka kwa kiasi kikubwa na inatusaidia sana sisi katika kutekeleza mipango, ukizingatia kwamba mipango mingi sasa ya Serikali tunaipanga kwa kutumia fedha zetu za ndani. Mfano, katika mapendekezo haya ambayo yapo, katika fedha za mpango wa maendeleo zaidi ya bilioni 12.6 za bajeti ya maendeleo zaidi ya trilion 10.1 zitakuwa sasa zinatokana na fedha zetu za ndani. Kwa hiyo tunaipongeza sana Serikali kwa juhudi kubwa ambayo imefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichangie katika sekta mbalimbali katika kuboresha Mpango wetu wa Maendeleo wa mwaka 2020/2021, nikianzia na sekta ya afya, kama nilivyosema juhudhi kubwa imefanyika katika Serikali hii ya Awamu ya Tano, lakini niombe sana katika Mpango huu kazi tulioifanya kwa mfano kwenye vituo vya afya, pamoja na wingi wa vituo vya afya tulivyoifanya ukilinganisha na idadi ya Watanzania zaidi ya milioni 55 waliopo sasa, juhudhi kubwa bado inatakiwa katika eneo hili. Pia tujue kwamba bila kuwa na afya njema hata kazi zetu na mipango yetu ya maendeleo haiwezi kutufikisha vizuri. Kwa hiyo niiombe sana Serikali na Mheshimiwa Waziri waangalie namna ambavyo wataongeza vituo vya afya. Ushauri wangu katika hili ni kwanza kukamilisha maboma ambayo yamekwishaanzishwa na wananchi wenyewe. Awamu zilizopita ikiwemo Awamu ya Nne ya Mheshimiwa Kikwete tulianza, wananchi wamejitelea sana katika ujenzi wa maboma ya vituo vya afya na maboma mengine kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya, kwa mfano katika jimbo langu, yapo boma katika Kata yetu ya Ngimu lakini nydingine Makuro ambayo yamekaa kwa muda ya miaka 10, wananchi hawa wametoa nguvu zao, lakini mpaka leo maboma hayo hayajaweza kukamilika na kwa kweli wananchi wamekuwa wamezidiwa na ukamilishaji wa

maeneo hayo kutokana na mipango mingi ambayo tunawapelekea, ukizingatia kwamba kwa kila fedha za Serikali zinazokwenda asilimia 20 ya nguvu za wananchi inahitajika huko. Kwa hiyo niombe sana Serikali ifanye mpango wa makusudi kama ilivyofanya kwenye sekta ya elimu tuweze kukamilisha maboma haya ambayo yapo katika nchi nzima na wananchi walishajitolea katika kuyajenga ili kusudi tuweze kuboresha huduma za . Tunahitaji afya bora na hasa tunahitaji kuzuia vifo vya wa kina mama na watoto wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye sekta ya maji; sekta hii ni muhimu sana, kwa kweli tunao uwezo wa kufanya kila kitu, lakini tunaweza tukashindwa kuishi bila maji. Tumewekeza sana katika maeneo mengi, tumewekeza vizuri katika miundombinu, sasa hivi tunaendelea kuwekeza katika miundombinu ya umeme, tunaendelea kuwekeza katika maeneo mengine, lakini maji ambalo ni hitaji la msingi la maisha ya binadamu kwa kweli bado tumekuwa na nguvu kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia katika bajeti ya maji, imekuwa ni kidogo sana na haina uwezo wa kututoa hapa tulipo. Tunajua llani ya Chama cha Mapinduzi inataka angalau kwa upande wa vijijini tufikie asilimia 85 mpaka kufikia mwaka unaokuja. Sasa hivi tunaongelea chini ya asilimia 65, utaona kazi hiyo ni ngumu, kazi hiyo ni kubwa, kwa hiyo niombe sana, zitafutwe fedha za maji. Mwaka jana tulikuja na ombi hapa la kuongeza shilingi 50, lakini ombi hilo halikukubaliwa na sisi hatupingani na hilo, lakini madhali vinaweza vikapatikana vyanzo vingine, suala la maji ni la muhimu sana wewe mwenyewe ni shahidi, Mheshimiwa Rais alipotembea kila mahali alipokwenda ni maji, maji, maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji linawagusa sana akinamama ambao ndio wazalishaji wakubwa na wanatumia muda mwingu sana kwenye kutafuta maji na tunaona kwamba takwimu tunazokuwa nazo zinaweza zisiwe za kweli kwa sababu tunadhani kwamba kisima kimoja kinakwenda pale kama kinasema kinahudumia wananchi

250 au wananchi 500 au 600, hizo ndizo takwimu tunazokuwa nazo, lakini utakuta wengine wapo zaidi ya mita 400 ambayo ndiyo sera yetu au Awamu hii ilikuwa imejiwekea, kusogea huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe sana Serikali, ukienda katika miradi ya vieleleze Sekta ya Maji sio sekta ya muhimu, sio sekta ya kipaumbele. Sasa hili halitupi sisi nafasi ya kuweza kutenga fedha nyngi kwenye kuboresha miundombinu ya maji. Niombe Mheshimiwa Waziri tulipe kipaumbele cha kwanza kabisa sasa hivi kwenye bajeti inayokuja hii ya mwaka 2020/2021 ili tuweze kuwatua akina mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata walioko mijini bado hawajapata maji ya kutosha, bado kumekuwa na urasimu mkubwa. Ukiangalia hata katika Mkoa wa Dar es Salaam shida ya maji bado ni kubwa, katika majiji yote shida ya maji bado ni kubwa. Kwa hiyo niombe sana Wizara hii iangalie na niombe sana Sekta ya Maji iwe ni moja ya sekta za kipaumbele katika Taifa letu. Tunaweza hata tukapunguza kwenye maeneo mengine; tunaweza tukaishi bila lami, tunaweza tukaishi bila miundombinu bora huko lakini hatuna uwezo wa kuishi bila maji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lipo katika kilimo; Sekta ya Kilimo inaa jiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania, wengi wao – asilimia 90 – wanatoka vijiji ambako mimi ni mwakilishi wao, lakini pia wako wakulima ambao wanaishi mijini. Bado mpango wa Serikali haujatenga fedha za kutosha katika kuboresha Sekta ya Kilimo, bado tunahitaji kuongeza fedha, tunahitaji kuongeza uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika mpango ambao umewasilishwa sasa, fedha nyngi zinazotegemewa ni hizi za mpango wa kuendeleza Sekta ya Kilimo ya Awamu ya Pili (*ASDP II*). Fedha hizi hazitoshi. Fedha hizi zina maeneo maalum, yako mazao mengine ambayo hayawi-covered kabisa kwenye mpango huu. Mpango huu wa *ASDP II*

wenyewe umelenga zaidi kwenye mazao yale ya kimkakati ambayo utakuta ni korosho, pamba, kahawa, chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yapo mazao mengine ambayo kwa kweli yanahitaji yapewe kipaumbele; tuna mazao ya mafuta kama ufuta, alizeti mchikichi, karanga na maeneo mengine. Haya yanahitaji kupewa kipaumbele kwa sababu tunajua kwamba nchi yetu inatumia fedha nyngi, zaidi ya bilioni 410 katika kuagiza mafuta ya kula kila mwaka. Fedha hizi ni nyngi sana, tusipowekeza katika kilimo hatuwezi kuwasaidia wananchi wetu. Huku ndiko wananchi wetu walio wengi tunakotoka sisi wote waliko. Kwa hiyo, niombe sana Sekta ya Kilimo ipewe umuhimu na kipaumbele cha kwanza pia ili kuweza kuboresha maisha ya wananchi wetu kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukumbuke kwamba nchi yetu sasa tunakwenda na tunakwenda kwenye uchumi wa kati ambaao utaongozwa na uchumi wa viwanda. Viwanda hivi vitahitaji malighafi za kutoka mashambani, viwanda hivi vitahitaji malighafi za mifugo, viwanda hivi vinahitaji malighafi kutoka kwenye uvuvi. Sasa tusipowekeza katika maeneo haya tutajikuta kwamba hatuwezi kufikia malengo yetu vizuri na ndoto ya Mheshimiwa Rais wetu ya kutufikisha uchumi wa kati 2025 haitaweza kutimia kwa sababu ya uwekezaji mdogo katika Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia Sekta ya Kilimo ni pamoja na mifugo vilevile. Tumeona zipo changamoto nyngi, na niipongeze sana Wizara ya Mifugo, sasa hivi wamekuja na utaratibu wa uhimilishaji wa mifugo ambaao unawasaidia wafugaji wetu kuwa na mazao bora zaidi.

Kwa hiyo, niombe sana uwekezaji uongezwe katika sekta hizi ikiwa ni pamoja na Sekta ya Uvuvi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Kengele ya pili imegonga Mheshimiwa.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante sana, tutamalizia na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai, na pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ili na mimi niweze kushiriki katika kuchangia hotuba ya Waziri wetu mpandwa, Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kusema naunga mkono hoja asilimia 100 kwa 100, na nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake yote kwa ujumla kwa utendaji wake mzuri wa kazi. Pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu na wataalam mbalimbali wa Wizara hii kwa umahiri wao wa utekelezaji wa mipango yote ambayo tumeanza nayo ya miaka mitano. Hongereni sana kwa *consistency* ambayo mmekuwa nayo. Tumeanza na mpango wa mwaka wa kwanza, wa pili, wa tatu, sasa wa nne; utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika sekta mbalimbali za vipaumbele hauna mashaka unatekelezwa kwa kiwango ambacho kinaridhisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa reli ya kisasa uko vizuri, ujenzi wa Bwawa la Umeme la *Stiegler's Gorge* au Bwawa la Mwalimu Nyerere unakwenda vizuri; upanuzi wa bandari zetu unakwenda vizuri, ujenzi wa meli katika maziwa makuu; Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa mambo yanakwenda vizuri; ujenzi wa Daraja refu kabisa ambalo litakuja kuwa la kihistoria la Kigongo – Busisi mpango unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa ndege za kisasa umeendelea kutekelezwa vizuri; yote haya yamo katika mipango yetu ambayo tumeanza nayo tangu uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano ulipoingia madarakani. Miradi mbalimbali inatekelezwa, mpango wa elimu bila malipo kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne unatekelezwa bila wasiwasi na Watanzania wanafurahia; uboreshaji wa huduma za afya na wenyewe unatekelezwa

na tunashukuru na ninaipongeza Serikali sana kwa sababu Watanzania sasa afya zao zinaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno haya napenda sasa niendelee kuchangia katika baadhi ya maeneo. Eneo mojawapo ambalo ninapenda kuchangia ni kuhusiana na suala zima la ujenzi wa wilaya hizi mpya na mikoa mipyä. Wilaya yangu ya Mbogwe ni miiongoni mwa wilaya mipyä; niipongeze sana Serikali kwa sababu imeendelea kufanya kazi zake vizuri inatupatia pesa tunajenga makao makuu ya wilaya kwa maana ya halmashauri na ofisi za mkuu wa wilaya na tumepewia pia pesa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali, naomba tu Serikali iendelee kutupatia pesa ili tuweze kukamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa uhakika kabisa na wa thabitii wa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma na ninaamini kabisa kila mmoja ni shuhuda kwamba ofisi mbalimbali za Wizara mbalimbali zimejengwa kuititia mipango hiihii ya Serikali ambayo tunaendelea kuitekeleza. Niombe Serikali iendelee na mkakati wake sasa wa kumalizia ujenzi wa Uwanja wa Msalato ili kwamba Makao Makuu yetu ya nchi yaweze kufikika kwa kufikia hata ndege na usafiri wa kimataifa kutoka mataifa mbalimbali ya nje. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kuyapandisha mapori ya akiba kuwa hifadhi za Taifa; Mapori ya Kigosi, Mto Ugala, Selous, Ibanda, Burigi Chato, mapori haya yanahitaji sasa uwekezaji mkubwa. Tuiombe Serikali itenye pesa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu katika mapori haya ili sasa huduma za utalii ziweze kufanyika kwa wepesi zaidi na uchangiaji wa Pato la Taifa kuititia hii Sekta ya Utali iweze kuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kilimo ninapenda kuishauri Serikali iendelee kuwekeza katika viwanda vyâ utengenezaji wa mbolea kwa sababu Watanzania walio wengi wanashiriki katika shughuli za kilimo,

na kwa maana hiyo tuiombe Serikali iwekeze zaidi katika kuvutia wawekezaji wa viwanda vya mbolea ili uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara uweze kuimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ikijitosheleza kwa chakula ninaamini kabisa hata ukuaji wake wa uchumi utakuwa ni wa uhakika zaidi kwa sababu wazalishaji mali wenyewe watakuwa wana nguvu za kutosha na kwa hakika wataweza kufanya uzalishaji katika sehemu mbalimbali za Serikali na hata katika viwanda na maeneo mbalimbali ya uzalishaji mali watafanya kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tena kuishauri Serikali sasa kuwekeza zaidi katika eneo la upimaji wa ardhi. Nchi yetu ina tatizo kubwa la ujengaji holela katika miji yetu, niombe kabisa Serikali ilippe kipaumbele suala zima la upimaji wa ardhi katika maeneo mbalimbali ya miji inayochipukia na miji mikubwa ambayo tayari tunayo katika nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia habari ya maendeleo hatuwezi kuzungumza maendeleo bila kutaja suala zima la mawasiliano kwa njia ya barabara. Niombe Serikali iendelee kutoa pesa katika wakala mbalimbali ikiwemo TANROADSna TARURA ili ujenzi wa barabara za lami kuunganisha maeneo mbalimbali kwa maana ya mikoa na makao makuu ya wilaya uendelee kwenda kwa kasi inayokubalika. Pia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini na wenyewe ujengewe uwezo, vitafutwe vyanzo mbalimbali vya mapato ili kuweza kuisaidia wakala hii ambayo ni changa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba REA inafanya vizuri kwa sababu imekuwa na chanzo cha uhakika cha tozo ya mafuta. Tumejikuta kwamba sasa hiki chanzo kinausaidia sana Wakala wa Umeme Vijijini kuweza kufanya mageuzi makubwa sana ya upatikanaji wa umeme katika vijiji vyetu na kwa maana hiyo ninaamini kabisa kwamba hata TARURA ikiwezekana kitafutwe chanzo kingine

ambacho kitauvwxyzesa kuwa na pesa za uhakika za kuweza kutekeleza miradi yake kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala mwingine ni Wakala wa RUWASA ambao na wenyewe ni Wakala wa Maji Mijini na Vijijini. Wakala huu na wenyewe ni wakala ambao ndio umeanza, niiombe Serikali na yenyewe iendelee kuujengea uwezo wakala huu ili uweze kusambaza maji kwa uhakika kwa Watanzania ili waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba watu wakipata maji safi na salama afya zao zitaimarika na magonjwa mbalimbali ambayo yanatokana na maji yanaweza yakazuilika tunaweza tukajikuta hata bajeti ya matumizi ya afya inaweza ikashuka kwa sababu kama tusipokuwa na wagonjwa wengi maana yake sasa hata mahitaji ya madawa yatapungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hao napenda kushukuru, ahsante sana kwa kunipata nafasi na Mungu awabariki.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Kuna mambo mawili; moja ni tangazo, lingine ni la kukumbushana. Nitaanza na tangazo linatoka Ofisi ya Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba ofisi imeshaanza kupokea maswali kuititia njia ya kielektroniki. (*Makofi*)

Sasa wako Waheshimiwa Wabunge ambao walituma nadhani kwa majoribio, yaani wakitaka kujua yanafika au hayafiki kwa hiyo waliandika mambo ambayo kidogo mengine hayajakamilika lakini wametuma kwa hiyo Ofisi imeniletea hapa ili niwaambie Waheshimiwa Wabunge mlichotuma kimefika.

Sasa kwa sababu tulielekezwa yale maswali wao hawawezi kuyafuta kwenye mtandao wako wewe, inabidi uingie ufute kwa sababu la sivyo wataweka sasa kwenye orodha kana kwamba kile ulichokuwa umetuma ndiyo swali lenyewe. Kwa hiyo, mnaombwa muingie ile sehemu ya maswali mfute yale maswali mliyokuwa mmetuma kwa majoribio kwa sababu kuna wengine wameandika Kichina hapa, wengine wameandika kabisa tunajaribu namna ya kuwasilisha maswali, kwa hiyo, inabidi sasa ukafute.

Uzuri kule imeandikwa kabisa na ni nani anayetuma kwa hiyo waliotuma Kichinachina na wenyewe wako hapa, waliotuma maswali ambayo yamekamilika lakini pengine inabidi wayatazame sasa vizuri ili liwe ni swali kamili pia wapo, orodha iko hapa. Kwa hiyo, mnaambiwa Ofisi ya Bunge imeshaanza kupokea na imeshapokea hata wale mliokuwa mnajaribu kwa hiyo, mnaombwa muende sasa ile sehemu ya maswali myafute kwa kuonesha kwamba hamkuwa mmekusudia yawe maswali kamili.

Lingine Waheshimiwa Wabunge la kukumbushana ni matakwa ya Kanuni yetu na namna ambavyo tumeletewa haya mapendekezo ili na sisi tushiriki kutengeneza huu mpango wa Serikali. Lakini michango mingi tunayoitoa haikidhi Kanuni yetu ya 94 inachotutegemea Bunge tufanye sasa ili kutoa fursa kwa Serikali kwenda kutayarisha mpango ambaao ndiyo utatoa mwongozo wa bajeti.

Tusipofanya hivyo mambo yale tunayotakiwa kuzungumza sasa tutaanza kuzungumza wakati wa kujadili bajeti na mpango wa wakati huo, na wakati huo ndiyo tunaanza kuona kama macho yamefunguka sana hivi tunaona na vyanzo vingine vya mapato. Wakati wa kusema hayo kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 94 ni sasa, ndicho tunachotarajiwa kufanya.

Ukiisoma, uzuri sasa hivi huna haja ya kubeba kwa hiyo iko humu; Kanuni ya 94 imesema kabisa mjadala wetu unatakiwa kujikita kwenye nini, na ukisoma 94(6) imeeleza kabisa mjadala unatakiwa kuwa kwenye mambo ya jumla

yanayohusu sera za kiuchumi na mambo kama hayo. Sisi wakati huu tunatakiwa kupendekeza vyanzo nya mapato; tunatakiwa kupendekeza vipaumbele. Serikali imeeleza ya kwake na vipaumbele vyake, sisi tunasema nini? Na je, sisi tunavyo vipaumbele tofauti? Na kama tunavyo sasa ndiyo wakati wa kusema, na kama tunavyo vyanzo nya mapato vitakavyoisaidia Serikali kutimiza malengo yake ambayo ndiyo wameleta sasa mapendekezo tunatakiwa kusema sasa.

Kuja kusema baadaye ndiyo maana tunaanza kusema Serikali imegoma kutoa hata nukta, ni kwa sababu tunasema wakati ambao sio. Serikali itaondoka hapa – haya yote tunayoongea ni kweli, kijiji chako hakina umeme ni sawa, Waziri wa Nishati atasikia, lakini Mheshimiwa Dkt. Mpango hicho anaandika pale lakini wala hatakitolea majibu hapa kwa sababu sicho ambacho Kanuni zetu zinamtaka afanye kipindi hiki cha Bunge la mwezi wa kumi na wa kumi na moja. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kanuni tunazo, wakati unaitwa jina kuchangia wewe pitia Kanuni yako ili ujipange unataka kuchangia kwenye hoja ipi kwa mujibu wa Kanuni zetu. Tukieleza kila mtu kwenye eneo lake, kila mtu sehemu yake Kanuni ya 94 haisemi, hayo tutakuja kuangalia Mheshimiwa Dkt. Mpango wakati huo yale tuliyomshauri sasa wameyazingatia, wameyatazama?

Tusipowashauri yale aliyoyleta yatakuja haya haya mwakani na wakati huo ndiyo tutaanza sasa ongeza 20 pale ongeza 50 pale, ongeza sijui 100 pale, inakuwa wakati wetu wa kushauri kwenye hilo umepita na hauwezi kuilaumu Serikali kwamba sasa mbona haisikilizi kwa sababu wakati wetu wa kushauri kuhusu mpango ni sasa kwa sababu Serikali imeleta mapendekezo haina mpango bado, imeleta mapendekezo.

Tusome Kanuni yetu Waheshimiwa Wabunge, hilo lilikuwa ni la kukumbushana kwa sababu siku tano zinakwisha punde na Mheshimiwa Dkt. Mpango atarudi nayo yale

aliyotuletea na sisi tunatarajiwa kuyaboresha na kuangalia mambo mengine ambayo yeye pengine hajayagusa.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, tarehe 07 Novemba, 2019, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.22 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 7 Novemba, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*